# SUNNAH NA ADABU 550

(Swahili)




Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal

**MUHAMMAD ILYAS**

**Attar Qadiri Razavi**

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِیْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰی خَاتَمِ النَّبِیّٖن

اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّیْطٰنِ الرَّجِیْمِ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ

# Sunnah na Adabu 550

## Ubora wa kumswalia Mtume Mtukufu ﷺ

Kipenzi chetu, Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Siku ya Kiyama hakutakuwa na kivuli kingine isipokuwa kivuli cha Arsh (kiti cha Enzi) ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Watu watatu watakuwa chini ya kivuli cha Arsh (kiti cha Enzi) ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.' Iliulizwa kwa unyenyekevu, 'Ya Rasuolallah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم! Ni nani hao watu?' Akajibu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

1. Mtu ambaye anaondoa wasiwasi wa Ummah wangu.
2. Mwenye kuhuisha Sunnah yangu.
3. Mwenye kuniswalia (kunitumia rehma na amani ) kwa wingi.

*(Al-Budu-rus-safirah, uk. 131, Hadithi ya 366)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِیْب   صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

Sayyiduna Imamu Dhahaak رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: “Mfano wa Sunnah duniani ni kama vile Pepo ilivyo katika Akhera. Yaani, kama vile atakayeingia Peponi katika akhera atakaa salama, vivyo hivyo mwenye kufuata Sunnah duniani atasalimika.”

*(Tafseer Qurtubi, juzuu ya 13, uk. 365)*

Sunnah na adabu 550 kuhusiana na mada tofauti zinawasilishwa. Usichukulie kila lulu ya Madani iliyowasilishwa hapa chini kuwa ni Sunnah. Kuna uwezekano kwamba lulu hizi za Madani zinaweza kuwa na maneno ya watangulizi wachamungu رَحِمَهُمُ اللّٰهُ badala ya Sunnah. Kumbuka hukmu ya kwamba hakuna amali inayoweza kutangazwa kuwa ‘Sunnah ya Mtume kipenzi’ isipokuwa inajulikana kuwa ni Sunnah kwa uhakika.

Wahubiri (wanaume na wanawake) wanaombwa kutaja Sunnah na adabu kutokana na mada yoyote iliyotolewa katika kijitabu hiki mwishoni mwa hotuba zao za Sunnah kulingana na hali. Na usome mistari ambayo imetolewa kabla na baada ya kila mada.

Enyi waja wa Rasuli! Mwishoni mwa hotuba, ningependa kutaja ubora wa Sunnah na kuwaeleza Sunnah chache na adabu. Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Mwenye kupenda Sunnah yangu amenipenda mimi, na mwenye kunipenda mimi atakuwa pamoja nami peponi. *(Ibn-e-Asakir, juzuu ya 9, uk. 343)*

*Seenah tayri Sunnat ka Madinah banay Aaqa*

*Jannat mayn parosi mujhay tum apna banana*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

# Sunna na Adabu 15 za Kutembea

1. Katika aya ya 37 ya Surah Bani Isra'iyl, Juzuu ya 15, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

وَلَا تَمْشِ فِی الْاَرْضِ مَرَحًا ۚ اِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْاَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُوْلًا ﴿۳۷﴾

*Wala msitembee katika ardhi kwa kiburi; bila shaka nyinyi hamtaipasua ardhi kamwe na hamtafikia milima kwa urefu.*

*[Kanz-ul-Iman (tafsiri ya Quran)] (Juzuu ya 15, Surah Bani Isra'eel, aya ya 37)*

2. Katika ukurasa wa 435 wa Bahar-e-Shari'at', juzuu ya 3, kuna Hadiyth iliyobarikiwa: Mtu aliyefunikwa na shuka mbili alikuwa akichechemea na alijivuna kwa kiburi. Alifanywa kuzama ndani ya ardhi; ataendelea kuzama mpaka Siku ya Hukumu.'

*(Muslim, uk. 1156, Hadithi ya 2088)*

3. Mtume wetu, kipenzi chetu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alipokuwa akitembea, baadhi ya wakati alikuwa akiushika mkono wa sahaba wake kwa mkono wake uliobarikiwa. *(Mu'jam Kabeer, juzuu ya 7, uk. 277, Hadithi ya 7132)*

4. Wakati Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akitembea, Yeye angeinama mbele kidogo kana kwamba anashuka kutoka kwenye sehemu ya juu.

*(Shumaail-ul-Muhammadiyyah lit-Tirmizi, uk. 87, Raqm 118)*

5. Usitembee kamwe kwa kiburi; kuvaa cheni ya dhahabu au chuma yoyote shingoni mwako, na vifungo vya mbele [za shati] vikiwa wazi kana kwamba ni kujionyesha. Huu ndio mtindo wa wasio na hekima, wenye kiburi, na warukao mipaka. Ni Haramu kwa wanaume kuvaa bangili na mkufu wa dhahabu

shingoni. Kuvaa mikufu mingine ya chuma au metali zingine pia hairuhusiwi.

6. Ikiwa hakuna kizuizi, tembea kando ya barabara kwa kasi ya kati. Usiwe na haraka sana hadi watu waanze kukutazama wakidhani kwamba anaenda wapi kwa haraka. Usitembee polepole sana mpaka watu wakufikirie kuwa wewe ni mgonjwa. Mtu asishike mkono wa kijana mwenye mvuto, kwa sababu kushikana au kupeana mikono au kumkumbatia ndugu yeyote wa Kiislamu kwa matamanio ni Haramu na kitendo cha kuelekeza Motoni.

7. Sio Sunnah kutazama huku na kule bila ya mahitaji ukiwa unatembea. Tembea kwa heshima na macho yako yawe yameangalia chini.

**KISA :** Sayyiduna Hassaan Bin Abi Sinaan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alikwenda kwa ajili ya Swala ya Idi. Aliporudi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه, mkewe akamuuliza: Umewaona wanawake wangapi leo? Akakaa kimya. Aliposisitiza, yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه akasema: Nilikuwa nikitazama vidole vya miguu (vya miguu yangu) kwanzia nitoke nyumbani mpaka nirudi kwako. *(Kitab-ul-Wara' ma' Mawsu'ah Imaam Ibn Abid Dunya, juzuu ya 1, uk. 205)*

سُبْحٰنَ اللّٰه عَزَّوَجَلَّ! Mawalii waliobarikiwa رَحِمَهُمُ اللّٰه hawakuangalia huku na kule pasipokuwa na dharura wakati wa kutembea, hasa pale paliposongamana, wasije wakamtazama asiyeruhusiwa na Shari'ah. Huu ulikuwa ni uchamungu wa mawalii wetu رَحِمَهُمُ اللّٰه. Hukumu ni kwamba ikiwa jicho lako litaangukia kwa mwanamke bila kukusudia na ukakwepa kutazama mara moja, hutakuwa na dhambi.

8. Haifai kutazama balconI au dirisha la nyumba ya mtu bila dharura.

9. Unapotembea au kupanda au kushuka ngazi, jihadhari kwamba viatu vyako havipigi kelele.

10. Ikiwa kuna wanawake wawili wamesimama au wanapita njia, basi usipite baina yao. Imekatazwa katika Hadiyth zilizobarikiwa. *(Abu Dawood, juzuu ya 4, uk. 470, Hadees 5273)*

11. Ni kinyume na adabu kutema mate, kupuliza pua, kuweka kidole ndani ya pua, kusafisha uchafu wa mwili wako kwa vidole vyako, kuweka vidole masikioni au kushika sehemu za siri n.k wakati unatembea, umekaa chini au umesimama mbele ya watu.

12. Baadhi ya watu wana tabia ya kupiga teke lolote linalowajia. Haya ni mazoea yasiyo na adabu sana. Pia kuna hatari ya mguu wako kujeruhiwa. Zaidi ya hayo, kupiga teke magazeti au masanduku, pakiti na chupa tupu za maji yenye maandishi juu yake pia ni ukosefu wa heshima.

13. Wakati wa kutembea barabarani ikiwa kivuko cha pundamilia au daraja la juu linapatikana, zitumie ili kuvuka barabara wakati wa trafiki.

14. Vuka barabara kwa kuangalia upande wa trafiki. Ikiwa uko katikati ya barabara na gari linakaribia, badala ya kukimbia, jaribu kukaa hapo kwani hii ni njia salama zaidi. Zaidi ya hayo, kuvuka reli nyakati ambazo kwa kawaida treni hupita ni kama kualika kifo chako. Yule anayeona treni kuwa mbali sana na kuvuka njia anapaswa kukumbuka hatari ya kunaswa na waya nk. na kuanguka kwa sababu ya haraka au kutojali na

kukandamizwa na treni. Tii sheria hizi; hasa kwenye vituo vya treni.

15. Tembea kwa dakika 45 ukifanya Zikr na ukariri Durood Shareef kila siku kwa nia ya kupata nguvu za kuabudu. اِنْ شَآءَاللّٰہ عَزَّوَجَلَّ, utabaki na afya njema. Njia bora ya kutembea ni kutembea kwa mwendo wa haraka kwa dakika 15 za kwanza, mwendo wa wastani kwa dakika 15 zinazofuata kisha haraka tena kwa dakika 15 za mwisho. Kwa kutembea kwa njia hii, mwili wote utatumika. اِنْ شَآءَاللّٰہ عَزَّوَجَلَّ, mfumo wa mmeng'enyo wa chakula utakuwa sawa, utakuwa salama kutokana na kuvimbiwa, gesi, uzito kupita kiasi, magonjwa ya moyo na maradhi mengine mengi اِنْ شَآءَاللّٰہ عَزَّوَجَلَّ.

Ili kujifunza maelfu ya Sunnah juu ya mada mbalimbali, nunua na usome vitabu vya Bahar-e-Shari'at Sehemu ya 16 ,na kitabu chenye kurasa 120 inayoitwa *'Sunnatayn aur Adaab,'* , kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah. Mojawapo ya njia bora za kujifunza Sunnah ni kusafiri na Madani Qafilah ya Dawat-e-Islami pamoja na waja wa Mtume Mpenzi.

*Lootnay rehmatayn qaflay mayn chalo*
*Seekhnay sunnatayn qaflay mayn chalo*

*Hongi hal mushkilayn qaflay mayn chalo*
*Khatam hon shamatayn qaflay mayn chalo*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِیْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Adabu 7 za

# Kuvaa Viatu

1. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Tumia viatu mara kwa mara kwa sababu maadamu mtu amevaa viatu, yuko sawa na mpanda farasi (huhisi uchovu kidogo) *(Muslim, uk. 1161, Hadithi nambari 2096)*

2. Tikisa viatu vyako kabla ya kuvivaa ili kama kuna wadudu au changarawe na kadhalika, vitoke.

   **KISA:** Inasemekana kwamba baada ya kuhudhuria karamu mahali fulani, mtu mmoja alipovaa viatu vyake, alianza kupiga kelele na mguu wake ukaanza kutiririka damu. Kwa sababu ya kuwa, wakati wa chakula, mtu alitupa mfupa uliochongoka ambao ulianguka na uliingia kwenye kiatu cha mtu huyo, naye alipovaa kiatu chake hakukitikisa kiatu hicho, kwa sababu hiyo, mguu wake ulijeruhiwa.

3. Ni Sunna kuvaa kiatu cha kulia kwanza kisha cha kushoto, na wakati wa kuvivua vua kiatu cha kushoto kwanza kisha cha kulia.

   Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Yeyote kati yenu akivaa viatu na aanze kuvivaa kwa mguu wa kulia, na akivivua aanzie mguu wa kushoto ili mguu wa kulia uweze kuwa ya kwanza kuvaa [viatu] na utakuwa wa mwisho wakati wa kuvivua.'

   *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 65, Hadithi ya 5855)*

   Imeelezwa katika *Nuzha-tul-Qaari:* Tanguliza mguu wa kulia unapoingia msikitini, na unapotoka msikitini weka mguu wa kushoto kwanza nje ya msikiti. Ni vigumu kufanyia amali juu ya Hadiyth hii [iliyobarikiwa] (amri ya kuvaa viatu kwa

utaratibu huo) wakati wa kuingia msikitini. Hivyo basi, Imam Ahmed Raza Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameeleza ufumbuzi wake ufuatao: Inapobidi kuingia msikitini, kwanza toa mguu wa kushoto kutoka kwa kiatu na uweke juu ya kiatu, kisha vua kiatu kutoka mguu wa kulia na uingie msikitini. Ukitoka msikitini toa mguu wako wa kushoto na uweke juu ya kiatu, kisha toa mguu wa kulia na uvae kiatu cha kulia, kisha vaa kiatu cha kushoto.

*(Nuzha-tul-Qaari juzuu ya 5, uk. 530)*

Sayyiduna Ibn-e-Jawzi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: “Mtu anayeanza na mguu wa kulia wakati wa kuvaa viatu na anaanza na mguu wa kushoto wakati wa kuvitoa, atasalimika na maradhi ya wengu. *(Hayat-ul-Haywan, juzuu ya 2, uk. 289)*

4. Wanaume wanapaswa kutumia viatu vya kiume na wanawake watumie viatu vya kike.

5. Mtu mmoja alimwambia Sayyidatuna Bibi Aaishah Siddiqah رَضِىَ اللّٰهُ عَنْهَا kwa unyenyekevu “Mwanamke fulani huvaa viatu (kama wanaume). Akajibu yeye رَضِىَ اللّٰهُ عَنْهَا, ‘Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amewalaani wanawake wa kiume (yaani wenye kufanana na wanamume).” *(Abu Dawood, juz. 4, uk. 84, Hadith 4099)* Wanawake hawapaswi kuvaa viatu vya jinsia ya kiume, bali wanaume na wanawake wamekatazwa kuigana kuhusiana na mambo hayo yote yanayotofautisha kati yao. Wanaume hawapaswi kuiga wanawake, wala wanawake hawapaswi kuiga wanaume.

*(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 3, uk. 422)*

6. Unapoketi, vua viatu vyako kwani kwasababu ya kitendo hiki, miguu hupata kupumzika.

7. Weka kiatu kilichotumika kwa njia sahihi ya kuelekea juu ikiwa imewekwa ikielekea chini. (Kutoweka kiatu kwa njia sahihi ya kuelekea juu hata baada ya kukiona ikiwa inaelekea chini ni moja ya sababu za ufukara).

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 18 za

# Kuketi/kukaa

1. Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰه عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: “Watu wanaokaa mahali fulani kwa muda mrefu na kutawanyika kutoka humo bila ya kufanya zikri ya Mwenyezi Mungu na kumswalia kipenzi chake, Mtume صَلَّى اللّٰه عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم watu kama hao hupata hasara. Mwenyezi Mungu akitaka atawaadhibu na akitaka atawasamehe.

*(Al-Mustadrak, juzuu ya 2, uk. 168, Hadithi ya 1869)*

2. Sayyiduna Ibn-e-‘Umar رَضِىَ اللّٰه عَنْهُمَا amesema: “Nilimwona Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰه عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akiwa amekaa katika uwanja wa Ka’aba tukufu kwa namna ya ihtiba *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 180, Hadithi ya 6272)*

3. Ihtiba ni mtindo wa kukaa ambapo mtu anakaa kwa kiuno chake na kuweka mikono yake kwa namna ambayo yanazunguka magoti yake. Kuketi kama hii inachukuliwa kuwa unyenyekevu.

*(Mullahs Al-Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 3, uk. 432)*

4. Ukiwa umeketi kama hivyo (ihtiba) au tuseme wakati wowote unapoketi, sehemu za siri hazipaswi kuonekana. Kwa hiyo, kwa

ajili ya kifuniko cha ziada, jifunike kwa shuka /kishale kutoka magoti hadi miguu. Ikiwa kamisi yako iko mpaka katikati ya miguu yako kwa mujibu wa Sunnah, sehemu yake ya chini inaweza kukupa pazia la ziada.

5. Baada ya kuswali Swalah ya Alfajiri, Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akikaa akiwa amekunja miguu yake yaliyobarikiwa mpaka jua linachomoza kabisa. *(Abu Dawood, juzuu ya 4, uk. 345, Hadithi ya 4850)*

6. Katika ukurasa wa 67 wa *'Jami' Karamaat-e-Awliya'*, juzuu ya 1, imeelezwa: "Imam Yusuf Nabhaani رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alikuwa na tabia ya kupiga magoti (yaani kukaa kama mtu anavyokaa katika Attahiyyat)."

7. Pia ni bora kukaa ukipiga magoti hata ukiwa hauko kwenye swalah.

*(Mirat, gombo la 8, uk. 90)*

8. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: "Miongoni mwa majalis (yaani mbele ya wengine) majlis (nafasi ya kukaa) yenye heshima kubwa ni ile ambayo ndani yake nyuso zinaelekea Qibla.

*(Mu'jam-e-Awsat, juzuu ya 6, uk. 161, Hadithi ya 8361)*

9. Sayyiduna Abdullah bin Umar رَضِىَ اللهُ عَنْهُمَا mara nyingi alikuwa akiketi kuelekea Qiblah. *(Al-Adab Al-Mufrid, uk. 291, Hadithi ya 1137)*

10. Kwa wahubiri na waalimu wakati wa kutoa hotuba na wakati wa kufundisha, ni Sunna kwamba wanapaswa kuweka mgongo wao kuelekea Qiblah ili wale wanaopata elimu kutoka kwao wawe wanaelekea Qiblah. Sayyiduna Allamah Hafiz Sakhaawi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: "Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa

akifundisha elimu au akinasihi akiwa amekaa kwa namna ambayo mgongo wake unaelekea Qibla ili wale waliokuwa wakipokea elimu au nasaha kutoka kwa Mtume wakae wakielekeza nyuso zao kwa Qiblah.” *(Al-Maqasid-ul-Hasanah, uk. 88)*

11. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم hakuwahi kukaa akinyoosha miguu yake iliyobarikiwa kuelekea yeyote katika mkusanyiko. Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم hakunyoosha miguu yake iliyobarikiwa kwa watoto wake, wala wake waliobarikiwa, wala watumwa na wala watumishi. *(Mirat, juzuu la 8, ukurasa wa 80)*

12. Sayyiduna Imaam A'zam Abu Hanifah رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: “Sijawahi kunyoosha miguu yangu kuelekea kwenye nyumba yenye baraka ya mwalimu wangu mheshimiwa Sayyiduna Hammad رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه kwa kumpa heshima (ingawa kulikuwa na umbali wa barabara chache kati ya nyumba iliyobarikiwa ya Sayyiduna Imam A’zam رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه na nyumba ya mwalimu wake mheshimiwa).”

*(Manaqib-ul-Imam al-A’zam Abi Hanifah, Sehemu ya 2, uk. 7, imerekebishwa)*

13. Kusogea kando kwa wale ambao wamefika hivi punde kumethibitishwa na Hadiyth iliyobarikiwa. Ni Hadiyth Na. 6 katika ukurasa wa 432 wa ‘Bahar-e-Shari’at’ juzuu ya 3. Mtu mmoja alikuja kwa Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم wakati yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alipokuwa amekaa msikitini. Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasogea kando. Mtu huyo kwa unyenyekevu akasema, ‘Ya Rasuolallah! (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) Kuna nafasi ya kutosha (yaani Bwana wangu (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) hakuna haja kwako ya kusogea). Mpenzi wetu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akajibu, 'Ni haki ya Muislamu kwamba ndugu yake akimuona, asogee kando kwa ajili yake.” *(Shu’ab-ul-Iman, juzuu ya 6, uk. 468, Hadithi ya 8933)*

14. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Ikiwa yeyote miongoni mwenu yuko kwenye kivuli na kivuli kikatoka juu yake na akawa katikati ya sehemu chini ya jua na sehemu yenye kivuli aondoke mahali hapo. *(Abu-Dawood, juzuu ya 4, uk 338, Hadithi ya 4821)*

15. A'la Hadrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: "Usikae kwenye kiti anachokaa kiongozi wako wa kiroho na mwalimu wako, hata wakiwa hawapo.

*(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 24, uk. 369-424, muhtasari)*

16. Unapokuja kwenye muhadhara au mkusanyiko, usijaribu kuenda mbele kwa kuruka mabega ya watu. Keti popote unapopata nafasi.

17. Unapoketi, vua viatu vyako. Miguu yako itapata kupumzika.

*(Al-Jami'-us-Sagheer, uk. 40, Hadithi ya 554)*

18. Ukisoma dua hii mara tatu baada ya kutoka kwenye mkusanyiko, dhambi zako huondolewa. Na mwenye kusoma dua ifuatayo katika mkusanyiko wa kheri na mkusanyiko wa dhikri, kwa ajili yake wema huo utapigwa muhuri. Dua hiyo ni kama ifuatavyo: 'سُبْحٰنَكَ اللّٰهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، لَآ اِلٰهَ اِلَّا اَنْتَ، اَسْتَغْفِرُكَ وَاَتُوْبُ اِلَيْكَ' *(Abu Dawood juzuu ya nne , kurasa 347, Hadithi 4857)* (Tafsiri: Wewe ni Msafi, Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Sifa njema zote ni kwako Wewe. Hapana apasae kuabudiwa kwa haki ila Wewe. Nakuomba msamaha, na ninatubu Kwako).

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب          صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

# Sunnah na Adabu 12 za Kuingia na Kutoka nyumbani

1. Unapotoka nyumbani kwako, soma dua ifuatayo:

‘بِسْمِ اللهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللهِ، لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللهِ’ Tafsiri: Kwa kuanzia na jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu, namtegemea yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu na hakuna nguvu wala uwezo bila Mwenyezi Mungu Mtukufu. *(Abu Dawood, juz. 4, uk. 420, Hadithi 5095-5096)* اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ kwa neema ya kusoma dua hii, utakuwa kwenye njia sahihi, utakaa salama kutoka kwa matatizo, na msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu utabaki na wewe.

2. Dua ya kuingia nyumbani:

اَللّٰهُمَّ اِنِّیْۤ اَسْئَلُكَ خَيْرَ الْمَوْلَجِ، وَخَيْرَ الْمَخْرَجِ، بِسْمِ اللهِ وَلَجْنَا، وَبِسْمِ اللهِ خَرَجْنَا، وَعَلَى اللهِ رَبِّنَا تَوَكَّلْنَا

*(Abu Dawood, juzuu ya 4, uk. 420, Hadithi ya 5095-5096)*

Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Nakuomba kheri ya kuingia na kutoka. Jina la Mwenyezi Mungu ndilo tuliloingia nalo (nyumbani) na jina la Mwenyezi Mungu ndilo tulilotoka nalo, na tukamtegemea Mola wetu Mlezi.

Baada ya kusoma hiyo dua, salimia watu wa familia yako, kisha toa salamu katika baraza la Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Baada ya hayo soma ‘Surah Al-Ikhlaas’. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ kutakuwa na baraka katika riziki yako, na utakaa salama kutokana na ugomvi wa familia / jamaa.

3. Sema salamu kwa maharim na muhrramaat (yaani mama, baba, kaka, dada, mke na watoto, n.k.) unaporudi nyumbani na kuondoka nyumbani.

4. Shetani anaingia nyumbani na mtu anayeingia nyumbani bila kusema 'بِسۡمِ اللهِ'.

5. Ikibidi uende kwenye nyumba iliyo tupu (hata kama ni yako), soma yafuatayo, 'اَلسَّلَامُ عَلَيۡنَا وَعَلٰى عِبَادِ اللهِ الصّٰلِحِيۡنَ' (rehema na amani za Mwenyezi Mungu zitushukie sisi na zishuke kwa waja wema wa Mwenyezi Mungu); Malaika watajibu salamu *(Radd-ul-Muhtar, juz. 9,uk. 682)* Vinginevyo, sema 'اَلسَّلَامُ عَلَيۡكَ اَيُّهَا النَّبِيُّ' (yaani ewe Mtume, swallallahu alayhi wa sallam, rehma na amani ziwe juu yako), kwa sababu roho iliyobarikiwa ya kipenzi Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ipo katika nyumba za Waislamu.

*(Bahar-e-Shari'at, juz. 3, uk. 453, Sharh-ul-Shafi` Lil-Qaari, juzuu ya 2, uk. 118)*

6. Unapotaka kuingia nyumbani kwa mtu sema hivi: 'اَلسَّلَامُ عَلَيۡكُمۡ Je naweza kuingia?'

7. Ikiwa hukupewa ruhusa, rudi kwa furaha. Labda mwenye nyumba hajakupa ruhusa kwa sababu makhsusi ya lazima.

8. Mtu Anapobisha mlangoni kwako, Sunnah ni kuuliza, 'Ni nani?' Aliye nje ataje jina lake, kwa mfano, 'Muhammad Ilyas'. Katika tukio hili, kama mtu atasema, 'Madina! 'Ni mimi!' au 'Fungua mlango', n.k badala ya kutaja jina lake, si Sunnah.

9. Baada ya kutaja jina katika jibu, simama mbali kidogo na mlango ili usione ndani ya nyumba wakati mlango unafunguliwa.

10. Ni marufuku kuchungulia ndani ya nyumba ya mtu. Nyumba zingine zilizo upande wa pili ziko kwenye kiwango cha chini. Kwa hivyo, watu kama hao wanapaswa kuwa waangalifu wakati

wa kuangalia nje ya balconi yao ili wasiangalie ndani ya nyumba kama hizo.

11. Ukienda kwa nyumba ya mtu, usikemee mpangilio wao. Hii inaweza kuumiza hisia zao.

12. Unapokaribia kurudi, mwombee mwenye nyumba, mshukuru na pia msalimie na mpe zawadi ya kijitabu chenye msukumo wa Sunnah, n.k. ikiwezekana.

## Sunnah na Adabu 15 kuhusu Majirani

**Misemo 7 ya Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم**

1. "Kwa fadhila ya Mwislamu mwema, Mwenyezi Mungu Mtukufu huondoa balaa katika nyumba 100 za jirani yake." Kisha yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasoma aya ifuatayo yenye baraka:

وَلَوْلَا دَفْعُ اللّٰهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ الْاَرْضُ

*'Na ikiwa Mwenyezi Mungu hatawaweka mbali watu wengine kwa wengine, basi ardhi itaharibika.'*

*[Kanz-ul-Iman (tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 2, Surah Al-Baqarah, aya ya 251)*

*(Majma' Al-Zawa`id, juzuu ya 8, uk. 299, Hadithi ya 13533)*

2. Mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, jirani bora ni yule anayemtakia mema jirani yake. *(Tirmizi, juzuu ya 3, uk. 379, Hadithi ya 1951)*

3. Yule ambaye jirani yake hajasalimika na uovu wake hataingia Peponi. *(Muslim, uk. 43, Hadithi ya 46)*

4. Anayekula akashiba, lakini jirani yake ana njaa si mwamini mkamilifu. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 3, uk. 225, Hadithi ya 3389)*

5. Mwenye kumsababishia uchungu jirani yake anani sababishia maumivu, na mwenye kuni sababishia maumivu huchukiza Mwenyezi Mungu Mtukufu. *(Attargheeb Wattarheeb, juzuu ya 3, uk. 241, Hadithi ya 13)*

6. Jibra'iyl (عَلَيْهِ السَّلَام) aliendelea kutilia mkazo (haki za) jirani kiasi kwamba nilifikiri angemfanya jirani kuwa mrithi. *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 104, Hadithi ya 6014)*

7. Mtu anayemwamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na Siku ya Qiyama ni lazima amtendee wema jirani yake. *(Muslim, uk. 44, Hadithi ya 48)*

8. Nyumba arobaini ni jirani. (Maraseel Abi Dawood uk. 16) Sayyiduna Imam Zuhri رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Ina maana ya nyumba 40 za kuelekea kila moja ya pande zote nne.' *( Maraseel Abi Dawood, uk. 16)* Imeelezwa katika 'Nuzha-tul-Qaari': "Kila mtu anaelewa 'nani ni jirani' kutoka kwa mazoea na mambo ya kawaida." *(Nuzha-tul-Qaari, juzuu ya 5, uk. 568)*

9. Sayyiduna Imamu Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Al-Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Hizi pia ni miongoni mwa haki za jirani kwamba unapaswa kumtolea salamu kwanza, usiwe na mazungumzo marefu naye na wala usiulize sana kuhusu hali yake. Ikiwa ni mgonjwa, unapaswa kuuliza afya yake; ikiwa ana shida, mfariji na umsaidie. Katika tukio la furaha, kumpongeza na kushiriki katika tukio la furaha. Aidha, msamehe makosa yake; usichunguze ndani ya nyumba yake kutoka kwa paa yako; usiipunguze njia iendayo nyumbani kwake; usijaribu kuona chochote anachopeleka nyumbani kwake; ficha makosa yake; na ikiwa amepata ajali au ana shida yoyote, msaidie mara moja; usighafilike na kulinda nyumba yake wakati hayupo nyumbani; usisikilize neno lolote

dhidi yake; weka macho yako chini mbele ya wanafamilia wake; sema kwa upole na watoto wake; na mpe muongozo juu ya mambo ya dini au ya kidunia ambayo yeye hana ujuzi nayo. *(Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 266,267, Muhtasari)*

10. **Kisa**: Mtu mmoja alimwambia Sayyiduna Abdullah Bin Mas'uud رَضِیَ اللهُ عَنْهُ, 'Jirani yangu ananiumiza, ananitukana na ananifanyia ukatili. Yeye رَضِیَ اللهُ عَنْهُ akajibu :', 'Ikiwa yeey amemuasi Mwenyezi Mungu kuhusu nyinyi, basi nyinyi mumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu yeye.'

*(Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 266,267, Muhtasari)*

11. **Kisa**: Mtu mcha Mungu alikuwa na idadi kubwa ya panya nyumbani kwake. Mtu fulani aliuliza hivi kwa unyenyekevu, 'Bwana! Ukifuga paka ni vizuri.' Akajibu yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَیْه, 'Nahofia kwamba panya, baada ya kusikia sauti ya paka, wanaweza kwenda nyumbani kwa jirani yangu. Kwa njia hii, nitakuwa ni mtu ambaye anapenda kwa ajili ya jirani yake kitu ambacho yeye hapendi kwa ajili yake mwenyewe.

*(Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 266,267, Muhtasari)*

12. Imepokewa kwamba akishika sehemu ya chini ya shati la jirani tajiri, jirani maskini atasema: "Ewe Mola wangu! Muulize kwa nini alininyima matendo yake mazuri na kwa nini alinifungia mlango wake." *(Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 266,267, Muhtasari)*

13. Mtu mmoja akasema kwa unyenyekevu, 'Ya Rasululallah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم! Inasemekana juu ya mwanamke fulani kwamba anaswali, anafunga na anafanya sadaka kwa wingi, lakini kuna jambo jengine ambalo ni kuwaudhi majirani zake kwa ulimi wake." Akajibu Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم' Yuko Motoni." Mtu huyo akasema kwa unyenyekevu, 'Ya Rasoolallah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم!

Inasemekana kuhusu mwanamke fulani kwamba yeye hufunga (nafl) chache, hutoa sadaka kidogo na huswali swala chache. Hutoa vipande vya jibini kama sadaka na wala hawaumizi jirani zake kwa ulimi wake.' Akajibu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, 'Yuko Peponi.' *(Musnad Ahmad Bin Hanbal, juzuu ya 3, uk. 441, Hadithi ya 9681)*

14. **Kauli ya Mustafa** صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Kuna aina tatu za majirani: Wengine wana haki tatu, wengine wana haki mbili na wengine wana haki moja. Jirani ambaye ni Muislamu na jamaa yako ana haki tatu - haki ya jirani, haki ya Uislamu na haki ya uhusiano; jirani Muislamu ana haki mbili - haki ya jirani na haki ya Uislamu; jirani kafiri ana haki moja tu - haki ya jirani. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 7, uk. 83, Hadithi ya 9560)*

15. **Kisa**: Wakati mmoja, jirani wa Kiyahudi wa Sayyiduna Ba-Yazeed Bistami رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alikwenda safarini. Mke wake na watoto walibaki nyumbani. Usiku, mtoto wa Myahudi angelia. Yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه aliuliza mara moja, 'Kwa nini mtoto analia?' Yule mwanamke wa Kiyahudi akajibu, 'Hakuna taa nyumbani kwetu na mtoto anaogopa giza.' Tangu siku hiyo, yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه akaanza kutuma taa iliyowashwa yenye mafuta mengi kila siku. Myahudi aliporudi, mke wake alimwambia kuhusu jambo hilo. Myahudi akasema, 'Kwa nini kuwe na giza (la ukafiri) ndani ya nyumba ambayo taa ya Ba-Yazid imeletwa!' Wote wakasilimu. *(Mirat, gombo la 6, uk. 573)*

## Sunnah na Adabu 13 za Kunywa Maji

### Maneno mawili yenye baraka ya Mustafa ﷺ

1. Usinywe [maji] kwa pumzi moja kama ngamia. Lakini badala yake, kunywa kwa pumzi mbili au tatu. Soma 'بِسْمِ الله' kabla ya

kukinywa na ukiisha soma اَلْحَمْدُ لِلّٰه. *(Sunan-ut-Tirmizi, juzuu ya 3, uk. 352, Hadees 1892)*

2. Rasuli Mtukufu صَلَّى اللّٰه عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amekataza kuvuta pumzi au kupuliza ndani ya chungu (cha maji). *(Sunan Abi Dawood, juzuu ya 3, uk. 474, Hadees 3728)* Akizungumzia juu ya Hadiyth zilizobarikiwa zilizotajwa hapo juu, mfasiri mashuhuri, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Kupumua ndani ya chombo ni kitendo kinachofanywa na mnyama, zaidi ya hapo, weka mdomo wako mbali na chombo (cha kula au kunywa) kwani pumzi wakati mwingine huwa na sumu (yaani, weka glasi mbali na mdomo wakati wa kuvuta pumzi). Usipulizie chai ya moto au maziwa ili kupoeza, lakini subiri kwa muda, ipoe kidogo, kisha unywe. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 6, uk. 77)* Hata hivyo, hakuna ubaya kupuliza maji baada ya kusoma Durood Shareef n.k., kwa nia ya kupata tiba.

3. Soma 'بِسْمِ الله' kabla ya kunywa maji.

4. Kunywa kwa mafundo madogo kwa kunyonya maji, mafundo makubwa husababisha ugonjwa wa ini.

5. Kunywa maji katika pumzi tatu.

6. Kunywa maji kwa kutumia mkono wa kulia na katika hali ya kukaa.

7. Kunywa maji yaliyobaki kwenye chungu baada ya Wudhu (udhu) ni tiba ya magonjwa 70, kwani yanafanana na maji ya Zamzam. Isipokuwa hivi viwili (yaani maji mabaki ya Wudhu na maji ya Zamzam), kunywa maji ya aina yoyote ukiwa umesimama ni Makruh. (Imetolewa kutoka: *(Fatawa Razawiyyah,*

*juz. 4, uk. 575; juzuu ya 21, uk. 669)* Kunywa maji mabaki ya Wudhu na maji ya Zamzam ukiwa umesimama na kuelekea Qiblah.

8. Hakikisha kuwa hakuna kitu chenye madhara n.k katika kinywaji (maji n.k.) kabla ya kukinywa. *(Ithaf-us-Sadah juzuu ya 5, uk. 594)*

9. Baada ya kunywa maji, sema اَلْحَمْدُ لِلّٰه.

10. Hujjat-ul-Islam Sayyiduna Imaam Muhammad Bin Muhammad Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Soma 'بِسْمِ الله' kabla ya kuanza kunywa maji. (mwisho wa pumzi ya kwanza, 'اَلْحَمْدُ لِلّٰه' baada ya pumzi ya pili na usome 'اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ' na baada ya pumzi ya tatu usome 'اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ' *(Ihya-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 8)* Hiyo ni amali njema lakini si la lazima kwani isipofanywa hivyo hakuna ubaya wowote. Ikiwa mtu atasema 'بِسْمِ الله' kabla na 'اَلْحَمْدُ لِلّٰه' baada yake, Sunnah itatekelezwa.'

11. Mabaki ya maji safi iliyonywewa na Mwislamu kwenye glasi yasitupwe bila ya dharura, wakati yanaweza kutumika.

12. Imepokewa 'سُؤْرُ الْمُؤْمِنِ شِفَاءٌ' yaani mabaki ya Muislamu yana tiba. *(Al-Fatawa Al-Faqihi-tul-Kubra li Ibn Hajar Al-Haytami, juzuu ya 4, uk. 117)*

13. Baada ya muda wa kunywa maji , ukiangalia glasi tupu, utaona matone machache ya maji yaliyokusanywa chini ya glasi, kunywa hayo pia.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na

## Adabu 32 za Kula Chakula

1. Chakula hakipaswi kuliwa kwa sababu ya kuwa ni kitamu pekee, bali weka nia wakati wa kula: Ninakula chakula kwa ajili ya kupata nguvu ili kumwabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

2. Chakula kinapaswa kuliwa kidogo kuliko hamu ya mtu. Ikiwa mtu akila chakula kwa kushiba, ni mubah yaani hatapata thawabu wala kuwa mwenye dhambi, kwa sababu inaweza pia kuwa na lengo sahihi kama mtu anaweza kuwa na nguvu zaidi. Kula zaidi ya hamu ya mtu ni haramu. Kula kupita kiasi kunamaanisha kula sana hivi kwamba kuna dhana kubwa kwamba unaweza kuwa na ugonjwa wa tumbo, kama vile kuhara, na kujisikia vibaya. *(Durr-e-Mukhtar, juz. 9, uk. 560)* Vile vile, ikiwa mtu mwenye afya njema atatumia chakula hicho kwa kiasi ambacho kwambakuna dhana kubwa kwamba anaweza kupata ugonjwa, ni dhambi. Vivyo hivyo, ikiwa mgonjwa akila chakula ambacho ni haramu kwake na kuna dhana kali kwamba chakula hicho kinazidisha ugonjwa wake, na hii inathibitishwa na uzoefu, kwa mfano, ni dhambi.

3. Kula chini ya hamu ya kula ni mkusanyiko wa faida nyingi, kwa sababu karibu asilimia 80 ya magonjwa hutokea tunapokula hadi kushiba. Kwa hivyo, ikiwa bado tuna hamu ya kula kidogo, tunapaswa kuacha kula.

4. Mistari imeandikwa kwenye mikeka mingi ya kulia (kwa mfano, beti au jina la kampuni yoyote, n.k.). Mikeka kama hiyo ya kulia haipaswi kutumiwa na wala milo haipaswi kutolewa juu yao. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 420)*

5. Kuosha mikono hadi vifundoni kabla na baada ya kula chakula ni Sunnah. *(‘Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 337)*

6. Mtume kipenzi صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: “Kutia udhu (yaani kuosha mikono miwili mpaka vifundoni) kabla na baada ya kula [chakula] kunaongeza riziki na humfukuza Shetani.” *(Musnad Al-Firdaus, juzuu ya 2, uk. 333, Hadithi ya 3501)*

7. Vua viatu vyako wakati wa kula chakula kwani kitapumzisha miguu yako. Mtume kipenzi صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: “Unapoanza kula chakula, vua viatu vyako, kwa sababu huleta faraja (yaani kupumzika) kwenye miguu yako. *(Mu’jam Awsat, juzuu ya 2, uk. 256, Hadithi ya 3202)*

8. Wakati wa kula, weka mguu wa kushoto chini na kuweka goti la kulia likiwa juu; au weka magoti yote mawili juu na ukae kwenye matako *(Murakhkhas az Bahar-e-Shari’at, juz. 3, uk. 378)* au ukae kwa hatua zote mbili. *(Ihya-ul-‘Uloom, juzuu ya 2, uk. 5)*

9. Iwe ni kaka wa Kiislamu au dada wa Kiislamu, wanapokaa kwa ajili ya kula, lazima wachukue sitara ya ziada kwa kutumia shela au sehemu ya chini ya kanzu yao.

10. Usiweke mchuzi au kikombe cha mchuzi kwenye chapati. *(Rad-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 562)*

11. Kula chakula ukiwa kichwa wazi (bila kofia) ni kinyume na heshima na kunapunguza riziki.

12. Ni makruh kula chakula kwa kushika tegemeo la sakafu kwa kuweka mkono wa kushoto juu yake. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 3, uk. 377)*

13. Ni jambo la busara kula chakula kwenye vyungu vya udongo. Malaika wanakuja kuona nyumba ya mtu anayetengeneza

vyungu vya udongo nyumbani kwake. *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 566)*

14. Ikiwa kuna mchuzi wa mboga kwenye mkeka wa kulia, malaika hushuka. *(Ihya-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 22)*

15. Soma dua ifuatayo kabla ya kula. Ikiwa chakula au kinywaji kitatiwa hata sumu, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ hakitakudhuru.

'بِسْمِ اللهِ الَّذِیْ لَایَضُرُّمَعَ اسْمِهٖ شَیْءٌ فِی الْاَرْضِ، وَلَافِی السَّمَآءِ، یَاحَیُّ یَا قَیُّوْمُ-'

*(Tirmizi, juzuu ya 5,uk. 250, Hadithi ya 3399 | Ibn-e-Majah, juz. 4, uk. 284, Hadithi ya 3829)*

Tafsiri: Jina la Mwenyezi Mungu kwa kuanzia, Ambaye kwa baraka ya jina Lake hakuna kitakacho weza kusababisha madhara kutoka katika ardhi au mbinguni; Ewe Ambaye yu hai kwa ridhaa Yake mwenyewe na Mhifadhi wa (wote) wengine. *(Al-Firdaus, juzuu ya 1, uk. 282, Hadithi ya 1106)*

16. Ukisahau kusoma 'بِسْمِ الله' mwanzoni, soma 'بِسْمِ اللهِ اَوَّلَهٗ وَاٰخِرَهٗ' katikati ya kula chakula. Tafsiri: 'Jina la Mwenyezi Mungu la kuanzia na kumalizia nalo.

17. Kula chumvi kabla na baada ya kula kwani ni Sunnah na inatibu maradhi 70. *(Rad-ul-Muhtar, juz. 9, uk. 562)* A'la Hazrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amekichukulia chakula chenye chumvi kuwa chumvi. *(Hayat-e-A'la Hadrat, juzuu ya 1, uk. 107)*

18. Kula kwa mkono wako wa kulia. Kula, kunywa, kuchukua na kutoa kwa mkono wa kushoto ni njia za Shetani. Ndugu wengi wa Kiislamu hula tonge kwa mkono wao wa kulia, lakini wanapoweka mkono wao wa kushoto chini ya midomo yao, baadhi ya makombo huanguka juu yake na kisha huviweka mdomoni kwa mkono wao wa kushoto. Vile vile, wao hutumia

mkono wao wa kushoto kuokota na kula makombo yaliyoanguka kwenye mkeka wa kulia chakula. Wachukue makombo kutoka kwa mkono wao wa kushoto hadi mkono wao wa kulia na kisha waweke kinywani mwao.

19. Kuchukua chapati kwa mkono wa kushoto na kuvunja kwa mkono wa kulia kwa ajili ya kufanya tonge huondoa kiburi. *(Fatawa Razawiyyah, juz. 21, uk. 669)* Unapokula peke yako, pata mazoea ya kuvunja chapati au mkate, n.k. katikati ya sahani au chombo cha mchuzi. Kwa njia hii, makombo ya chapati au mbegu za sesame kutoka kwa mkate zitaanguka kwenye sahani. Vinginevyo, vinaweza kuanguka kwenye mkeka wa kulia na huenda yatupwe.

20. Kula kwa vidole vitatu (yaani kwa kidole cha kati, cha mbele na kidole gumba) kwani mtindo huu ni Sunna ya manabii waliobarikiwa. Ikiwa nafaka za mchele ni tofauti na haiwezekani kufanya kipande kwa vidole vitatu, unaweza kula kwa vidole vinne au tano.

21. Chukua vipande vidogo na usitoe sauti ya kutafuna. Kwa tahadhari hii, tafuna kiasi kwamba chakula kinywani mwako kinakuwa nyembamba. Kwa njia hii, mate ya kusaga chakula pia yatachanganywa nayo vizuri. Ukimeza chakula bila kukitafuna vizuri, tumbo lako litakuwa na matatizo ya kumeng'enya na hivyo unaweza kukabiliwa na magonjwa ya aina nyingi. Kwa hivyo, usitumie utumbo ambapo meno hutumiwa.

22. Soma 'يَاوَاجِدُ' baada ya kila tonge au tonge ya pili. Hii Hutengeneza nuru kwenye tumbo na magonjwa huondoka.

23. Baada ya kula, kwanza lamba kidole cha kati kiwe safi, kisha kidole cha shahada na kisha kidole gumba mara tatu. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akilamba vidole vyake vilivyobarikiwa mara tatu baada ya kula. *(Al-Shamaail Al-Muhammadiyyah Tirmizi, uk. 96, Hadithi ya 133)*

    Ikiwa athari ya chakula bado itabaki pale kwenye vidole hata baada ya kulamba mara tatu, rambaza [vidole vyako] zaidi mara nyingi inavyohitajika hadi athari ya chakula isibaki hapo tena.

24. Lamba chombo kiwe safi pia. Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa: 'Kwa mtu ambaye amelamba chombo kikiwa kisafi baada ya kula, sahani hiyo huomba na kusema: "Mwenyezi Mungu Mtukufu akuepushe na moto wa Jahannam kama ulivyo niokoa mimi kutoka kwa Shetani." *(Jam'-ul-Jawami', juzuu ya 1, uk. 347, Hadithi ya 2558)* Kwa mujibu wa riwaya nyingine: "Chombo kinamuombea msamaha mtu huyo. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 4, uk. 14, Hadithi ya 3271)*

25. Sayyiduna Imamu Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: "Mwenye kulamba bakuli (au sahani) safi (baada ya kula) na akanywa maji ya kusuuza atapata ujira wa kumwacha huru mtumwa mmoja. Kuokota na kula makombo yaliyodondoshwa ni mahari ya Hurul aini." *(Ihya'-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 8)*

26. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: "Mwenye kuokota na kula vipande vilivyoanguka vya chakula anaishi maisha ya mafanikio, na watoto wake watakaa salama na shida na matatizo. *(Ihya'-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 8)*

27. Baada ya kula, safisha meno yako.

28. Baada ya kula, soma dua ifuatayo pamoja na swala iliyobarikiwa kabla na baada yake: ‘اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِىْ اَطْعَمَنَا وَسَقَانَا، وَجَعَلَنَا مُسْلِمِيْنَ’ Tafsiri: ‘Shukrani kwa Mwenyezi Mungu Aliyetulisha na Aliyetunywesha na Akatujalia tuwe waisilamu.’

29. Iwapo kuna mtu amekupa chakula, soma dua hii pia: ‘ اَللّٰهُمَّ اَطْعِمْ مَنْ اَطْعَمَنِىْ، وَاسْقِ مَنْ سَقَانِىْ’ Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Mlishe aliyenilisha na mnyweshe aliyeninywesha. *(Al-Hasn Al-Haseen, uk. 71)*

30. Soma ‘Surah Al-Ikhlaas’ na ‘Surah Al-Quraysh’ baada ya kula chakula. *(Ihya-ul-‘Uloom, juzuu ya 2, uk. 4-8)*

31. Baada ya kula, osha mikono yako kwa njia inayofaa na sabuni na uifute.

32. Sayyiduna Imamu Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: Udhu (kuosha mikono miwili hadi kwenye vifundo vya mikono) baada ya kula humkinga mtu na maradhi ya akili. *(Ihya-ul-‘Uloom, juzuu ya 2, uk. 4-8)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب    صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 30 za Ukarimu

**Misemo minane ya Mustafa** صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

1. Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na Siku ya Kiyama amheshimu mgeni. *(Bukhari, juz. 4, uk. 105, Hadith 6018)* Kuhusu Hadithi hii yenye baraka, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, “Heshima ya mgeni ni kukutana naye kwa tabasamu kwa namna ifaayo, amtengenezee chakula na huduma nyinginezo, amhudumie mwenyewe kadri awezavyo.” *(Mirat , gombo la 6, uk. 52)*

2. Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na Siku ya Kiyama asimpe uchungu mgeni. *(Ikram-ul-dayf, uk. 25, Hadithi ya 13)*

3. 'Mgeni anapomjia mtu huleta riziki yake pamoja naye, na anapotoka huwa ni sababu ya kusamehewa dhambi za mwenyeji. *(Kanz-ul-'Ummal, juzuu ya 9, uk. 107, Hadithi ya 25831)*

4. Mwenye kuswali, kutoa zaka, kuhiji, kufunga Ramadhani na kumpa ukarimu mgeni wake ataingia Peponi. *(Mu'jam-ul-Kabeer, juzuu ya 12, uk. 106, Hadithi ya 12692)*

5. Mtu asiyeonyesha ukarimu (licha ya kuwa na pesa za kutosha) hana wema. *(Musnad Ahmad Bin Hanbal, juzuu ya 6, uk. 142, Hadithi ya 17424)*

6. Sio busara kwa mtu kumfanya mgeni wake afanye kazi. *(Al-Jami'-ul-Sagheer, uk. 288, Hadithi ya 4686)*

7. Sunnah ni kwamba mtu amwone mgeni wake mlangoni. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 4, uk. 52, Hadithi ya 3358)*

8. Katika nyumba ambamo chakula huliwa, wema na baraka huja haraka kuliko kufikiwa kwa kisu kwenye nundu ya ngamia. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 4, uk. 51, Hadithi ya 3357)*

   Ufafanuzi wa Hadiyth: yaani baraka hubakia katika nyumba ambayo wageni, mahujaji na watembeleaji wanakula chakula. Vinginevyo, washiriki wa kila familia hula nyumbani kwao. Nundu ya ngamia haina mfupa, bali mafuta tu; kwa hiyo, kisu huikata haraka sana na kufikia chini yake. Ulinganisho, kwa hivyo, umefanywa nayo, yaani, wema na baraka hufikia haraka sana kwenye nyumba kama hiyo. *(Mirat, gombo la 6, uk. 67)*

9. Sayyiduna Bibi Khadijah رَضِیَ اللہُ عَنۡہَا amesema: "Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم huwapa jamaa zake utendeaji bora, huwapa ukarimu

wanaosafiri,na kwa ajili ya ukweli na uadilifu husaidia wote kwenye shida na matatizo zao. *(Seerat-e-Mustafa, uk. 109, Mukhtasran)*

10. Mtu mmoja akasema kwa unyenyekevu, ‘Ya Rasuolallah صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم! Nilimtembelea mtu. Hakunionyesha ukarimu. Sasa akinijia nimlipize kisasi?’ Akajibu Yeye صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, ‘Hapana, bali mfanyie ukarimu. *(Tirmizi, juzuu ya 3, uk. 405, Hadithi ya 2013)*

11. Sayyiduna Ata' رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alisema: "Wakati wa kula chakula, wakati hakukuwa na mtu wa kula naye, Sayyiduna Ibrahim عَلَيْهِ السَّلَام. Alikuwa akitoka nje na kuenda kwa msafara wa maili moja au mbili kumtafuta mtu ili apate mtu ambaye angeweza kula naye.” *(Tanbih-ul-Ghafileen, uk. 249)*

12. Sayyiduna Ikramah رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: “Sayyiduna Ibrahim Khalilullah عَلَيْهِ السَّلَام jina la ‘Abu Dhaifan’ (yaani mtu mkarimu sana) ilikuwa maarufu. Nyumba yake ilikuwa na milango minne; angeendelea kutazama milangoni akitarajia mgeni kutoka kwa yoyote kati yao.” *(Tanbih-ul-Ghafileen, uk. 249)*

13. Sayyiduna Anas Bin Malik رَضِیَ اللهُ عَنْهُ amesema: “Malaika wa rehema hawaji kwenye nyumba ambayo wageni hawaingii humo.’ *(Ihya`-ul-‘Uloom, (Urdu), juzuu ya 2, uk. 43 | Ihya`-ul-‘Uloom, juzuu ya 2, uk. 16)*

14. Mufti Ahmed Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Mgeni wetu ni yule anayekuja kukutana nasi kutoka nje (yaani kutoka mji au nchi nyingine) tukiwa tayari tunamjua au hatumjui. Mtu anayekuja kukutana nasi kutoka eneo letu au jiji letu kwa dakika mbili au nne ni mtembeleaji, sio mgeni. Akutanishwe ipasavyo na apewe chakula chepesi, lakini asipewe karamu. Mtu ambaye si mmoja wa marafiki zetu na ambaye anakuja

kwetu kwa ajili ya kazi yake si mgeni. Yeye ni sawa na mtu anayekwenda kwa mtawala au mufti na kesi yake au kwa ajili ya kupata fatwa. Yeye si mgeni wa mtawala (au mufti). *(Mirat, gombo la 6, uk. 54)*

15. Mgeni anapaswa kutunza ratiba na jedwali la majukumu ya mwenyeji wake.

16. Hadithi iliyobarikiwa # 14 katika ukurasa wa 391 wa Bahar-e-Shari'at juzuu ya 3: Mtu anayemwamini Mwenyezi Mungu (Mtukufu) na Siku ya Kiyama anapaswa kumheshimu mgeni wake, ampe ukarimu kamili na apate milo ya siku iliyoandaliwa kwa ajili yake. Na amchunge kadiri inavyowezekana na kisha amkaribishe (yaani asiwe rasmi naye baada ya siku moja, bali atoe chochote alicho nacho) kwa muda wa siku tatu, na baada ya siku tatu ni sadaqah. Sio halali kwa mgeni kuendelea kukaa kwa mwenyeji wake ambapo kukaa kwake kutasababisha yeye (mwenyeji) kupata matatizo. *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 136, Hadithi ya 6135)*

17. Unapomwendea mtu kama mgeni, ni bora kuchukua zawadi kwa mwenyeji au watoto wake kwa nia njema kulingana na uwezo wako.

18. Allamah Maulana Mufti Muhammad Amjad Ali A'zami رحمۃ اللہ علیہ amesema: Mambo manne ni ya lazima kwa mgeni.

    i. Anapaswa kuketi popote anapopewa kiti.

    ii. Chochote anacholetewa, awe na furaha nacho; asiseme: 'Nakula bora kuliko hii nyumbani kwangu,' au maneno mengine kama haya.

    iii. Hapaswi kuondoka mahali hapo bila idhini ya mwenyeji.

iv. Anapoondoka mahali hapo, anapaswa kumwombea mwenyeji.

*(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 394 | 'Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 344)*

19. Kuhusu nyumba au chakula, n.k mgeni hatakiwi kutoa ukosoaji wa aina yoyote, na wala asitoe sifa za uwongo.

20. Mwenyeji hapaswi kumuuliza mgeni maswali yoyote ambayo yatasababisha mgeni kuhitaji kudanganya, kama vile kusema yafuatayo: Nyumba yetu ikoje? Ulipenda chakula chetu au hukupenda? Katika pindi kama hiyo, licha ya kutopenda nyumba au chakula, mgeni akisifu kwa uwongo nyumba au chakula kwa heshima, atakuwa mtenda dhambi.

21. Mwenyeji hapaswi kumuuliza mgeni wake swali kama hilo: Je, ulikula na kushiba au la? Kwani hapa, kuna hatari pia ya kusema uwongo katika jibu. Mgeni anaweza kusema uwongo kwa mwenyeji kwa kusema, 'Nimekula nikashiba.' Hii ni licha ya mgeni huyo kula kidogo kutokana na mazoea ya kufanya hivyo, mlo uliowekwa au sababu nyinginezo, na bado alisema hivyo laiti mwenyeji angesisitiza kwamba mgeni ale zaidi.

22. Wakati mwingine, wakati wa kula chakula, mtu hupewa jukumu la kuweka mchuzi, vipande vya nyama, n.k. kwenye sahani ya mgeni kwa mkono wake mwenyewe. Inaweza kusababisha shida kwa mgeni. Kwa mfano, mgeni anataka kuepuka kula nyama, lakini mtu huyo anaendelea kuweka vipande vya nyama kwenye sahani yake.

23. Mwenyeji anapaswa kumwambia mgeni mara kwa mara, 'chukua zaidi', lakini hapaswi kusisitiza juu yake kwani mgeni anaweza kula kupita kiasi kutokana na msisitizo unaoweza kumdhuru. *('Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 344)*

24. Sayyiduna Imamu Abu Hamid Muhammad bin Muhammad bin Muhammad Ghazali رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه amesema: 'Ikiwa mwenzako anakula kidogo kwa ajili ya kumshawishi, sema: 'Tafadhali kula!' Lakini usiseme hivi zaidi ya mara tatu kana kama ni kusisitiza. na ni nje ya mipaka. *(Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 2, uk. 9)*

25. Mwenyeji hapaswi kuwa mtulivu kabisa, na wala hapaswi kutoweka baada ya kuweka chakula, bali anapaswa kuwepo hapo. *('Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 345)*

26. Usimkasirikie mtumishi wako mbele ya wageni wako. *('Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 345)*

27. Mwenyeji anapaswa kujishughulisha katika kumhudumia mgeni wake. Asiwagawie waja wake jukumu hili kama ni Sunna ya Sayyiduna Ibrahim Khalilullah عَلَيۡهِ السَّلَام (kumkaribisha mgeni wake) *('Aalamgeeri, juz. 5, uk.345 | Bahar-e-Shari'at, juz. 3, uk. 394)* Hakutakuwa na hesabu [Siku ya Hukumu kwa chakula] kwa ajili ya mtu anayekula na ndugu zake [Waislamu]. *(Qoot-ul-Quloob, juzuu ya 2, uk. 306)*

28. Sayyiduna Imamu Abu Hamid Muhammad bin Muhammad bin Muhammad Ghazali رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه amesema: Mtu mwenye kula kidogo anapokula na wengine, aanze kula baada ya muda kidogo, achukue vipande vidogo na ale polepole ili ale na watu wengine mpaka mwisho. *(Mirqat-ul-Mafatih, juzuu ya 8, uk. 84, chini ya Hadithi ya 4254)*

29. Iwapo mtu ataacha kula ili watu wengine wavutiwe naye na kumchukulia kuwa yeye ndiye anayekula kidogo kuliko hamu yake ya kula, atakuwa ni mnafiki na atastahiki adhabu ya Jahannam.

30. Iwapo mtu anakula zaidi ya hamu yake kwa sababu anakula na mgeni na anajua kama ataacha kula, mgeni wake ataona haya na hatakula kwa kushiba, katika kesi hii, anaruhusiwa kula zaidi. lakini isiwe kwa kiwango ambacho kutokana nayo anaishia kudhuru tumbo lake. *(Mukhlis AZ Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 6, uk. 561)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب        صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunnah na Adabu 13 za Kutendea

# Jamaa kwa Wema

1. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu, ‘وَاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِیْ تَسَآءَلُوْنَ بِهٖ وَالْاَرْحَامَ’ *(Sehemu ya 4, Surah Al-Nisa, aya ya 1)* Kuhusu aya hii iliyobarikiwa, imeandikwa katika ‘tafseer e Mazharii’ yaani ‘epuka kukata uhusiano na jamaa.’ *(Tafseer-e-Mazhari, juzuu ya 2, uk. 212)*

2. Misemo / Kauli saba za Mustafa صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: “Mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu na Siku ya Kiyama anatakiwa kuwatendea wema jamaa. *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 136, Hadithi ya 6138)*

3. Siku ya Hukumu, aina tatu za watu watakuwa chini ya kivuli cha ‘Arsh ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mwenye kuwatendea wema jamaa (atakuwa miongoni mwao). *(Al-Firdaus, juzuu ya 2, uk. 99, Hadithi ya 2526)*

4. Mwenye kuvunja mahusiano hataingia Peponi. *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 97, Hadithi ya 5984)*

5. Mbora miongoni mwa watu ni yule anayesoma Qur'ani Tukufu kwa wingi, ni mchamungu zaidi, anaamrisha [watu] kutenda mema na anawakataza kufanya maovu zaidi na mwenye

kuwatendea wema jamaa zake zaidi. *(Musnad Imam Ahmad, juzuu ya 10, uk. 402, Hadithi ya 27504)*

6. Bila shaka, sadaqah iliyo bora zaidi ni ile inayotolewa kwa jamaa ambaye ana uadui.

*(Musnad Imam Ahmad, juzuu ya 9, uk. 138, Hadithi ya 23589)*

7. Rehema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu haishuki kwa umma ambao una watu wanaokata uhusiano na jamaa zao. *(Zwajir, juzuu ya 2, uk. 153)*

8. Mwenye kutaka kujengewa kasri (peponi) na cheo chake kinyanyuliwe amsamehe anayemdhulumu, amjaalie anayemnyima na adumishe uhusiano na mwenye kuvunja uhusiano naye. *(Al-Mustadrak, juzuu ya 3, uk. 12, Hadithi ya 3215)*

9. Sayyiduna Faqihi Abu Al-lays Samarqandi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Kuna faida kumi za kuwatendea wema jamaa.

   i. Inampendeza Mwenyezi Mungu Mtukufu. ii. Huwafurahisha watu. iii. Inaleta furaha kwa malaika. iv. Waislamu wanamsifu mtu huyo. v. Inampa uchungu Shetani. vi. Inaongeza maisha. vii. Huleta baraka katika riziki. viii. Mababu waliokufa (yaani baba wa Kiislamu, babu) wanahisi furaha. ix. Inaongeza upendo wa pande zote. x. Kutokana na hilo, malipo ya mtu huongezeka baada ya kifo chake kwa sababu watu wanamuombea dua. *(Tanbih-ul-Ghafileen, uk. 73)*

10. Kurasa kutoka 558 hadi 560 za 'Bahar-e-Shari'at' juz. 3, zinasema: Kuwatendea jamaa kwa wema kunamaanisha kuanzisha uhusiano, yaani kuwatendea wema jamaa. Ummah mzima umeunda maafikiano juu yake kwamba kuwatendea wema jamaa ni wajibu na kuvunja uhusiano na jamaa ni

haramu. Ni akina nani jamaa ambao uhusiano mzuri na wao ni wajib? Baadhi ya wanazuoni wa Kiislamu waliobarikiwa wamesema wao ni zu-raham mahram, na wengine wakasema inamaanisha zu-raham, wawe mahram au la. Na msemo huu wa pili ni sahihi zaidi. Katika Ahadith zilizobarikiwa, tumeamrishwa kuwatendea wema jamaa zetu bila sharti lolote. Katika Quran Tukufu, (jamaa) wametajwa bila ya sharti lolote, lakini kuna jambo moja: kwa vile kuna viwango tofauti vya jamaa, (kwa njia sawa) kuna viwango tofauti vya ukarimu kwa jamaa. Daraja ya wazazi ni ya juu zaidi, baada yao daraja ya zu-raham mahram (yaani jamaa ambao nikah yako ni haramu milele kutokana na kuwa na uhusiano wa damu nao), baada ya hapo jamaa waliobakia kwa kufuatana na ukaribu wa uhusiano. *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 678)*

11. Kuna aina mbalimbali za kutendea wema kwa jamaa: kuwapa zawadi na kuwasaidia katika kazi yoyote ambayo wanahitaji msaada wako, kuwasalimia, kwenda kukutana nao, kukaa nao, kuzungumza nao na kuwatendea kwa ukarimu. *(Durar, gombo la 1, uk. 323)*

12. Ikiwa mtu yuko katika nchi ya kigeni, anafaa kutuma barua kwa jamaa zake na kuendelea kuwasiliana nao kwa njia ya barua ili kusiwe na kikosi kati yake na jamaa zake. Na ikiwezekana, arudi katika nchi yake na kuburudisha uhusiano wake na jamaa zake. Kwa njia hii, mapenzi yataongezeka *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 678)* (Kuwasiliana kwa simu au mtandao pia ni muhimu.)

13. Kutendea vizuri kwa jamaa haimaanishi kwamba ikiwa wanakutendea vizuri, unapaswa pia kuwatendea vizuri. Kwani kwa kweli uhusiano huu, unaitwa kubadilishana, ambayo ina

maana kama ikiwa wamekutuma kitu, wewe pia unawatuma kitu; wakikujia wewe nawe unaenda kwao.Kutendea wema jamaa kwa ubora zaidi ni kuwa wakikata (uhusiano na wewe), basi wewe uuimarishe; ikiwa wanataka kuondoka kwako, wakawa wazembe kuelekea kwako, wewe tunza haki za uhusiano ulio nazo kwa wao. *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 678)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 11 za

# salamu

1. Ni Sunnah kumsalimia Muislamu wakati wa kukutana naye. (Madada wa Kiislamu wanapaswa kuwasalimia akina dada wa Kiislamu na maharimu zao.)

2. Wakati wa kusalimia, nia hii iwe moyoni kwamba mali na heshima ya mtu ambaye ninakaribia kumsalimia iko chini ya ulinzi wangu, na najua ni haramu kuingilia yoyote kati yao. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 459, imerekebishwa)*

3. Haijalishi ni mara ngapi unakutana na Waislamu, ukiingia na ukitoka kwenye chumba chochote, nk kwa siku, ni kitendo cha malipo kutoa salaam kwa Waislamu waliopo hapo.

4. Ni Sunnah kutoa salaam kwanza.

5. Mwenye kutoa Salamu mwanzo ni mtu ambaye anapata ukaribu na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

6. Mwenye kutoa Salamu mwanzo huepuka na kiburi. Mtume mpendwa صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenye kutoa Salamu

mwanzo huepuka na kiburi.’ *(Shu’ab-ul-Iman, juz. 6, uk. 433, Hadithi ya 8766)*

7. Rehema 90 huteremka kwa mwenye kutoa salamu kwanza, na rehema 10 humshukia mwenye kuitikia salamu. *(Kimiya-e-Sa’adat, juzuu ya 1, uk. 394)*

8. Mtu hupata fadhila (mema) 10 kwa kusema ‘اَلسَّلَامُ عَلَيْكُم’ (yaani amani iwe juu yenu). Akiongeza ‘وَرَحْمَةُ الله’ (na rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu [iwe juu yenu]), atapata fadhila (mema) 20. Akiongeza ‘وَبَرَكَاتُهٗ’ (na baraka [ziwe juu yenu]), atapata fadhila (mema) 30. Baadhi ya watu huongeza maneno ‘جَنَّتُ الْمقامِ و دوزخُ الْحرام’ kwa salaam,hii ni njia isiyo sahihi, na sentensi hii pia si sahihi kwa mtazamo wa kilugha. Baadhi ya watu wajasiri hata مَعَاذَالـلّٰه hutamka kwa mzaha kiasi cha kusema, ‘Watoto wako ni watumwa wetu’. Katika ukurasa wa 409 wa Fatawa-e-Razawiyyah, juz. 22, Imaam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Angalau semeni ‘اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ’, na bora kuliko hili ni kuongeza ‘وَرَحْمَةُالله’, na lililo bora zaidi ni kuongeza ‘وَبَرَكَاتُهٗ’, na hakuna haja ya kuzidisha hapo. Na ikiwa mtu amekuambia ‘اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ’ mwambie ‘وَعَلَيْكُمُ السَّلَامُ وَرَحْمَةُ الله’, na akisema ‘اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ الله’, Unapaswa kusema ‘وَعَلَيْكُمُ السَّلَامُ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهٗ’ [kwa kujibu]. na iwapo atasema hadi ‘وَبَرَكَاتُهٗ’, unapaswa pia kusema hivyo kwa sababu hakuna cha kuongeza zaidi. ‘وَاللهُ تَعَالٰى اَعلم’

9. Vivyo hivyo, kwa kusema ‘وَعَلَيْكُمُ السَّلَامُ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهٗ’ katika kujibu, mtu anaweza kupata fadhila (mema) 30.

10. Ni wajibu kujibu salamu kwa mara moja na kwa sauti ya kutosha ili aliyetoa salaamu aweze kuisikia.

11. Jifunze matamshi sahihi ya salaamu na matamshi ya jibu la salaam. Kwanza,mimi nasema, wewe unarudia baada ya kuisikiliza: 'اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ' Sasa kwanza nawaambia jibu, kisha mnarudia: 'وَعَلَيْكُمُ السَّلَامُ')

*Raza'ay Haq kay li'ay tum salam 'aam karo*

*Salamti kay talab gaar ho salam karo*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 14 za kupeana mkono

1. Waislamu wawili wanapokutana, ni Sunnah kutumia mikono miwili kwa ajili ya kupeana mkono.

2. Sema salaam kabla ya kupeana mikono.

3. Sema salaam unapoondoka; unaweza pia kupeana mikono.

4. Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Waislamu wawili wanapopeana mikono wakati wa kukutana na kuulizana hali yao, wao kwa wao, Mwenyezi Mungu Mtukufu hutuma baina yao rehema mia moja, kati ya hizo rehema 99 ni kwa ajili ya mwenye kukutana na ukarimu zaidi na kumuuliza hali ya ndugu yake kwa njia bora zaidi. *(Mu'jam-e-Awsat, juzuu ya 5, uk. 380, Hadithi ya 7672)*

5. Mswalie Mtume huku mkipeana mikono. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Dhambi zenu zilizopita na zijazo zitasamehewa kabla ya kutenganisha mikono.

6. Wakati wa kupeana mikono, ikiwezekana, soma dua ifuatayo baada ya kusoma salat-'alan-Nabiy:

يَغْفِرُ اللهُ لَنَا وَلَكُمْ

*yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu atusamehe sisi na wewe!*

7. Dua wanayoomba Waislamu wawili wakati wa kupeana mikono itaitikiwa إِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ, na wote wawili watasamehewa kabla ya kutenganisha mikono yao.

8. Kupeana mikono huondoa uadui.

9. Mtu anaweza kupata thawabu ikiwa atamsalimia Muislamu, kupeana naye mkono au tuseme akimtazama kwa mapenzi. Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa: "Mwenye kumuangalia ndugu yake Mwislamu kwa mapenzi na hana chuki naye moyoni mwake, atasamehewa madhambi yaliyotangulia kabla ya macho yake kurejea kwake. *(Mu'jam-e-Awsat, juzuu ya 6, uk. 131, Hadithi ya 8251)*

10. Unaweza kupeana mikono kila mara mnapokutana.

11. Siku hizi, baadhi ya watu hupeana mikono kwa mkono mmoja au tuseme wanagusa vidole vyao kwa vidole tu. Yote haya ni kinyume na Sunnah.

12. Ni makruh kubusu mkono wako mwenyewe baada ya kupeana mikono. *(Bahar-e-Shari'at, juz. 3, uk. 472)* Hata hivyo, mtu akibusu mkono wake mwenyewe kwa ajili ya kupata baraka baada ya kupeana mikono na mtu mcha Mungu, haichukiwi. A'la Hadrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Mtu akipeana mkono na mtu, na akabusu mikono yake mwenyewe kwa ajili ya kupata baraka, haikatazwi, maadamu anayepeana naye mikono ni miongoni mwa shakhsia ambao watu hupata baraka kutoka kwao. *(Jadd-ul-Mumtar, juzuu ya 7, uk. 65)*

13. Iwapo kupeana mikono na mvulana mrembo [au mwanamume] kunapelekea kwenye matamanio, haijuzu kupeana naye mikono, bali ikiwa kumtazama kunasababisha matamanio, sasa hata kumwangalia pia ni dhambi. *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 2, uk. 98)*

14. Wakati wa kupeana mikono, Sunnah ni kwamba viganja vyote viwili viwe tupu, visiwe na leso, n.k. mkononi, na kiganja kiguse kiganja. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 471)*

## Sunna na Adabu 12 za Mazungumzo

1. Zungumza kwa tabasamu na kwa furaha.

2. Kwa nia ya kuwaridhisha Waislamu, zungumza na wazee kwa heshima na zungumza na vijana kwa ukarimu. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ utapata ujira, na utaheshimika kwa wote wawili.

3. Kuzungumza kwa sauti kubwa kana kwamba unapiga kelele sio Sunnah.

4. Ukiwa na nia njema, uwe na mazoea ya kuzungumza na hata watoto wadogo kwa tabia njema. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Adabu zako zitaboreka na watoto pia watajifunza adabu.

5. Wakati wa mazungumzo, kugusa sehemu za siri, kuondoa uchafu kutoka kwa mwili kwa vidole, kugusa mara kwa mara pua mbele ya wengine, kuingiza kidole kwenye pua au sikio na kutema mate mara kwa mara sio vitendo vyema; wengine wanachukia jambo hilo.

6. Endelea kumsikiliza mtu mwingine kwa utulivu maadamu anazungumza. Sio Sunnah kuanza kusema unachotaka kusema kwa kufupisha mazungumzo yake.

7. Usicheke kwa sauti kubwa wakati wa kuzungumza, au katika hali yoyote. Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم hakuwahi kucheka kwa sauti kubwa.

8. Kuzungumza kupita kiasi na kucheka kwa sauti mara kwa mara huharibu heshima ya mtu.

9. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: "Unapomuona mtu ambaye amepewa baraka ya kutengwa na dunia na kusema machache, basi uwe na ukaribu wake na ushirika wake, kwani amebarikiwa na hekima. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 4, uk. 422, Hadithi ya 4101)*

10. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mtu anayenyamaza anapata wokovu.' *(Tirmizi juzuu ya nne kurasa 225 Hadithi nambari 2509)*

Imam Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Kuna aina nne za mazungumzo:

a) Yenye madhara kamili

b) Yenye manufaa kamili

c) Yenye yote mawili yaani manufaa na madhara

d) Haina madhara wala manufaa.

Ni muhimu kujiepusha kila mara na mazungumzo yenye madhara kamili; shiriki kwenye mazungumzo yenye manufaa kamili. Ikiwa mazungumzo yana manufaa na madhara, basi uwe mwangalifu kwa sababu ni bora kujiepusha nayo. Aina ya nne ya mazungumzo ni ya kupoteza muda pekee. Ni vigumu kutofautisha mazungumzo haya; kwa hiyo, kukaa kimya ni bora zaidi. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 6, uk. 464, muhtasari)*

11. Unapozungumza na mtu, kunapaswa kuwa na madhumuni mahususi ya mazungumzo, na kila mara zungumza na watu kulingana na saikolojia na hisia zao.

12. Epuka kutumia lugha chafu na isiyofaa kila wakati. Epuka kuapa. Kumbuka! Kumtukana Muislamu bila ya idhini ya Shariyyah ni haramu kabisa. *(Fatawa Razawiyyah, juz. 21, uk. 127, mukhtasari)* Na Pepo ni haramu kwa mwenye kutumia lugha chafu. Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, "Pepo ni haramu kwa mtu anayetumia lugha chafu." *( Kitab-ul-Samt Ma' Mawsua' Al-Imam Ibn Abi Al-Dunya, juz. 27, j. , Raqm 325)*

    Lugha chafu maana yake ni: 'اَلتَّعْبِيْرُ عَنِ الْاُمُوْرِ الْمُسْتَقْبَحَةِ بِالْعِبَارَاتِ الصَّرِيْحَةِ' yaani kujadili mambo ya aibu na machafu kwa uwazi.

*(Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 3, uk. 151)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 17 za kupiga chafya

Misemo miwili yenye baraka ya kipenzi Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

1. Mwenyezi Mungu Mtukufu anapenda kupiga chafya na hapendi miayo. *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 163, Hadithi ya 6226)*

2. Anapopiga chafya mtu na kusema اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ, Malaika husema 'رَبِّ الْعٰلَمِيْن', na akisema 'رَبِّ الْعٰلَمِيْن', Malaika husema: 'يَرْحَمُكَ الله' yaani Mwenyezi Mungu akurehemu *(Mu'jam-e-Kabeer, juzuu ya 11, uk. 358, Hadithi ya 12284)*

3. Unapopiga chafya, inamisha kichwa chako, funika mdomo wako na piga chafya kwa sauti ya chini; ni upumbavu kupiga chafya kwa sauti kubwa. *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 684)*

4. Mtu aseme اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ baada ya kupiga chafya. (Imeelezwa katika ukurasa wa 3 wa Khaza`in-ul-'Irfan kwa kurejelea Tahtaawi kwamba ni Sunnah muakkadah [imesisitizwa] kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu baada ya kupiga chafya). *(Haashiyah Tahtaawi Ala Al-Maraqi, uk. 7)* Ni bora kusema 'اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ' au 'اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَلٰى كُلِّ حَال'.

5. Ni wajibu kwa msikilizaji kusema 'يَرْحَمُكَ الله' (yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu akurehemu!) mara moja kwa sauti ya kusikika ili aliyepiga chafya asikie. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 476-477, muhtasari)*

6. Akiisikia jibu hiyo, mtu aliyepiga chafya anapaswa kusema:

   'يَغْفِرُ اللهُ لَنَا وَلَكُمْ' (yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu atusamehe sisi na nyinyi!) au sema: 'يَهْدِيْكُمُ اللهُ، وَيُصْلِحُ بَالَكُمْ' Mwenyezi Mungu akuongoze na aboreshe hali yako! *(Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 326)*

7. Mwenye kusema 'اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَلٰى كُلِّ حَال' baada ya kupiga chafya na kupitisha ulimi wake juu ya meno yake yote, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ atasalimika na maradhi ya meno. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 6, uk. 396)*

8. Sayyiduna 'Ali رَضِىَ اللّٰهُ عَنْهُ amesema: "Mwenye kusema 'اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَلٰى كُلِّ حَال' kwa kupiga chafya, hatapatwa na maumivu ya meno wala hatapata maumivu ya masikio.

   *(Mirqat-ul-Mafatih, juzuu ya 8, uk. 499, chini ya Hadithi ya 4739)*

9. Mwenye kupiga chafya amsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu [i.e. sema حَمْد] kwa sauti ili mtu asikilize kisha yeye ajibu. *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 684)*

10. Jibu la kupiga chafya ni wajib kwenye chafya ya kwanza. Ikiwa mwenye kupiga chafya atasema اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ kwenye chafya ya pili vile vile, si wajibu kujibu, bali ni mustahab.
*(Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 326 | Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 476)*

11. Jibu litakuwa wajib pale tu mwenye kupiga chafya atakaposema اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ; asiposema حَمْد, hakuna jibu.
*(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 477)*

12. Ikiwa mtu atapiga chafya wakati wa khutba ya Ijumaa, yule anayeisikia hatakiwi kumjibu. *(Fatawa Qazi Khan, juzuu ya 2, uk. 377)*

13. Ikiwa kuna ndugu wengi wa Kiislamu waliopo na wengine wamejibu, jibu lao litatosha kwa niaba ya kila mtu. Walakini, ni bora kwa kila mtu kujibu.
*(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 684)*

14. Mtu akipiga chafya nyuma ya ukuta na akasema اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ, basi mwenye kusikia ajibu. *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 684)*

15. Mtu akipiga chafya wakati wa Swala basi anyamaze, na akisema اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ, haitaathiri Swalah yake. Ikiwa hatatamka hamd wakati wa Swalah, basi aitamke baada ya kukamilisha Swalah. *(Aalamgiri, juzuu ya 1, uk. 98)*

16. Ikiwa mtu atapiga chafya wakati wewe unaswali na ukasema اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ, kwa nia ya kujibu, Swalah yako itabatilika. *(Aalamgiri, juzuu ya 1, uk. 98)*

17. Mkafiri Akisema اَلۡحَمۡدُ لِلّٰهِ, baada ya kupiga chafya, mtu aseme ‘يَهۡدِيۡكُمُ اللّٰهُ’ (yaani Mwenyezi Mungu Mtukufu akuongoze!) katika kujibu.

*(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 684)*

صَلُّوۡا عَلَى الۡحَبِيۡب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 4 za
# Kupaka wanja (kohl)

1. Kauli ya Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم : “Kohl / wanja bora miongoni mwa yote ni ‘Ismid’ kwani inaboresha nguvu ya kuona na kusababisha kope kuota.” *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 4, uk. 115, Hadithi ya 3497)*

2. Hakuna ubaya kutumia kohl / wanja iliyotengenezwa kwa mawe. Hata hivyo, ni makruh kwa wanaume kutumia kohl au kajal (wanja) nyeusi kwa nia ya kujipamba, lakini haichukizwi ikiwa kujipamba sio makusudio. *(Fatawa Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 359)*

3. Ni Sunnah kutumia kohl (wanja) wakati wa kulala usiku. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 6, uk. 180)*

4. Huu hapa ni muhtasari wa mbinu tatu zilizosimuliwa za kutumia kohl (wanja) :

   i. Wakati mwingine, ipake mara tatu kwa kila jicho.

   ii. Wakati mwingine, ipake mara tatu kwenye jicho la kulia na mara mbili katika jicho la kushoto.

   iii. Wakati mwingine, ipake mara mbili kwa kila jicho na mwisho, chukua kifaa cha kupaka na uweke ndani ya

chombo chenye wanja ili kohl (wanja) ijipake juu yake, kisha tumia hicho kifaa kwa kila jicho moja baada ya nyingine. إِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Kupaka kwa njia hii kutatimiza njia zote tatu. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 5, uk. 218,219)*

Enyi waja wa Rasuli! Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akianza amali zote za heshima kutoka upande wa kulia, basi weka kohl (wanaj) kwenye jicho la kulia kwanza kisha kwa jicho la kushoto.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 15 za
# Kuamka

1. Tikisa matandiko vizuri kabla ya kulala ili ikiwa kuna mdudu hatari n.k., aweze Kutoweka.

2. Soma dua hii kabla ya kulala:

   اَللّٰهُمَّ بِاسْمِكَ اَمُوْتُ وَاَحْيَا

   Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Ninakufa na kuishi kwa jina lako (yaani kulala na kuamka). *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 196, Hadithi ya 6325)*

3. Usilale baada ya swala ya 'Asr kwani kuna khofu ya kupoteza akili. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenye kulala baada ya swala ya 'Asr na kupoteza akili yake basi ajilaumu mwenyewe.

   *(Musnad Abu Ya'la, juzuu ya 4, uk. 278, Hadithi ya 4897)*

4. Ni mustahabu kulala wakati wa mchana.

   *(Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 376 | Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 435)*

5. Ni makruh kulala mwanzo wa siku na katika wakati wa baina ya Maghrib na 'Isha. *(Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 376)*
6. Ni mustahabu kulala katika hali ya twahara.
7. Kwanza lala upande wa kulia [wa mwili] ukielekea Qiblah na mkono wa kulia uwe chini ya shavu la kulia kwa muda fulani, na kisha ulale upande wa kushoto. *(Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 376)*
8. Likumbuke kaburi lako unapolala, kwani tutakuwa peke yetu kaburini na hakutakuwa na mtu ila matendo yetu.
9. Jishughulishe na kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wa kulala. Soma لَا اِلٰهَ اِلَّا الله, سُبْحٰنَ اللّٰه na اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ mpaka ulale, kwani mtu huinuka katika hali ile ile atakayo lala na atainushwa siku ya Qiyama katika hali ile ile atakayo kufa. *(Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 376)*
10. Soma dua hii baada ya kuamka:

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْٓ اَحْيَانَا بَعْدَ مَآ اَمَاتَنَا، وَاِلَيْهِ النُّشُوْرُ

Tafsiri: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyetujaalia maisha baada ya kufa na Kwake tunapaswa kurejea. *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 196, Hadithi ya 6325)*

11. Weka nia madhubuti juu ya kuamka kwamba utakuwa mwenye kujiepusha kutoka matamanio na utakuwa mchamungu na hautawaudhi wengine.

*(Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 376)*

12. Wavulana na wasichana wanapofikia umri wa miaka 10, wafanye walale tofauti. Mvulana wa umri huu hatakiwi kulala na wavulana wa rika moja wala na wanaume waliomzidi umri.

*(Durr-e-Mukhtar Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 629)*

13. Wakati mume na mke wake wanalala kitanda kimoja, wasiwe na mtoto wa miaka kumi awe amelala pamoja nao. Hukumu za wanaume zitatumika kwa mvulana anapokuwa amepevuka umri wa kuhisi matamanio. *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 9, uk. 630)*

14. Tumia miswak baada ya kuamka.

15. Timiza swala ya Tahajjud baada ya kuamka usiku kwani ni fursa ya kufanya hivyo. Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Baada ya swala za fardhi, Swala bora ni swala ya usiku.

*(Muslim, uk. 591, Hadithi ya 1163)*

## Sunnah na adabu 22 kuhusu nywele na Mtindo wa nywele unaolingana na Sunnah n.k.

1. Zulfayn [Mtindo wa nywele] wa Rasuli Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم wakati mwingine ulikuwa hadi nusu ya masikio yaliyobarikiwa.

2. wakati mwingine, mpaka kwa mwisho wa masikio yaliyobarikiwa

3. na wakati mwingine, yangefikia mabega yaliyobarikiwa. *(Shumaail-ut-Tirmizi, uk. 34, 35, 18)*

4. Mara kwa mara, tunapaswa kufatilia kila moja ya Sunnah hizi tatu. Kwa hivyo, wakati mwingine, tunapaswa kuweka Zulfayn (nywele) zetu chini hadi nusu ya masikio, wakati mwingine kwa mwisho wa masikio, na wakati mwingine mpaka kwa mabega.

5. Sunnah ya kuweka Zulfayn [mtindo wa nywele unaolingana na Sunnah] kwenye mabega mara nyingi ni ngumu zaidi kwa Nafsi zetu. Hata hivyo, kila mtu anapaswa kuifanyia kazi

Sunnah hii angalau mara moja au mbili katika maisha yake. Hata hivyo, ni muhimu kutunza kwamba nywele zisiende chini ya mabega. Urefu wa nywele unaweza kuonekana kwa usahihi wakati nywele zimetota. Kwa hivyo katika siku ambazo nywele zinakua kwa kutekeleza Sunnah hii, chana nywele baada ya kuoga na uangalie vizuri kwamba nywele haziendi chini ya mabega.

6. Bwana wangu, A'la Hadrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Ni Haramu kwa wanaume kuweka nywele chini ya mabega, kama wanawake wanavyofanya. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 21, uk. 200)*

7. Mwanachuoni mashuhuri wa Shari'ah na Tareeqah, 'Allamah Maulana Mufti Muhammad Amjad 'Ali A'zami رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Haijuzu kwa mwanamume kuwa na nywele ndefu kama mwanamke. Wengine wanaoitwa Masufi [mystic] huweka nywele ndefu sana ambazo zinaning'inia kwenye kifua chao kama nyoka, na baadhi yao husuka nywele zao sawa na za wanawake. Haya yote hayaruhusiwi na ni kinyume na Shari'ah. Ucha Mungu hauko katika kuota nywele na kuvaa nguo za rangi, bali upo katika kumtii kipenzi Rasuli صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم na kukataa matamanio ya Nafsi na kujitolea kabisa. *(Bahar-e Shari'at, juzuu ya 3, sehemu ya 16, uk. 587)*

8. Ni Haramu kwa mwanamke kunyoa kichwa. *(Imefupishwa kutoka: Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 664)*

9. Haijuzu na ni dhambi kwa mwanamke kukata nywele zake kama vile wanawake makafiri walivyoanza kunyoa nywele zao; jambo hilo limelaaniwa. Hukumu hiyo hiyo itatumika hata ikiwa mume atamwomba mke wake afanye jambo kama hilo. Mwanamke akifanya hivyo atakuwa ni mwenye dhambi, kwa sababu hakuna mtu [mama, baba au mume n.k.] anayepaswa

kutiiwa ikiwa kuna jambo la kuasi Shari'ah. Usikate nywele za wasichana wadogo sawa na nywele za wanaume. Kuanzia utotoni, fanya tabia zao kuwa na nywele kama wanawake. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 588)*

10. Watu wengine hugawanya nywele kwa upande wa kulia au wa kushoto. Hii ni kinyume na Sunnah.
11. Ikiwa mtu ana nywele kichwani, Sunnah ni kutenganisha katikati. *(Bahar-e Shari'at, juzuu ya 3, sehemu ya 16, uk. 587)*
12. Mwanamume ana chaguo ama kunyoa kichwa chake au,kuwacha nywele zimee halafi atenganishe katikati.
13. Yote mawili yamethibiti kutoka kwa Rasuli Mpenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Ingawa kunyoa kunathibitishwa tu wakati wa Ihram, na sio wakati mwengine wowote. *(Bahar-e-Shari'at juzuu ya 3 uk. 586)*
14. Siku hizi, nywele hukatwa kwa mtindo fulani, kwa kutumia makasi au mashine, na kufanya sehemu fulani ya nywele kuwa ndefu na sehemu nyingine fupi. Sio Sunnah kuwa na mtindo wa nywele kama hiyo.
15. Kauli Ya Rasuli Kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Mwenye nywele na aziheshimu (yaani azioshe, azipake mafuta na azichane). *(Sunan Abi Dawood, juzuu ya 4, uk. 103, Hadees 4163)*
16. Sayyiduna Ibrahim Khaleelullah عَلَيْهِ السَّلَام alikuwa wa kwanza kupunguza nywele za masharubu, na wa kwanza kuona nywele nyeupe. Akasema عَلَيْهِ السَّلَام, 'Ewe Mola عَزَّوَجَلَّ! Hii Ni nini?' Allah عَزَّوَجَلَّ akajibu, 'Ewe Ibraahiym! Huu ndio ukuu wako.' Akasema عَلَيْهِ السَّلَام ,'Ewe Mola wangu! Niongezee ukuu wangu.' *(Muwatta, gombo la 2, uk. 415, Hadees 1756)*

Mufassir Hakeem Ul Ummat Hadrat Mufti Ahmed Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema kuhusu hii Hadees: Kabla yake (Sayyiduna Ibraheem Khaleelullah) hakuna masharubu ya nabii yeyote iliyokua zaidi au ilikua na ikapunguzwa nao, lakini ilikuwa hawakuamrishwa katika Shari´ah zao kupunguza masharubu. Sasa kutokana na yeye (Sayyiduna Ibrahim Khaleelullah عَلَيْهِ السَّلَام, kitendo hiki kikawa ni Sunnah ya Ibrahim.

17. Ni Bid'ah [uzushi] kunyoa au kung'oa nywele kutoka sehemu iliyo kati ya mdomo wa chini na kidevu. *(Fatawa Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 358)*

18. Ni Makruh kunyoa nywele kwenye kitanga cha shingo. *(Alamgiri uk. 357-358)* Lakini inatumika pale mtu anaponyoa tu nywele kwenye kitanga ya shingo na sio nywele za kichwa. Watu wengi hunyoa nywele kwenye shingo zao wakati ndevu zao zimekatwa kwa njia inayolingana na Sunnah. Ikiwa nywele juu ya kichwa nzima hunyolewa, basi pamoja na hili, nywele kwenye kitanga ya shingo inapaswa pia kunyolewa. *(Bahar-e Shari'at, juzuu ya 3, sehemu ya 16, uk. 587)*

19. Imeamrishwa kuzika vitu vinne, nywele, kucha, kipande cha kitambaa anachotumia mwanamke kusafisha damu ya hedhi, na damu. *('Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 358)*

20. Ni Mustahab kwa wanaume kugeuza nywele nyeupe za ndevu na kichwa kuwa nyekundu au njano katika rangi. Kwa kusudio hili, Mehndi [henna] inaweza kutumika.

21. Mtu hapaswi kulala na henna iliyowekwa kwenye ndevu au nywele. Kulingana na Hakeem [mtaalamu wa mitishamba], kulala baada ya kupaka hina kwa njia hii kunaweza kusababisha athari kwenye macho, hii ni hatari kwa macho.

Ushauri huu wa Hakeem [mganga wa mitishamba] ulithibitishwa kwa njia ambayo kipofu aliwahi kufika kwa Sag-e-Madinah [i.e. Ameer-e-Ahl-e-Sunnat دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَة]. Alisema kwamba hakuzaliwa kipofu, lakini kwa kusikitisha, alipaka hinna kwenye nywele zake kisha akalala. Alipozinduka, alikuwa amepoteza uwezo wa kuona.

22. Weupe wa nywele za masharubu, mdomo wa chini, na kando ya ndevu za watu hao wanaotumia henna huonekana baada ya siku chache tu na hii haionekani kuwa nzuri. Kwa hiyo, ikiwa huwezi kurudia rangi ya ndevu nzima, basi baada ya kila siku nne, angalau jaribu kutumia kiasi kidogo cha henna kwenye sehemu ambazo weupe huonekana.

## Sunna na adabu 19 za kupaka mafuta na kuchana nywele.

1. Sayyiduna Anas رَضِىَ اللهُ عَنْهُ amesema kwamba Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akipaka mara nyingi mafuta kichwani mwake kilichobarikiwa na kuchana ndevu zilizobarikiwa na yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mara nyingi alikuwa akiweka kitambaa (Sarband Shareef) kichwani kilichobarikiwa, hata kwa kiwango ambacho kitambaa kilikuwa na unyevu wa mafuta. *(Ash-Shumaail-ul-Muhammadiyyah, uk. 40, Hadiyth 32)*

Kutokana na hili, tunapata kujua kwamba matumizi ya 'Sarband' ni Sunnah. Ndugu wa Kiislamu wanapaswa kuvaa kitambaa kidogo juu ya vichwa vyao kila wanapopaka mafuta vichwani mwao, kwa hili, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ kofia ya kitambaa na kilemba vitabakia kulindwa kutokana na mafuta kwa kiasi kikubwa. اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ, Sag-e-Madinah عُفِيَ عَنْهُ amekuwa akitumia

'Sarband' kwa nia ya kutenda Sunnah kwa miaka mingi. Aala Hazrat amesema,

*Tayl ki bondayn tapakti nahin balon say Raza*

*Subh 'Ariz peh lutatay hayn sitaray gaysu*

*(Hadaiq-e-Bakhshish, p. 121)*

2. Kauli ya Rasuli Mtukufu صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Mwenye nywele , aziheshimu. *(Sunan Abi Dawood, juzuu ya 4, uk. 103, Hadithi 4163)* yaani anapaswa kuziosha, kuzipaka mafuta na kuzichana.

*(Ashi'a-tul-Lam'aat, juzuu ya 3, uk. 617)*

Harufu mbaya mara nyingi hutoka kwa nywele za wale ambao hawaoshi nywele na ndevu zao kwa sabuni nk., ingawa wao wenyewe hawajui lakini wengine wanaweza kuhisi. Ni Haramu (imekatazwa) kuingia Msikitini ikiwa harufu mbaya itatoka mdomoni, kwenye nywele, mwilini na kwenye nguo n.k., kwani inaleta matatizo kwa Malaika na watu.

3. Sayyiduna Naafi' رَضِیَ اللهُ عَنْهُ amehadithia: Sayyiduna Ibn 'Umar رَضِیَ اللهُ عَنْهُمَا alikuwa akipaka mafuta katika nywele zake mara mbili kwa siku. *(Musannaf Ibn Abi Shaybah, juzuu ya 6, uk. 117)*

Kupaka nywele mafuta mara kwa mara ni muhimu hasa kwa wasomi kwani huzuia mba, huburudisha ubongo na kujenga kumbukumbu imara.

4. Kauli Ya Rasuli Kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم: Mtu miongoni mwenu akipaka mafuta, aanze na nyusi, huondoa maumivu ya kichwa. *(Al-Jami'-us-Sagheer, uk. 28, Hadiyth 369)*

5. Kila wakati Mtume wetu Mpenzi صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم angepaka mafuta, kwanza angemimina mafuta kwenye kiganja chake cha kushoto, kisha angepaka mafuta nyusi zote mbili

zilizobarikiwa, kisha macho yenye baraka [yaani kope zake zilizobarikiwa] na kisha kichwa kilichobarikiwa. *(Kanz-ul-'Ummal, juzuu ya 7, uk. 46, Raqm 18295)*

6. Imepokewa katika Tabarani: Wakati Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alipopaka mafuta katika ndevu zilizobarikiwa, yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. angeanza na 'Anfaqah (yaani nywele zilizoota katikati ya mdomo wa chini na kidevu). *(Al-Mu'jam-ul-Awsat, juzuu ya 5, uk. 366, Hadiyth 7629)*

7. Ni Sunnah kuchana ndevu. *(Ashi'a-tul-Lam'aat, juzuu ya 3, uk. 616)*

8. Ni kinyume cha Sunnah kupaka mafuta bila ya kusoma 'بِسمِ الله' na kuweka nywele kavu na katika hali ya kutochanwa.

9. Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa: Mwenye kupaka mafuta bila ya kusoma (بِسمِ الله), Mashetani sabini hufuatana naye. *('Amal-ul-Yawm wal-Laylah, juzuu ya 1, uk. 327, Hadiyth 173)*

10. Hujjat-ul-Islam Sayyiduna Imaam Muhammad Bin Muhammad bin Muhammad Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ. amesema: Hapo zamani za kale, Shetani aliyekuwa akifuatana na Mwislamu wa kweli alikutana na Shetani aliyekuwa akifuatana na kafiri. Shetani wa kafiri alikuwa na afya njema na amevaa vizuri, ambapo Shetani aliyeandamana na Mwislamu alikuwa dhaifu, amevuliwa nguo na nywele zake hazikuchanwa. Shetani aliyekuwa akifuatana na kafiri akamuuliza Shetani aliyefuatana na Mwislamu: Kwa nini wewe ni dhaifu sana? Akajibu: Mimi hufuatana na mtu wa namna hiyo ambaye anasoma 'بِسمِ الله' wakati wa kula na kunywa hivyo basi mimi hubakia na njaa na kiu. Anasoma 'بِسمِ الله' huku anapaka mafuta ili nywele zangu ziachwe bila kuchana.

Alipoisikia, Shetani akifuatana na kafiri akasema: Mimi naandamana na mtu kama huyo asiyefanya chochote (yaani hasomi 'بِسمِ اللهِ'] wakati wa kufanya vitendo hivi hivyo najihusisha naye katika kula, kunywa (maji n.k.), kuvaa na kupaka mafuta. *(Ihya-ul-'Uloom, juzuu ya 3, uk. 45)*

11. Kabla ya kupaka mafuta, soma 'بِسمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْم' na mimina mafuta kidogo kwenye kiganja cha mkono wa kushoto. Kisha, kwanza paka mafuta nyusi za jicho la kulia, kisha za jicho la kushoto, kisha kope za jicho la kulia, kisha za jicho la kushoto, na kisha nywele za mafuta. Ikiwa ndevu zinapakwa mafuta, anza na nywele zilizokua kati ya mdomo wa chini na kidevu.

12. Wakati mtu anayetumia mafuta ya haradali anapoondoa kofia au kilemba, wakati mwingine harufu mbaya hutoka. Kwa hiyo, yeyote anayeweza kumudu, anapaswa kutumia mafuta yenye harufu nzuri kwa kichwa. Njia rahisi ya kutengeneza mafuta yenye harufu nzuri ni kuongeza matone ya 'Itr yako uipendayo kwenye chupa ya mafuta ya nazi na kuyayeyusha, mafuta yenye harufu nzuri sasa yako tayari kutumika. Osha nywele za kichwa na ndevu kwa sabuni mara kwa mara.

13. Wanawake lazima wafiche nywele zinazoanguka wakati wa kuchana au kuosha, ili kwamba hakuna mgeni (yaani mtu ambaye Nikah si Haraam kwake milele) aweze kuziona.

*(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 449)*

14. Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amekataza kuchana nywele kila siku. *(Sunan-ut-Tirmizi, juzuu ya 3, uk. 293, Hadees 1762)*

Makatazo haya ni (Makruh) Tanzeehi na makusudio yake ni kwamba mwanamume asibaki na shughuli ya kujipamba. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 592)*

Imaam Manaawi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Iwapo mtu atahitaji kuchana kutokana na fugo la nywele, anaweza kuchana kila siku bila wasiwasi. *(Fayd-ul-Qadeer, juzuu ya 6, uk. 404)*

Limetajwa hapa swali lenye jibu lake aliloulizwa kiongozi wa Ahl-us-Sunnah, Imam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه.

15. **Swali:** ndevu zinapaswa kuchanwa saa ngapi?

    **Jibu:** Hakuna muda maalumu uliowekwa katika Shari'ah kuchana, imeamrishwa kuchukua wastani, wala mwanamume asimfanye aonekane wa kiajabu wala asibaki na shughuli ya kujipamba kila wakati.

    *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 29, uk. 92, 94)*

16. Anza na upande wa kulia wakati wa kuchana. Umm-ul-Mu`mineen, Sayyidatuna 'Aaishah Siddiqah رَضِىَ اللهُ عَنْهَا amesema: Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alipenda kuanza kufanya kila kitu kwa upande wa kulia; hata kuvaa viatu, kuchana, na kupata usafi. *(Sahih Bukhari, juzuu ya 1, uk. 81, Hadiyth 168)*

    Mfasiri wa Sahih Bukhari, 'Allamah Badruddin 'Ayni Hanafi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika kuhusu Hadiyth hii: Mambo matatu haya yametajwa kuwa ni mifano tu, vinginevyo ni Mustahab kuanza kwa upande wa kulia kila jambo la haki na wema. Kama vile kuingia Msikitini, kuvaa mavazi, kutumia Miswak, kupaka wanja, kukata kucha na masharubu, kunyoa makwapa, kufanya wudhu, kuoga, kutoka chooni n.k., na vitendo ambavyo si vizuri kama vile kutoka Msikitini, kuingia chooni, kupuliza. pua, kuondoa suruali (Shalwar) na nguo, ni Mustahab kuanza na upande wa kushoto. *('Umda-tul-Qaari, juzuu ya 2, uk. 476)*

17. Ni Mustahab kupaka mafuta na manukato kwa ajili ya Swalah ya Jumu'ah. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 774)*

18. Sio Makruh kupaka mafuta kwenye ndevu na masharubu wakati wa kufunga, lakini ikiwa mtu atapaka mafuta kwa nia ya kufuga ndevu licha ya kuwa tayari amevaa ndevu zinazofikia urefu wa ngumi, sasa ni Makruh hata kama hajafunga, na makruhu ya daraja la juu zaidi ikiwa amefunga. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 774-997)*

19. Hairuhusiwi na ni dhambi kuchana nywele za ndevu au kichwa cha marehemu. *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 3, uk. 104)* Watu hunyoa ndevu za marehemu, hii pia hairuhusiwi na ni dhambi. Marehemu hatakuwa mwenye dhambi bali wale walionyoa au walioamuru kunyoa ndio watakuwa na dhambi.

## Sunnah na Adabu 22 kuhusu Miswak

Kwanza, kauli mbili zilizobarikiwa za Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم yamewasilishwa hapa chini:

1. Rak'aat mbili zinazotolewa baada ya kufanya Miswak ni bora kuliko Rak'aat 70 zinazotolewa bila Miswak. *(Attargheeb Wattarheeb, juzuu ya 1, uk. 102, Hadees 18)*

2. Jilazimishe kutumia Miswak kwa sababu ndio sababu ya usafi wa kinywa na radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ.

*(Musnad Imam Ahmad, juzuu ya 2, uk. 438, Hadiyth 5869)*

3. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akitumia miswak mara nyingi kila usiku. Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akitumia miswak kila mara wakati wa kulala na kuamka. *(Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 1, uk. 1019)*

4. Bila nia njema, ukitumia miswak, utapata manufaa yake ya kiasili lakini hutapata malipo (thawabu). Kwa mfano, ikibidi utumie miswak kwa ajili ya wudhu, fanya makusudio matatu

kama haya: Nitatumia miswak ili nisafishe kinywa changu kwa ajili ya kumridhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kufuata Sunna na kufanya zikr na kusoma Swalah yenye baraka.

5. Wanachuoni waheshimiwa wanasema kwamba mwenye kutumia Miswak mara kwa mara, atabarikiwa kusoma Kalimah wakati wa kifo chake, na mwenye kula kasumba hatabarikiwa kusoma Kalimah wakati wa kifo chake. *(bahar e Shariat, juzuu ya kwanza , kur. 288)*

6. Seyyiduna Abdullah Ibn Abbas رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُمَا amesimulia kuwa Miswak ina sifa kumi: Inasafisha kinywa, inatia nguvu fizi, inaboresha macho, inaondoa kohozi, inaondoa harufu mbaya ya mdomoni, ni kufuata sunnah,malaika hufurahia, Inafurahisha Mwenyezi Mungu, huongeza matendo mema na inaboresha kazi za tumbo. *(Jam'-ul-Jawami', juzuu ya 5, uk. 249, Hadiyth 14867)*

7. Sayyiduna 'Abdul Wahhab Sha'rani رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesimulia: Mara moja, Sayyiduna Abu Bakr Shibli Baghdadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alihitaji Miswak alipokuwa akifanya wudhu. Aliitafuta lakini hakuiona. Basi yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه akanunua Miswak kwa dinari moja (yaani sarafu ya dhahabu) na akaitumia. Baadhi ya watu wakamwambia, 'Umetumia pesa nyingi sana kwa ajili ya jambo hilo! Je, mtu atumie pesa nyingi kiasi hiki kwa Miswak?' Akajibu رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه, 'Bila shaka, dunia hii na vyote vilivyomo havina thamani hata sawa na bawa la mbu katika mahakama ya Mwenyezi Mungu. Nitajibu vipi ikiwa, Siku ya Kiyama, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ataniuliza, 'Kwa nini umeiacha Sunnah (Miswak) ya Kipenzi Changu Rasuli صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم? Uhalisia wa pesa na mali nilizokupa hazilingani hata kidogo na bawa la mbu, basi baada ya yote, kwa nini hukutumia mali hiyo isiyo

muhimu kwa ajili ya kukamilisha Sunnah hiyo kubwa (Miswak)?'*(Imetolewa kutoka: Lawaqa-ul-Anwaar, uk. 38)*

8. Sayyiduna Imamu Shaafi'i رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Mambo manne yanaongeza akili: kujiepusha na mazungumzo yasiyo na faida, kutumia Miswak, kundi la watu wema na kutenda juu ya elimu yako, *(Hayat- ul- hayawan juzuu 2, ukurasa wa 166)*

9. Miswak inapaswa kuwa ya Peelu, Zaytoon, Neem n.k yaani mti yenye ladha chungu.

10. Unene wa Miswak unapaswa kuwa sawa na ule wa kidole kidogo.

11. Miswak haipaswi kuwa refu zaidi ya mkono mmoja. Vinginevyo, Shetani huketi juu yake.

12. Kamba za Miswak zinapaswa kuwa laini. Vinginevyo husababisha nafasi kati ya meno na ufizi.

13. Ikiwa Miswak ni bichi, basi ni bora. Vinginevyo iweke kwenye glasi ya maji ili iwe laini.

14. Inafaa kupunguza nyuzi za Miswak kila siku.

15. Piga mswaki meno yako kwa mtindo wa mlalo kwa kutumia Miswak.

16. Wakati wowote unapotumia Miswak, itumie mara tatu.

17. Na suuza baada ya kila wakati.

18. Shika Miswak kwa mkono wa kulia kwa namna ambayo kidole kidogo kibaki chini, vidole vitatu vya kati vikibaki juu yake, huku kidole gumba kikibaki juu (karibu na nyuzi laini zinazotumika kupigia mswaki).

19. Kwanza brashi (kwa Miswak) meno ya juu ya upande wa kulia na kisha kushoto. Baada ya hapo, safisha meno ya chini kuanzia upande wa kulia na kisha kushoto.

20. Kutumia Miswak kwa kuishika na ngumi kunaleta hatari ya milundo.

21. Miswak ni Sunnah ya kufanywa kabla ya Wudhu, lakini ikiwa mtu ana harufu mbaya mdomoni, basi kutumia Miswak inakuwa Sunnat-ul-Muakkadah.

*(Imetolewa kutoka: Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 1, uk. 623)*

22. Usitupe Miswak iliyotumika kwani ni chombo kinachotumika kufanyia Sunnah. Badala yake, iweke mahali fulani kwa heshima, uizike au uiweke baharini baada ya kuifunga kwa mawe au kitu kizito n.k.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunna na Adabu 10 za
# Kukata Kucha

1. Ni mustahab kukata kucha siku ya Ijumaa. Hata hivyo, mtu hapaswi kusubiri Ijumaa ikiwa kucha yake imeongezeka kwa muda mrefu. *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 9, uk. 668)* Imepokewa: Yeyote anayekata kucha siku ya Ijumaa, Mwenyezi Mungu Mtukufu atamlinda na misiba mpaka Ijumaa ijayo na kwa siku tatu baada ya hapo, yaani kwa siku kumi kwa jumla. Imepokewa pia kuwa: Atakayekata kucha siku ya Ijumaa, atamiminwa rehema na madhambi yake yataondolewa. *(Radd-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 668-669 | Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 583)*

2. Ufuatao ni mukhtasari wa njia iliyosimuliwa ya kukata kucha: Anza na kidole cha shahada cha mkono wa kulia na kata kucha zako kwa mpangilio hadi kwenye kidole kidogo lakini usikate ukucha wa kidole gumba. Sasa, ukianza na kidole kidogo cha mkono wa kushoto, kata kucha zako kwa mpangilio ikiwa ni pamoja na ile ya kidole gumba. Mwishoni, kata kucha ya kidole gumba cha mkono wa kulia. *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 9, uk. 670 | Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 1, uk. 193)*

3. Hakuna mpangilio maalum wa kukata kucha za vidole vya miguu umesimuliwa. Ni bora kuanza kutoka kidole kidogo kwenye mguu wa kulia na kukata kwa utaratibu, ikiwa ni pamoja na kucha ya kidole kigumba kikubwa, kisha kata kucha ya mguu wa kushoto kwa utaratibu, kuanzia na kidole kikubwa mpaka pamoja na kidole kidogo. *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 9, uk. 670 | Ihya`-ul-'Uloom, juzuu ya 1, uk. 193)*

4. Ni makruh [tanzeehi] kukata kucha katika hali ya kutokuwa na tohara, yaani wakati wa kuoga ni wajibu. *(Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 358)*

5. Ni makruh [tanzeehi] kuuma kucha kwa meno. Kuna hofu ya kupata *leukoderma* kwa kufanya hivyo. *(Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 358)*

6. Zika kucha baada ya kuzikata. Zinaweza pia kutupwa mbali. *(Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 358)*

7. Ni makruh [tanzeehi] kurusha kucha chooni au bafuni kwani hii husababisha magonjwa. *(Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 358)*

8. Kucha haipaswi kukatwa siku ya Jumatano kwa sababu hii inaweza kusababisha *leukoderma*. Lakini ikiwa mtu hajakata kucha kwa muda wa siku 39, na Jumatano ikawa siku ya 40, (yaani ikiwa hatakata kucha siku hiyo, muda wake utazidi siku 40), ni wajibu kwake kukata kucha yake. kucha siku hiyo

[Jumatano] kwani hairuhusiwi na makruh tahreemi kuweka kucha isiyokatwa kwa zaidi ya siku arobaini. (Kwa maelezo ya kina, tafadhali soma kurasa 574 na 685 za Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22 iliyorejelewa. *(Aalamgeer, juzuu ya 5, uk. 358)*

9. Kucha mirefu ni mahali pa kukaa kwa Shetani, yaani, Shetani huketi kwenye kucha ndefu. *(Ittihaf-us-Sadah, juzuu ya 2, uk. 653)*

10. Hakuna ubaya kukata kucha usiku. **Kisa**: Harun Rasheed alimuuliza Imam Abu Yusuf رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه kuhusu kukata kucha usiku. Akajibu, 'Inaruhusiwa.' Haroon Rasheed akauliza kuhusu ushahidi. Akajibu, 'Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa: 'اَلْخَيْرُ لَا يُؤَخَّرُ' yaani Usichelewe kutekeleza kitendo cha wema.' *(Fatawa 'Aalamgeeri, juz. 5, uk. 358)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunnah na Adabu 17

# Za Mavazi

Kwanza, misemo (kauli) mitatu iliyobarikiwa ya Rasuli Mpenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

1. Pazia baina ya macho ya majini na Satr ya watu ni kwamba mtu anapovua nguo yake basi asome 'بِسْمِ اللّٰهِ'. *(Al-Mu'jam-ul-Awsat, juzuu ya 2, uk. 59, Hadiyth 2504)* Mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan Na'eemi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Kama ukuta na mapazia yanavyokuwa kizuizi kwa macho ya watu, vivyo hivyo Zikr hii ya Mwenyezi Mungu itakuwa kizuizi cha macho ya majini . Yaani majini hawataweza kuona (sehemu zake za siri). *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 1, uk. 268)*

2. Atakayevaa nguo zake na akasoma yafuatayo, atasamehewa madhambi yake ya wakati ujao na yaliyopita. *(Shu'ab-ul-Iman, ya 5, uk. 181, Hadiyth 6285)*

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِیْ کَسَانِیْ ھٰذَا، وَرَزَقَنِیْہِ مِنْ غَیْرِحَوْلٍ مِّنِّیْ وَلَاقُوَّۃٍ

Tafsiri: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu aliye nivalisha nguo hii na akanijaalia riziki bila ya nguvu zangu na uwezo wangu. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 5, uk. 181, Hadiyth 6285)*

3. Licha ya kuwa na nyenzo za kuvaa nguo za kifahari, mwenye kuziepuka kutokana na unyenyekevu, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ atamvisha vazi la Karamah. *( Abu Dawood, juzuu ya 4, uk. 326, Hadees 4778)*

4. Tajiri akivaa vazi zuri linaloruhusiwa katika Shariah kwa nia ya kueleza fadhila alizojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, atastahiki malipo.

5. Vazi tukufu la Mtume Mtukufu صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa kawaida lilikuwa la nguo nyeupe. *(Kashf-ul-Iltibas fi Istihbab Lil Libas, uk. 36)*

6. Mtume kipenzi صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: “Bora ya mle mnayokutana nayo Mwenyezi Mungu katika makaburi yenu na misikiti yenu ni nguo nyeupe. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 4, uk. 146, Hadithi ya 3568)* Maana yake ni kwamba, ni vyema kuswali katika nguo nyeupe na kumfanya marehemu avae sanda nyeupe. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 403)*

7. Imam Shafi'i رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Huzuni ya mtu anayeweka nguo yake safi itapungua na akili ya mtu anayepaka manukato itaongezeka.' *(Ihya ul uloom, (Urdu) juzuu ya 1, uk. 561)*

8. Nguo lazima ziwe za mapato ya halali, na hakuna swalah - iwe fard na nafl - inakubaliwa ikiwa inatekelezwa ikiwa imevaliwa

nguo [iliyonunuliwa] na mapato ya haramu. *(Kashf-ul-Iltibas Fi-Istihbab Lil-Libas, p. 39-41)*

9. Imesimuliwa kuwa : mwenye kufunga ‘Imamah (kilemba) yake akiwa amekaa au kuvaa nguo yake ya chini (yaani pajama au suruali) akiwa amesimama, Allah عَزَّوَجَلَّ atamtia maradhi ambayo hayana tiba. *(Kashf-ul-Iltibas Fi-Istihbab Lil-Libas, uk. 39)* Sayyiduna Imam Burhanuddin Zarnooji رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: “Kufunga imamah (kilemba) ukiwa umekaa au kuvaa suruali au shalwar ukiwa umesimama ni sababu za ufukara. *(Ta’leem-ul-Muta’allim, uk. 43-126)*

10. Wakati wa kuvaa nguo, anza kutoka upande wa kulia (kwa sababu ni Sunnah). Kwa mfano, unapovaa kanzu, weka mkono wako wa kulia kwenye mkono wa kulia wa kanzu kwanza na kisha mkono wako wa kushoto kwenye mkono wa kushoto wa kanzu. *(Ta’leem-ul-Muta’allim, pp. 43-126)*

11. Vivyo hivyo, unapovaa vazi la chini (suruali), weka mguu wako wa kulia ndani ya mguu wa kulia wa hiyo suruali kwanza na kisha mguu wako wa kushoto ndani ya mguu wa kushoto wa suruali, na unapovua nguo zako, fanya kinyume chake, yaani anza na upande wa kushoto.

12. Imeelezwa katika ukurasa wa 409, juzuu ya 3 ya kitabu Bahar-e-Shari'at: Ni Sunnah kuwa na urefu wa kamisi hadi nusu ya chini ya mguu, urefu wa mikono ya kamisi hadi kwenye upeo wa vidole, na upana wake unapaswa kuwa wa mkono mmoja. *(Rad-dul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 579)*

13. Ni Sunnah kwa wanaume kuweka sehemu ya chini ya suruali zao/ Tahband juu ya vifundo vya miguu. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 6, uk. 94)*

14. Wanaume wavae mavazi ya kiume pekee na wanawake wavae nguo za kike pekee. Tofauti hii inapaswa pia kuzingatiwa wakati wa kuvisha watoto wadogo. (vinginevyo, wale wanaowafanya wavae nguo hizo watakuwa wenye dhambi). Hata hivyo, vazi ambalo huvaliwa na wanaume na wanawake na watoto (wa kiume na wa kike) linaweza kuvaliwa na wote wawili iwapo Shariah itaruhusu.

15. Imeelezwa katika ukurasa wa 481, juzuu ya 1 ya kitabu Bahar-e-Shari'at: Sehemu ya mwili wa mwanadamu kutoka chini ya kitovu mpaka chini ya magoti ni 'Awrat yaani kuificha ni Fard. kitovu haijajumuishwa ndani yake lakini magoti yanajumuishwa. *(Durr-e-Mukhtar, Rad-dul-Muhtar, juzuu ya 2, uk. 93)* Siku hizi, watu wengi huvaa pajama au Tahband chini ya kitovu kwa njia ambayo sehemu fulani chini ya kitovu hubaki wazi. Ikiwa shati n.k., inafunika eneo hilo kiasi kwamba rangi ya ngozi haionekani, basi ni sawa, vinginevyo ni Haraam. Iwapo robo ya sehemu hiyo itabaki wazi katika Swalah, basi Swalah haitakuwa sahihi. *(Bahar-e-Shari'at, juz. 1, uk. 481)* Yeyote ambaye amevaa Ihram (kwa ajili ya Hajj au 'Umrah) anapaswa kuitunza jambo hili sana.

16. Siku hizi, watu wengi huzunguka huku na huko wakiwa wamevaa kaptula, wakionyesha magoti na mapaja yao. Hii ni Haramu. Kutazama kwenye magoti na mapaja yaliyo wazi ya watu kama hao pia ni Haramu. Mito, uwanja wa michezo na ukumbi wa michezo ni vituo vya kawaida vya matukio haya. Kwa hiyo, mtu lazima awe mwangalifu sana ikiwa anapaswa kutembelea maeneo hayo.

17. Nguo inayovaliwa kuonyesha kiburi ni marufuku. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 409; Rad-dul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 579)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunnah na Adabu 25 zinazohusu 'Imamah (Kilemba)

Kauli 7 yaliyobarikiwa ya Mtume Mpendwa صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

1. Rak'aat 2 za Swalah zinazotekelezwa ukiwa umevaa 'Imamah ni bora kuliko kutekeleza Rak'aat 70 bila ya kuvaa 'Imamah.' *(Al-Firdaus bima Soor-il-Khitab, juzuu ya 2, uk. 265, Hadiyth 3233)*

2. Kuvaa 'Imamah juu ya kofia ni tofauti kati yetu na washirikina. Kwa kila mkunjo wa 'Imamah ambao Muislamu huzungushia kichwa chake, atapewa Nuru moja kwa ajili yake Siku ya Hukumu. *(Al-Jami'-us-Sagheer, uk. 353, Hadees 5725)*

3. Bila shaka Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na Malaika wake wanatuma Durud, siku ya Ijumaa, kwa wale wanaovaa 'Imamah. *(Al-Firdaus bima Soor-il-Khitab, juzuu ya 1, uk. 147, Hadees 529)*

4. Kuswali ukiwa umevaa 'Imamah ni sawa na fadhila 10,000. *(Al-Firdaus , juzuu ya 2, uk. 406, Hadees 3805; Fatawa Razawiyyah Mukharrajah juzuu ya 6, uk. 213)*

5. Salat-ul-Jumu'ah moja iliyoswaliwa huku mtu amevaa 'Imamah ni sawa na Salat-ul-Jumu'ah 70 iliyoswaliwa bila ya 'Imamah. *( Ibn 'Asakir, juzuu ya 37, uk. 355)*

6. 'Imaamah ni taji za Waarabu, basi vaeni 'Imamah na utukufu wenu utazidi. Mwenye kufunga 'Imamah anapata fadhila moja kwa kila mkunjo [wa 'Imamah anaouzungushia kichwa chake]. *(Kanz-ul-'Ummal, vol. 15, p. 133, Raqm 41138)*

7. Vaa imamah, uvumilivu wako utaongezeka. *(Mustadrak, juz. 5, uk. 272, Hadithi ya 7488)* Ufafanuzi wa Hadithi: Kwa kuvaa imamah, ustahimilivu wako utaongezeka na kifua chako kitakuwa kipana, kwa sababu ikiwa sura ya mtu ni nzuri, humfanya awe mzito na mwenye heshima na humwokoa kutoka kwa hisia na kutoka kwa shughuli zisizo heshimika. *(Fayz-ul-Qadier, juzuu ya 1, uk. 709, chini ya Hadithi ya 1142)*

8. Imetajwa katika kitabu cha Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3 ukurasa wa 660: Funga 'Imamah ukiwa umesimama, na uvae pajama [i.e. suruali] ukiwa umeketi. Atakayefanya kinyume na hili (yaani afunge ‘Imamah akiwa amekaa, na kuvaa suruali akiwa amesimama); ataugua ugonjwa, ambao hauna tiba.

9. Kabla ya kufunga Imamah fanya nia njema, ikiwa hakuna nia njema hutapata thawabu; kwa hiyo, angalau fanya nia hii kwamba mimi ninafunga Imamah kutenda juu ya Sunnah ya Bwana Mtume na kumridhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu (pia sema hii ikiwa unajiandaa kwa ajili ya Swalah huku umevaa Imamah) na kwa ajili ya kujipamba vizuri kwa ajili ya swalah.

10. Inafaa kukunja mkunjo wa kwanza wa ‘Imamah kuelekea upande wa kulia wa kichwa. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 199)*

11. Shimlah [i.e. mwisho uliofunuliwa] wa Imamah wa kipenzi Rasuli صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa ujumla ulikuwa unaning’inia nyuma (ya mwili wake juu ya mgongo wake) na kwa upande wa mkono wake wa kulia na mara nyingine alikuwa na shimla mbili zinazoning’inia kwa mabega yake mawili yaliyobarikiwa. Kutundika Shimlah kwa upande wa kushoto ni kinyume na Sunnah. *(Ashi’a-tul-Lam’aat, juzuu ya 3, uk. 572)*

12. Urefu wa Shimlah wa ‘Imamah kwa uchache unapaswa kuwa sawa na angalau vidole vinne

13. Na kwa urefu zaidi unafaa kuwa hadi katikati ya mgongo, yaani takriban urefu wa mkono mmoja. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 182)* *(Kutoka ncha ya kidole cha kati hadi kiwiko huitwa urefu wa mkono mmoja.)*

14. Funga ‘Imamah ukiwa umesimama ukielekea Qiblah. *(Kashf-ul-Iltibas Fi Istihbab LIl Libaas, uk. 38)* Imepokewa katika Mirat Sharif: “Ukiwa unafunga imamah msikitini au sehemu nyingine yoyote, ni Sunna kuivaa ukiwa umesimama. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 6, uk. 106)*

15. Sunnah ya ‘Imamah ni kwamba isiwe fupi zaidi ya yadi 2½ kwa urefu, wala isiwe ndefu zaidi ya yadi 6, na ifungwe katika umbo la kuba. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 186)*

16. Ikiwa una kitambaa kikubwa ambacho unaweza kutengeneza mikunjo ya kutosha kufunika kichwa kizima, kitazingatiwa kuwa ni ‘Imamah.

17. Ni Makruh kufunga kitambaa kidogo ambacho mtu anaweza kutengeneza mkunjo mmoja au mbili tu. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 7, uk. 299)*

18. Unapotaka kufunga tena ‘Imamah tena basi fungua kila mkunjo mmoja baada ya mwingine kama ulivyoifunga. Usiitoe yote kwa jumla mara moja tu. *(Aalamgheeri, juzuu ya 5, uk. 330)*

19. Ikiwa Imamah imefunguliwa kwa sababu ya dharura na unakusudia kuifunga tena basi fungua mkunjo moja baada ya moja. Ukifanya hivyo, basi dhambi moja itaondolewa kwa kufungua kila mkunjo wa Imamah. *(Fatawa Razawiyya (iliyorekebishwa) juzuu ya 6, kur. 214, mukhtasari)*

20. Tafadhali soma faida 6 za kiafya za ‘Imamah:

21. Nywele za watu ambao hubakia vichwa wazi zinakabiliwa moja kwa moja na athari za majira ya baridi, majira ya joto na jua. Sio tu husababisha madhara kwa nywele lakini pia madhara ya ubongo na uso na inaweza kusababisha hasara kwa afya ya mtu. Kwa hiyo, kufunga Imamah/kilemba kwa nia ya Sunnah kuna manufaa kwa ulimwengu yote mbili.

22. Kwa mujibu wa utafiti wa kimatibabu, kuvaa Imamah kuna manufaa makubwa kwa maumivu ya kichwa.

23. Imamah huimarisha ubongo na huipa nguvu kumbukumbu.

24. Kuvaa Imamah humweka salama mtu kutokana na baridi kali, ikiwa mvaaji anaugua baridi, athari zake ni ndogo. Shimla ya Imamah huokoa mtu kutokana na kupooza kwa sehemu ya chini ya mwili, kwa sababu Shimla hutoa ulinzi kwa uti wa mgongo kutokana na athari za hali ya hewa k.m. majira ya baridi, majira ya joto nk.

25. Shimla hupunguza hatari ya "سرسام" uvimbe wa ubongo. Ugonjwa wa uvimbe wa ubongo unaitwa "سرسام" *(Phrenitis)*

## Sunnah naAdabu 19 kuhusu uvaaji wa pete

1. Ni Haramu kwa wanaume kuvaa pete ya dhahabu. Rasuli Mpenzi na Mwenye Baraka صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ameharamisha kuvaa pete ya dhahabu. *(Sahih Bukhari, juzuu ya 4, uk. 67, Hadithi 5863)*

2. Ni Haramu kumvisha mtoto mdogo wa kiume(kijana) vito vilivyotengenezwa kwa dhahabu na fedha, na yule mzazi wa mtoto mdogo atakaye fanya hivyo atakuwa ni mwenye dhambi. Mwanamke anaweza kupaka hina mikononi na miguuni mwake lakini akimpaka mvulana hinna atakuwa ni mwenye

dhambi. *(Bahar-e-Shari'at, juz. 3, uk. 428; Durr-e-Mukhtar, Rad-dul-Muhtar, juz. 9, uk. 598)*

3. Pete ya chuma ni vito (pambo) vya wakaaji wa motoni. *(Jami' Tirmizi, juzuu ya 3, uk. 305, Hadees 1792)*

4. Inajuzu kwa wanaume kuvaa pete ya kiume tu yaani ile yenye kito kimoja tu. Ikiwa kuna vito zaidi ya moja au vito vingi, basi haitoruhusiwa kwa wanaume hata ikiwa imetengenezwa kwa fedha. *(Rad-dul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 597)*

5. Hairuhusiwi [kwa wanaume] kuvaa pete bila vito kwani pete isiyo na kito haichukuliwi kuwa pete.

6. Inajuzu kuvaa pete iliyoandikwa Huroof-e-Muqatta'at [herufi za mwanzo wa baadhi ya Sura za Qur'ani] lakini haijuzu kuvaa au kugusa pete hiyo bila ya Wudhu. Kadhalika, haijuzu pia kwa mtu kupeana mikono na aliyevaa pete namna hiyo bila ya Wudhu.

7. Vile vile haijuzu kwa wanaume kuvaa pete zaidi ya moja (kutokamana na pete inayoruhusiwa) au kuvaa pete moja au zaidi kutokamana na pete bila ya kito kwani hizi mbili (pete yenye kito na isiyo na kito ) hutofautiana. Wanawake wanaweza kuvaa pete zisizo na vito. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 428)*

8. Hata bila ya haja ya kutumia pete kama muhuri, inaruhusiwa kuvaa pete ya fedha ambayo ina uzito chini ya 4.5 Masha (yaani gramu 4 na 374 mg) na ambayo ina kito kimoja tu. Hata hivyo, kwa yule ambaye hahitaji kuitumia kama muhuri wake rasmi, ni vyema asivae hata pete inayoruhusiwa. Ama kwa yule anayehitaji kuitumia kama muhuri wake rasmi, si tu kwamba inaruhusiwa bali pia ni Sunna kuvaa aina hiyo ya pete kwa madhumuni yale yale. Hata hivyo, ikiwa mtu ataivaa kwa

kuonyesha kiburi au kuchukua mtindo wa kike au kwa nia nyingine yoyote mbaya, basi haitaruhusiwa kuvaa hata vazi zuri, achilia mbali pete. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 141)*

9. Ni vyema (Mustahab) kuvaa pete wakati wa Eid lakini wanaume wanaweza kuvaa pete ile inayoruhusiwa tu.

10. Kuvaa pete ni Sunnah tu kwa wale wanaohitaji kuitumia kama muhuri rasmi kama vile mfalme, Qadhi na Mufti kupiga Fatawa (na pete). Isipokuwa kwa watu hawa, si Sunnah kwa wale wasiohitaji kuitumia kama muhuri rasmi ingawa inajuzu kuivaa. *(Fatawa 'Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 335)* Pete hazitumiki tena kama stempu bali muhuri fulani hutumika kwa kusudi hili. Kwa hiyo, si Sunnah tena kuvaa pete hata kwa Qadi n.k. ambao hawahitaji kuitumia kama muhuri.

11. Wanaume wanapaswa kuvaa pete kwa njia ambayo kito inabaki kwenye kiganja wakati wanawake wanapaswa kuweka kito nyuma ya mkono. *(Al-Hidayah, juzuu ya 4, uk. 367)*

12. 'Pete' ya fedha isiyo na kito ni mfano wa pambo la kike na, kwa wanaume, ni Makruh (Tahrimi, isiyoruhusiwa na dhambi). *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 130)*

13. Wanawake wanaweza kuvaa pete nyingi za fedha na dhahabu wapendavyo iwe na vito au bila vito. Kwao hakuna kikomo cha uzito wa fedha na dhahabu na idadi ya vito.

14. Ikiwa pete ya chuma imevalishwa fedha mpaka chuma kisionekane kabisa, basi kuvaa pete kama hiyo sio marufuku (wote kwa wanaume na wanawake). *(Fatawa 'Aalamgiri, juzuu ya 5, uk. 335)*

15. Mtu anaweza kuvaa pete kwenye mkono wowote lakini anapaswa kuivaa kwenye kidole kidogo. *(Rad-dul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 596)*

16. Pia hairuhusiwi na ni dhambi kwa wanaume kuvaa bangili ya chuma hata inayohusiana na *Mannat au dham.*

17. Kadhalika, haijuzu kuvaa pete isiyo na kito iliyotengenezwa kwa fedha au chuma chochote au pete ya chuma iliyoletwa kutoka Madinah Munawwarah ama Ajmer.

18. Pia hairuhusiwi kwa wanaume kuvaa pete isiyo na kito iliyotengenezwa kwa fedha au chuma chochote, ambacho *Dam (maombi)* yametolewa, kwa ajili ya kutibu milundo na magonjwa mengine.

19. Iwapo ndugu wa Kiislamu amevaa bangili iliyotengenezwa kwa chuma au pete isiyo na kito au cheni au aina yoyote ya pete isiyoruhusiwa, ni wajibu kwa Shari'ah kuzivua mara moja, atubie kwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na kuweka nia thabiti ya kutokuvaa hizo tena.

## Sunnah na Adabu 25 zinazohusu ´Aqiyqah

1. Kauli ya Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, 'Mvulana analipiwa fidia kwa ajili ya aqeeqah yake.' Mnyama atolewe kafara kwa niaba yake siku ya saba, apewe jina na kichwa chake kinyolewe. *(Tirmizi, juzuu ya 3, uk. 177, Hadithi ya 1527)* Kuwekewa fidia maana yake ni kwamba faida kamili hazitapatikana kutoka kwake isipokuwa aqiiqah yake itekelezwe, na baadhi (muhadithiin) wamesema kwamba usalama wa mtoto, makuzi yake na sifa njema ndani yake huhusishwa na aqeeqah. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 354,355, 357)*

2. Mnyama anapochinjwa kwa shukrani kwa kuzaliwa mtoto, huitwa aqeeqah. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 354,355, 357)*
3. Wakati mtoto anapozaliwa, ni vyema zaidi kuita adhana na iqamat katika masikio yake. Kuita adhana kutaondoa mashaka اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ.
4. Ni bora kuita adhana mara nne katika sikio la kulia na iqamat mara tatu katika sikio la kushoto.
5. Ni desturi ya watu wengi kuita adhana mtoto wa kiume anapozaliwa na mtoto wa kike anapozaliwa hawamwitii Adhana. Haipaswi kufanywa hivyo; adhana na iqamat pia zinapaswa kuitwa wakati mtoto wa kike anapozaliwa.
6. Siku ya saba ya kuzaliwa, mtoto atapewa jina na kichwa chake kinyolewe; aqeeqah yake itekelezwe wakati wa kunyoa kichwa chake. Kiasi cha fedha au dhahabu sawa na uzito wa nywele zilizonyolewa kinapaswa kutolewa kama sadaka. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 354,355,357)*
7. Mbuzi beberu wawili katika aqeeqah ya mvulana na mbuzi yaya mmoja katika aqeeqah ya msichana wachinjwe, yaani kwa mvulana, wanyama wa kiume, na kwa msichana, mnyama wa kike anafaa. Hakuna ubaya ndani yake ikiwa mbuzi yaya watachinjwa katika aqeeqah ya mvulana na mbuzi wa beberu atachinjwa katika aqeeqah ya msichana. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 354,355,357)*
8. Ikiwa mtu hana uwezo wa kumchinjia mwanawe mbuzi wawili, mbuzi mmoja pia atatosha. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 20, uk. 586)*
9. Mtu anaweza kuwa na hisa za aqeeqah hata kwenye ngamia wa kafara, na kadhalika.

10. Aqiiqah si fard wala si wajib, bali ni Sunnah mustahabbah [kama unaweza kumudu ni lazima uifanye, na usipoifanya hutakuwa mtenda dhambi. Hata hivyo, utanyimwa ujira wa aqeeqah.] Haijuzu hata kidogo kwa masikini kutekeleza aqeeqah baada ya kupata mkopo wa riba. *(Islami Zindagi, uk. 27)*

11. Ikiwa mtoto ameaga dunia kabla ya kufikisha umri wa siku saba, na ‘aqeeqah yake haikutekelezwa, hili halitaathiri uwezo wake wa uombezi n.k., kwa sababu amefariki kabla ya wakati wa ‘aqeeqah. Hata hivyo, ikiwa mtoto alikuwa amefikisha umri wa siku saba, lakini´aqeeqah yake haikufanywa bila ya sababu yoyote ya kweli pamoja na kwamba wazazi wake walikuwa na uwezo wa kuitekeleza, imeelezwa kwa mtoto huyo kwamba hatoweza kuwaombea wazazi wake. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 20, uk. 586,596)*

12. Ni Sunnah kufanya´aqeeqah katika siku ya 7 ya kuzaliwa, na hii ni bora zaidi. Inaweza pia kufanywa siku ya 14 au 21 ya kuzaliwa. *(Fatawa Razawiyyah, juz. 20, uk. 586,596)* Ikiwa mtu hawezi kuitekeleza siku ya 7, anaweza kuitekeleza wakati wowote anapotaka. Sunnah itazingatiwa kuwa imetekelezwa. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 3, uk. 356)*

13. Iwapo aqeeqah ya mtu haijatekelezwa, anaweza kutekeleza aqeeqah yake katika ujana wake au katika uzee wake. *(Fatawa Razawiyyah, juz. 20, uk. 588)* Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alitekeleza aqeeqah yake mwenyewe baada ya tangazo la utume. *(Musannaf Abdul Razzaq, juzuu ya 4, uk. 254, Hadithi ya 2174)*

14. Baadhi ya (wanazuoni wa Kiislamu waliobarikiwa) wamesema ni bora kufanya aqeeqah ama siku ya 7, siku ya 14 au siku ya 21 ya kuzaliwa, yaani kuwe na pengo la siku 7. Ikiwa mtu haikumbuki, anapaswa kukumbuka siku ambayo mtoto wake

alizaliwa. Wakati siku iliyotangulia kuzaliwa kwa mtoto inakuja, hii itazingatiwa siku ya saba. Kwa mfano, ikiwa mtoto wake alizaliwa siku ya Ijumaa, basi (kila) Alhamisi (ya maisha yake) ni siku (yake) ya saba. *(Bahar-e-Shari'at, juz. 3, uk. 356)* Ikiwa hatakumbuka siku ya kuzaliwa ya mtoto wake, anaweza kufanya aqeeqah siku yoyote anayotaka.

15. Baada ya kunyoa kichwa cha mtoto, ni bora kusugua zafarani iliyosagwa kichwani mwake. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 357)*

16. Ni bora kutovunja mifupa ya mnyama aliyechinjwa kwa ajili ya aqeeqah, bali nyama iondolewe kwenye mifupa. Hii ni ishara nzuri kwa usalama wa mtoto. Ikiwa nyama hupikwa baada ya kuvunja mifupa, hakuna madhara ndani yake. Nyama inaweza kupikwa kwa njia yoyote, lakini ikiwa imepikwa kwa ladha tamu, ni ishara nzuri kwa mtoto kuwa na tabia nzuri. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 357)*

17. Njia mbili za kupika nyama tamu:

    i. Mimina mafuta au samli kulingana na mahitaji na weka kilo moja ya nyama, nusu kilo ya maziwa mala uliotiwa sukari, vipande 7 vya iliki na gramu 50 za mlozi kwenye sufuria. Baada ya hayo, pika viungo vyote. Baada ya kuchemsha, ongeza sukari ndani yake kulingana na mahitaji. Kwa ajili ya kupamba, karoti zilizokatwa vizuri na zabibu, nk pia inaweza kuongezwa kwake.

    ii. Weka nusu kilo ya beetroot na kilo moja ya nyama kwenye sufuria na uipike kwa njia ya kawaida.

18. Kwa ujumla inaaminika kwamba wazazi na babu wa upamde wa baba na babu wa upande wa mama wa mtoto hawapaswi

kula nyama ya aqeeqah, ambayo ni makosa kabisa, na hakuna uthibitisho wa itikadi hiyo. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 357)*

19. Hukumu za ngozi ya mnyama 'aqeeqah ni sawa na hukumu zinazohusu ngozi ya wanyama wa kafara. Mtu anaweza kuitumia kibinafsi, kuitoa kwa masakeen au kuitoa kwa sababu yoyote nzuri kama msikiti au madrasah. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 357)*

20. Mnyama wa aqeeqah lazima awe chini ya masharti sawa na yaliyowekwa kwa ajili ya mnyama wa kafara. Nyama yake mbichi inaweza kusambazwa kati ya maskini, jamaa na marafiki wa karibu. Inaweza pia kutolewa kwao baada ya kupika, au inaweza kutumika kwao kwenye sikukuu. Kesi hizi zote zinaruhusiwa. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 357)*

21. Kulisha nyama ya aqeeqah kwa korongo na kunguru hakuna maana; wao ni fasiq. (Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 20, uk. 590)

22. Aqeeqah [hufanywa] kwa kushukuru kuzaliwa; kwa hiyo, aqeeqah haiwezi kufanywa baada ya kifo.

23. Wakati wa aqiiqah ya mvulana, baba yake amchinje mnyama na asome dua ifuatayo:

اَللّٰهُمَّ هٰذِهٖ عَقِيْقَةُ ابْنِىْ فُلَانٍ، دَمُهَا بِدَمِهٖ وَلَحْمُهَا بِلَحْمِهٖ، وَعَظْمُهَا بِعَظْمِهٖ وَجِلْدُهَا بِجِلْدِهٖ، وَشَعْرُهَا بِشَعْرِهٖ، اَللّٰهُمَّ اجْعَلْهَا فِدَاءً لِابْنِىْ مِنَ النَّارِ، بِسْمِ اللهِ اَللهُ اَكْبَرـ

Badala ya kusema fulani na fulani, taja jina la mwana. Ikiwa 'aqeeqah ni ya binti, sema neno 'بِنْتِى' badala ya 'اِبْنِى' katika sehemu zote mbili na 'ها' badala ya 'ہٖ' katika sehemu tano. Iwapo yeyote asiyekuwa baba atachinja mnyama huyo, abadilishe maneno 'اِبْنِىْ فُلَان' au 'بِنْتِى فُلَان' badala ya 'فُلَان اِبْنِ فُلَان' au

'فُلَانَہ بِنْتِ فُلَان'. Mvulana anafaa ahusishwe na baba yake na msichana anafaa ahusishwe na mama yake. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 20, uk. 585, muhtasari)*

24. Ikiwa hukumbuki dua hiyo, weka fikra tu moyoni mwako bila kusoma dua kwamba ni aqeeqah ya mvulana fulani na fulani au msichana fulani. Baada ya hayo, soma 'بِسْمِ اللّٰهِ اَللّٰهُ اَكْبَرْ' kisha mchinje mnyama. Aqiiqah itazingatiwa kuwa imetekelezwa. Sio lazima kusoma dua kwa ajili ya aqeeqah. *(Jannati Zaywar, uk. 323)*

25. Siku hizi, jamaa kwa kawaida hualikwa kwenye sherehe ya 'aqeeqah na huhudumiwa kwa karamu, ambalo ni tendo zuri. Wageni pia huleta zawadi kwa ajili ya mtoto, ambayo pia ni sawa. Hata hivyo, kuna baadhi ya maelezo katika suala hili. Ikiwa mgeni hataleta zawadi yoyote, mwenyeji au wanafamilia wake, wakati mwingine, hufanya dhambi ya kumsema vibaya mgeni. Ikiwa mgeni ana hakika au ana dhana yenye nguvu kwamba atakabili hali hiyo ikiwa atahudhuria sherehe hiyo, hapaswi kuhudhuria isipokuwa ahisi kwamba amelazimishwa. Anapaswa kuhudhuria sherehe pale tu inapohitajika na pia anapaswa kuleta zawadi. Hata hivyo, ikiwa mwenyeji anapokea zawadi kwa nia ya kwamba kama mgeni asingemletea zawadi, angemsema vibaya, au kama mwenyeji hana nia yoyote hiyo, lakini ana tabia mbaya ya kuzungumza mbaya kwa mgeni katika hali hiyo, atakuwa ni mwenye dhambi na anayestahili Moto wa Jahannamu, na zawadi itakuwa aina ya rushwa kwake, kwa sababu mwenyeji ana dhana kubwa kwamba mgeni amemletea zawadi ili kukaa salama kutokana na kuchukuliwa hatua mbaya kutoka kwake. Hata hivyo, ikiwa mwenyeji hana nia ya kumsema vibaya mgeni, na wala hana mazoea ya kufanya jambo kama hilo, hakuna ubaya kupokea zawadi hiyo.

## Sunnah na Adabu 18 za Kuweka Jina

1. Kauli mbili za Mtume Mustafa صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

    i. Weka jina la [mtoto] kufuatia watu wema. *(Al-Firdaus, juzuu ya 2, uk. 58, Hadithi ya 2329)*

    ii. Siku ya Hukumu, mtaitwa kwa majina yenu na majina ya baba zenu. Kwa hivyo, peaneni majina mazuri. *(Abu Dawood, juzuu ya 4, uk. 374, Hadithi ya 4948)*

2. Mufti Muhammad Amjad Ali A'zami رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Mtoto apewe jina zuri. Katika bara, watu wengi wana majina kama haya ambayo hayana maana au yana maana mbaya. Kwa hivyo, jiepushe na majina kama haya. Ni bora kumtaja mtoto kwa jina la manabii waliobarikiwa عَلَيْهِمُ السَّلَام, maswahaba waliobarikiwa, tabi'iyn na watangulizi wema رَحِمَهُمُ اللّٰه. Inatarajiwa kwamba mtoto atapata baraka kutoka kwao. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 653)*

3. Ikiwa mtoto amezaliwa akiwa hai au amezaliwa mfu, mwili wake umeumbwa kabisa au la, apewe jina; atafufuliwa Siku ya Hukumu. *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 3, uk. 153,154 | Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 841)* Imedhihirika kuwa kijusi kilichotoka kutoka kwa mimba iliyoharibika pia kinapaswa kutajwa. Katika ukurasa wa 17 wa 'Haki za Watoto', kijitabu cha Maktaba-tul-Madinah, imeelezwa: Taja hata kijusi kilichotoka kwenye mimba iliyoharibika, vinginevyo, atalalamika katika mahakama ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: "Taja kijusi kilichotoka kwa kuharibika kwa mimba, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu ataifanya mizani yako (yaani mizani ya matendo) kuwa nzito kupitia kwake." *(Al-Firdaus, juzuu ya 2, uk. 308, Hadithi ya 3392)*

4. Kauli tatu za Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَالِهٖ وَسَلَّم kuhusu kumpa mtoto wa kiume jina la 'Muhammad':

   i. Yule ambaye amebarikiwa kuzaliwa mtoto wa kiume na akamwita 'Muhammad' kutokana na mapenzi yangu na kwa kupata baraka ya jina langu,wote ( mtoto wake na yeye) wataenda Peponi. *(Jam'-ul-Jawami, juzuu ya 7, uk. 295, Hadithi ya 23255)*

   ii. Siku ya Hukumu, watu wawili watasimamishwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Itaamrishwa: 'Wapeleke Peponi.' Watasema kwa unyenyekevu: "Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Kwa tendo gani tunapelekwa Peponi? Hatukufanya kitendo chochote kinachotupeleka Peponi!" Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema: "Nendeni Peponi; Nimeweka kiapo kwamba mtu ambaye jina lake ni Ahmed au Muhammad hataingia Motoni. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 24, uk. 687, Al-Firdaus, juzuu ya 5, uk. 535, Hadithi ya 9006)*

   iii. Ana hasara gani yeyote miongoni mwenu ikiwa ana Muhammad mmoja au wawili au watatu nyumbani kwake! *(Al-Tabqat-ul-Kubra, juzuu ya 5, uk. 40)*

Mukhtasari A'la Hazrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه aliyoiandika baada ya kusimulia Hadithi hii iliyobarikiwa ni kama ifuatavyo: Kwa hiyo, niliwaita wanangu na wapwa wangu wote 'Muhammad' katika mnasaba wa aqeeqah yao. Kisha, kwa kuheshimu jina lililobarikiwa na kwa utambulisho wa watoto wangu, niliwapa majina tofauti ya kwanza. بِحَمْدِ لِلّٰهِ 'Muhammad' watano bado wako hai; ambapo, zaidi ya watano wamefariki. *(Fatawa Razawiyyah, juz. 24, uk. 689, muhtasari)* Sayyiduna Imam Abu Hamid Muhammad Bin Muhammad Bin Muhammad Ghazali, baba

yake na babu yake wana jina moja (Muhammad), hivyo basi akaitwa, Muhammad bin Muhammad bin Muhammad. Sayyiduna Aayman Abu Al-Barakat Bin Muhammad رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه ndiye mtu mkubwa ambaye katika ukoo wake, baba yake na wahenga hadi watangulizi kumi na wanne waliomtangulia wanaitwa 'Muhammad'. *(Al-Durr-ul-Kaminah, juzuu ya 1, uk. 431)*

5. **Baraka ya mtu aitwaye Muhammad:** Imepokewa kuwa, ikiwa watu waliokusanyika kwa ajili ya kushauriana juu ya jambo fulani akiwemo mtu anayeitwa Muhammad, lakini watu hao hawachukui ushauri wowote kutoka kwake [Mtu ambaye jina lake ni Muhammad] hawatafanikiwa kufikia lengo lao. *(Hashiyah Ala Al-Jami' Al-Sagheer, juzuu ya 1, uk. 149)*

6. **Dua kwa ajili ya mtoto wa kiume:** Mtangulizi wa Tabii, Imaam Atta رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه, amesema: Anayetaka mtoto wa kiume kutoka kwa mke wake mwenye mimba, aweke mkono wake juu ya tumbo la mke wake [mjamzito] na aseme: " Ikiwa ni mvulana, nimempa jina la 'Muhammad." اِنۡ شَـآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Atazaliwa mtoto wa kiume. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 24, uk. 690, imerekebishwa kidogo)*

7. Siku hizi, مَعَاذَاللّٰه Majina yanaharibiwa kwa kawaida, na inauma sana kupotosha jina la 'Muhammad'. Kwa hivyo, mpe jina kila mtoto wa kiume Muhammad au Ahmed, lakini kwa kuwaita, wape majina ya watangulizi wema. Matamshi ya majina yanapaswa kuwa rahisi.

8. Usimtajie [mtoto wako] kwa jina la Jibra'iil au Mika'iil, n.k Mtume صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Msimwite [mtoto] kwa jina la Malaika. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 6, uk. 394, Hadithi ya 8636)*

9. Ni haraam kumtaja [mtoto] Muhammad Nabi, Ahmed Nabi au Nabii Ahmed. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 24, uk. 677, muhtasari)*

10. Wakati wowote unapochagua jina, muulize mwanachuoni yeyote wa Kiislamu wa Kisunni kuhusu maana yake. Usichague jina ambalo lina maana mbaya. Kwa mfano, Ghafoor-ud-din maana yake ni muondoaji wa dini; ni ubaya sana kuchagua jina hili. Majina mabaya yana athari mbaya. A'la Hazrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: "Nimejionea jinsi majina mabaya yana athari mbaya sana. Pia nimegundua Sunni mcha Mungu ambaye anaficha imani yake na anajitahidi kueneza imani potovu katika mwishoni mwa maisha yake. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 24, uk. 681,682, muhtasari)*

11. Madhara ya jina yanaweza kuwa kwa kizazi kijacho pia. (Ukurasa wa 601, juzuu ya 3 ya Bahar-e-Shari'at, Hadithi # 21). Imesimuliwa na Saeed bin Musayyab رَضِىَ اللّٰه عَنْهُ katika Sahih Bukhari: Babu yangu alikwenda katika mahakama ya Nabii mpendwa. Yeye (صَلَّى اللّٰه عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) akauliza, 'Jina lako ni nani?' Babu yangu akajibu, 'Huzn.' Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰه عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema, 'Wewe ni Sahl.' yaani jipe jina la Sahl, ambalo maana yake ni laini, na Huzn ina maana ya ngumu. Babu yangu akasema, 'Sitabadilisha jina ambalo baba yangu amenipa.' Said Bin Musayyab رَضِىَ اللّٰه عَنْهُ akasema, 'Kwa sababu hiyo, bado tuna ugumu.' *(Bukhari, juz. 4, uk. 153, Hadithi ya 6193)*

12. Ni marufuku (imekatazwa) kumpa jina [mtoto] Yaseen au Taha. *(Fatawa Razawiyyah, juz. 24, uk. 680)* Usimpe jina [mtoto wako] hata Muhammad Yaseen. Hata hivyo, kama unataka, unaweza kumpa jina [mtoto wako] Ghulam Yaseen na Ghulam Taha.

13. Katika Sehemu ya 15 ya 'Bahar-e-Shari'at', imeelezwa katika 'Aqeeqay ka Bayan': Abdullah na Abdul Rahman ni majina mazuri sana, lakini katika zama hizi, imeonekana mara nyingi kwamba badala ya kuwaita mtu ambaye jina lake ni Abdul Rahman kwa jina lake Abdul Rahman, watu wengi humwita Rehman, na ni haraam kumwita mtu yeyote 'Rehman' asiyekuwa Mwenyezi Mungu. Vile vile watu huwaita Abdul Khaliq 'Khaliq' na Abdul Ma'bood 'Ma'bood'. Mabadiliko kama haya yasiyoruhusiwa hayapaswi kufanywa hata kidogo katika aina kama hizo za majina. Kadhalika, kuna mtindo wa kufupisha majina, yaani watu kuharibu majina kwa njia ya matusi. Majina kama haya hayapaswi kufupishwa hata kidogo. Kwa hiyo wakati kuna uwezekano kwamba majina yatafupishwa, majina hayo hayapaswi kuchaguliwa, bali majina mengine yanapaswa kuchaguliwa. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 356)*

14. Majina mabaya yabadilishwe na kuwekwa majina mazuri kwa sababu Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم angebadilisha jina baya [ kwa jina zuri]. *(Tirmizi, juz. 4, uk. 382, Hadith 2848)* Kulikuwa na mwanamke ambaye jina lake lilikuwa Asia [mwenye dhambi]; Mtume Mpenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alibadilisha jina lake na kuweka Jameelah. *(Muslim, uk. 1181, Hadithi ya 2139)*

15. Majina hayo ni haramu ambayo kwayo mtu anaweza kujisifia. Katika Aya ya 32 ya Surah Najm, sehemu ya 27, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: 'فَلَا تُزَكُّوْۤا اَنْفُسَكُمْ' *'Basi, msijifanye kuwa ni watakasifu.'* Kwa kunakili kitabu *'fuzool e Imadi'* A'ala Hadhrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: "Mtu yeyote asichague jina kama hilo linalodhihirisha kujisifu. *(Fatawa Razawiyyah, juz. 24, uk. 684)* Imeelezwa katika Muslim Sharif: Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alibadilisha jina la mwanamke aliyeitwa 'Barrah' [ yaani mwanamke mwadilifu] kwa kumpa jina 'Zaynab' na akasema,

‘Usijisifu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anajua vyema ni nani miongoni mwenu aliye mwadilifu.’ *(Muslim, uk. 1182, Hadithi ya 2142).*

16. Haijuzu kuchagua majina hayo ambayo ni mahususi kwa wasiokuwa Waislamu. Kutoka ukurasa wa 663 hadi 664 wa Fatawa-e-Razawiyyah, juz. 24, imeelezwa: Kuna aina za majina ambayo ni makhsusi kwa makafiri, kama vile Jirjis, Putrus, Yuhanna n.k., Kwa hiyo, hairuhusiwi kwa Waislamu kuchagua aina hizo za majina [kwa ajili ya watoto wao], kwa sababu ina mfanano na makafiri. واللہ تَعالیٰ اعلم

17. Inajuzu kumwita [mtoto] Ghulam Muhammad na Ahmed Jaan, lakini ni vyema kutoongeza Ghulam au Jaan, n.k. ili mtu aweze kupata fadhila za majina 'Muhammad' na 'Ahmed' yaliyotajwa katika Ahadith zilizobarikiwa. .

18. Inaruhusiwa kuchagua majina kama Ghulam Rasool, Ghulam Siddique, Ghulam Ali, Ghulam Hussain, Ghulam Ghaus na Ghulam Raza.

## Sunna na Adabu 35 za Kusafiri

1. Msafiri, kwa mujibu wa Shariah, ni mtu ambaye, kwa nia ya kusafiri umbali wa siku tatu anatoka nje ya makazi yake, kama vile mji au kijiji chake. Kusafiri kwa nchi kavu kwa siku tatu kunamaanisha umbali wa maili hamsini na saba na nusu (yaani takriban kilomita 92). *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 8, uk. 243-270, muhtasari)*

2. Kwa yule anayefanya safari ya Shar’i, ni lazima awe amejifunza hukumu zinazohitajika wakati wa safari. (Inafaa kusoma ‘Swala ya Msafiri’ iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah.)

3. Imepokewa katika Bukhari Sharif: Kwa ajili ya Vita vya Tabuk, kipenzi chetu, Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alitoka siku ya Alkhamisi,

naye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم angependelea kusafiri siku ya Alhamisi. *(Bukhari, juzuu ya 2, uk. 296, Hadithi ya 2950)*

4. Unapolazimika kusafiri, ni bora kusafiri siku ya Jumatatu, Alhamisi au Jumamosi. *(Fatawa Razawiyyah_referenced, vol. 23, p. 400, muhtasari)*

5. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akamhimiza Sayyiduna Jubair Bin Mut'im رَضِىَ اللهُ عَنْهُ kusoma dua hii ili abakie kufaulu zaidi kuliko maswahaba zake safarini :

   i. Surah Al-Kafiroon

   ii. Sura Al-Nasr

   iii. Sura Al-Ikhlaas

   iv. Sura Al-Falaq

   v. Surah Al-Naas.

   Soma surah zote mara moja; soma 'بِسۡمِ اللهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡم' kabla ya kila surah na wakati mmoja baada ya surah zote (kwa njia hii, utasoma surah tano na utasoma 'بِسۡمِ الله' mara sita). Sayyiduna Jubair Bin Mut'im رَضِىَ اللهُ عَنْهُ amesema, 'Nilikuwa na hali sawa, lakini nilipokuwa nikisafiri, nilikuwa sijafanikiwa kuliko wenzangu. Nilianza kusoma surah zilizotajwa hapo juu kila niliposafiri Kwa sababu ya baraka zao, ningeendelea kuwa tajiri na tajiri mpaka nitakaporudi. *(Abu Ya'la, juzuu ya 6, uk. 265, Hadithi ya 7382, muhtasari)*

6. Wakati wa kuondoka, kutana na jamaa na marafiki zako wote na uwaombe msamaha kwa makosa yako. Baada ya hayo, inakuwa ni lazima kwao kukusamehe kutoka moyoni. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 1052)*

7. Baada ya kuvaa nguo za kusafiria, swali rakaa 4 ya swala ya nafl pamoja na Surah Al-Fatihah na Surah Al-Ikhlaas kisha uondoke. Kwa mujibu wa rakaa hizi, familia yako na mali yako vitakaa salama hadi utakaporudi. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 1052)*

8. Rakaa mbili pia zinaweza kuswaliwa. Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa, 'Hakuna mtu aliyeacha kitu bora zaidi na familia yake kuliko rakaa mbili alizoswali nyumbani wakati wa kufanya nia ya kusafiri.' *(Musannaf Ibn Abi Shaybah, juz. 1, ukurasa wa 529)*

9. Ikiwa kuna ndugu watatu au zaidi wa Kiislamu wanaosafiri, wafanye mmoja kuwa kiongozi wao kwani ni Sunnah. Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa: "Wakiwapo watu watatu safarini, mfanyeni mmoja wenu kuwa kiongozi." *(Abu Dawood, juzuu ya 3, uk. 51, Hadithi ya 2609)*

10. Kwa njia hii, shughuli zinasimamiwa ipasavyo. Mtu huyo anapaswa kufanywa kuwa kiongozi ambaye ni mwenye tabia njema, hekima na dini. Kiongozi anapaswa kupendelea kupumzika kwa wenzi wake kuliko kupumzika kwake. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 1051, 1052)*

11. Mtu anatakiwa kuweka kioo, kohl(wanja), kichana na miswaki katika safari kwani ni Sunnah. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 1051, 1052)*

12. Baba yake A'la Hazrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه, Mufti Naqi Ali Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه, ameandika: Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم angeweka

    i. mswaki

    ii. kohl (wanja)

    iii. kioo

    iv. kichana

v. makasi

vi. sindano na

vii. uzi. *(Anwar-e-Jamal-e-Mustafa, uk. 160)* Katika riwaya nyingine:

viii. Neno ‘mafuta’ pia limetajwa. *(Subu-lul-Huda, juzuu ya 7, uk. 347)*

13. Jifurahishe na dhikri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sababu malaika atabaki nawe; lakini ukijifurahisha kwa mashairi [mabaya] na mazungumzo machafu, Shetani atakuwa pamoja nawe. *(Fatawa Razawiyyah _ imerejelewa, juzuu ya 10, uk. 729)*

14. Ikiwa una khofu kwa adui yako au jambazi, soma Sura kamili la ‘لِاِیْلٰفِ’. Mtasalimika اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ kutokana na kila shida. Kitendo hiki kimethibitishwa kikamilifu. *(Al-Hisn-ul-Haseen, uk. 79-80)*

15. Ukiwa safarini au haupo, wakati wowote unapohisi huzuni au una shida yoyote, soma ‘حَسْبُنَا الله، وَنِعْمَ الْوَكِيْل’ na ‘لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللهِ’. اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ Utaondokana na shida.

16. Wakati wa safari, soma ‘اللهُ اَكْبَر’ unapopanda juu kwenye mteremko na usome سُبْحٰنَ اللّٰه unaposhuka.

17. Ikiwa mtu anaenda safarini, mpe mkono msafiri na umuombee dua: ‘اَسْتَوْدِعُ اللهَ دِيْنَكَ، وَاَمَانَتَكَ، وَخَوَاتِيْمَ عَمَلِكَ’ *(Al hisn ul haseen uk, 82)*

18. Kwa ajili ya yule ambaye si msafiri, msafiri anapaswa kuomba dua ifuatayo: ‘اَسْتَوْدِعُكَ اللهَ الَّذِىْ لَا يُضِيْعُ وَدَائِعَهٗ’ *(Ibn-e-Majah, 28, juz 28, Hadith)*

19. Soma yafuatayo unaposhuka [i.e. popote inapobidi kusimama njiani] hadi mwishoni mwa safari yenu: ‘اَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللهِ التَّامَّاتِ، مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ’ اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ. Mtasalimika na kila hasara. *(Al-Hisn-ul-Haseen, uk. 82)*

20. Dua inayofanywa na msafiri hukubaliwa; kwa hiyo, jiombee nafsi yako, wazazi wako, familia yako na Waislamu wengine.

21. Ikiwa mtu ataugua au kupoteza fahamu wakati wa safari, maswahaba zake wanaweza kutumia kutoka kwa mali yake bila ruhusa yoyote ili kumtimizia haja zake. *(Rad-ul-Muhtar, juzuu ya 9, uk. 334, 335 | Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 222)*

22. Ni wajibu kwa msafiri kufanya qasr katika swalah, yaani kuswali rakaa mbili badala ya rakaa nne, kwa sababu kwake rakaa mbili zitakuwa ni swala kamili. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 743 | 'Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 139)*

23. Hakuna qasr katika Maghrib na Witr Swalah.

24. Hakuna qasr katika swalah ya Sunnah, bali ni lazima swala zote za Sunnah zitekelezwe. Kuna ruhusa ya kuacha swala ya Sunnah katika hali ya khofu na wasiwasi, lakini zitatekelezwa katika hali ya amani. *('Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 139)*

25. Jaribu uwezavyo kusafiri kwa ndege au garimoshi au basi, n.k. wakati ambapo hakuna wakati wa salah katikati.

26. Wakati wa kulala wakati wa safari, usiwe mzembe kiasi kwamba مَعَاذَاللّٰه unakosa swala yako.

27. Usighafilike na swala hata wakati wa safari. Tawadha kwa mapema, hasa unaposafiri kwa ndege, treni na kwa basi linalofuata njia ndefu.

28. Ikiwa basi lako litaharibika njiani, kuwa na subira badala ya kuweka maisha yako ya baadaye hatarini kwa kumkosoa na kuzungumza matusi kwa dereva au mmiliki wa basi; badala yake, jishughulishe na dhikri na swala kwa ajili ya kupata Pepo.

Vile vile vitu vilivyotajwa vinaweza kufanywa ikiwa treni au ndege yako imechelewa.

29. Kwa kuzingatia haki za abiria wengine wanaosafiri kwa treni, basi, n.k., watendee kwa wema mkubwa. kabili matatizo wewe mwenyewe, lakini walete faraja wao.

30. Usifanye abiria wengine kuwa na maoni ya chini kukuhusu wewe kwa kuzungumza kwa sauti na kwa kucheka kwa sauti kubwa.

31. Ukiona mzee au Mwislamu mgonjwa kwenye basi n.k ambalo limejaa, sisitiza kumpa kiti chako kwa nia ya kupata malipo (thawabu).

32. Jaribu kadri uwezavyo kusafiri kwa basi au kochi n.k. ambayo haichezeshi filamu na muziki ndani yake.

33. Unaporudi kutoka kwa safari yako, lete zawadi kwa ajili ya familia yako. Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, "Mtu anaporudi kutoka safarini, alete zawadi kwa ajili ya familia yake, hata kama amebeba mawe kidogo." *(Ibn-Asaakir , juz.52 uk, 230)*

34. Iwapo si wakati wa makruh unaporudi kutoka katika safari ya Shar'i, sali rakaa mbili za nafl, kwanza kabisa katika msikiti wako na kisha nyumbani baada ya kufika nyumbani.

35. Maombi yanayofanywa na msafiri hukubaliwa. *(Tirmizi, juzuu ya 5, uk. 280, Hadithi ya 3459)*

## Sunnah na adabu 33 za kumtembelea [mtu mgonjwa]

Kauli nane za Mtume Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

1. 'عُوْدُوا الْمَرِيْضَ' Mtembelee mgonjwa. *(Al-Adab Al-Mufrid, uk. 137, Hadithi*

*ya 518)*

2. Mwenye kumzuru mgonjwa, Mwenyezi Mungu Mtukufu humpa kivuli cha Malaika 75,000, na kwa kila hatua anayopiga, Mwenyezi Mungu Mtukufu humwandikia fadhila (jema) moja, na kwa kila hatua anayoichukua, Mwenyezi Mungu Mtukufu huondoa dhambi yake moja na huinua daraja yake moja mpaka atakapoketi mahali pake. Anapokaa, rehema humfunika na itaendelea kumfunika mpaka atakaporudi nyumbani kwake. *(Mu'jam-ul-Awsat, juzuu ya 3, uk. 222, Hadithi ya 4396)*

3. Mwenye kumtembelea mgonjwa, mwitaji anaita kutoka mbinguni: 'Habari njema ni kwa ajili yenu; kutembea kwako ni kuzuri, na umejitengenezea mahali peponi.' *( Ibn-e-Majah, juz. 2, uk. 192, Hadith 1443).*

4. Iwapo Muislamu atamzuru Mwislamu mgonjwa asubuhi, Malaika 70,000 wanamuombea msamaha mpaka jioni, na akizuru jioni, Malaika 70,000 wanamuombea msamaha hadi asubuhi, na kwa ajili yake kutakuwa na bustani katika Pepo. *(Tirmizi, juzuu ya 2, uk. 290, Hadithi ya 971)*

5. Mwenye kutawadha vizuri kisha akamzuru ndugu yake Mwislamu (mgonjwa) kwa nia ya kupata malipo atahamishwa mbali na Jahannam [sawa na] umbali wa miaka 70. *(Abu Dawood, juzuu ya 3, uk. 248, Hadithi ya 3097)*

6. Unapomtembelea mgonjwa, muombe akuombee dua, kwani dua yake ni kama dua ya Malaika. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 2, uk. 191, Hadithi ya 1441)*

7. Dua inayoombwa na mgonjwa haikatazwi mpaka apone. *(Attargheeb Wattarheeb, juzuu ya 4, uk. 166, Hadithi ya 19)*

8. Muislamu anapomtembelea Mwislamu mgonjwa, anatakiwa asome dua ifuatayo mara 7: ‘اَسْأَلُ اللهَ الْعَظِيْمَ، رَبَّ الْعَرْشِ الْكَرِيْمِ اَنْ يَّشْفِيَكَ’, ikiwa wakati wake wa kufa haujafika, atapata nafuu. *(Abu Dawood, juzuu ya 3, uk. 251, Hadithi ya 3106)*

9. Maana ya kumtembelea mgonjwa: maana halisi ni kuulizia afya ya mgonjwa kwa kwenda kwake. *(Urdu Lughat, juzuu ya 13, uk. 604)*

10. Kumtembelea mgonjwa ni Sunnah. Ikiwa unahisi kuwa ziara yako itakuwa ngumu kwa mgonjwa, usimtembelee. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 3, uk. 505)*

11. Hata ikiwa una uhusiano mbaya na mgonjwa au humpendi, bado unapaswa kumtembelea.

12. Mtembelee mgonjwa kwa nia ya kufuata Sunnah pekee. Ukimtembelea mgonjwa kwa sababu ya kwamba atakutembelea pia unapougua, hutapata thawabu.

13. Ukimtembelea mgonjwa na kugundua ugonjwa wake ni mkali, usizungumze naye kwa njia ambayo itamfanya ahisi hofu, kwa mfano, 'Uko katika hali mbaya sana!' Wala hupaswi kutikisa kichwa chako kwa njia inayoonyesha kuwa yuko katika hali mbaya.

14. Wakati wa kutembelea, onyesha dhiki na huzuni kutoka kwa sura yako ya uso kulingana na hali mbele ya mgonjwa au mtu aliyehuzunishwa.

15. Usizungumze kamwe kwa namna ambayo mgonjwa au mtumishi wake ana minong’ono ya kishetani kwamba umefurahishwa na tatizo lake.

16. Onyesha huruma yako kwa wanafamilia wa mgonjwa pia na uwape usaidizi au ushirikiano wote unaowezekana.

17. Mtembelee mgonjwa na uulize kuhusu hali yake na umuombee apone na apate usalama.

18. Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa na tabia iliyobarikiwa. Kila alipokuwa صَلَّى اللهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akimtembelea mgonjwa, Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikuwa akimsomea 'لَابَأْسَ طَهُوْرٌ اِنْ شَآءَ اللهُ' *(Bukhari, juzuu ya 2, uk. 505, Hadithi ya 3616)*

19. Muombe mgonjwa akuombee dua, kwani maombi ya mgonjwa haikatazwi.

20. Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Njia sahihi ya kumuuliza mtu mgonjwa hali yake ni kuweka mkono wako juu ya paji la uso wake na umuulize hali yake.' *(Tirmizi, juz. 3, uk. Hadithi ya 2740)*

21. Kuhusu Hadiyth hii yenye baraka, Mufti Ahmad Yar Khan رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه amesema: "Mtu yeyote anapomtembelea mgonjwa, aweke mkono wake juu ya paji la uso la mgonjwa na aseme: "Unasikiaje?" Hili humfariji mgonjwa, lakini aepuke kuweka mkono wake kwa muda mrefu. Kitendo hiki cha kuweka mkono ni njia ya kuonyesha upendo. *(Mirat, gombo la 6, uk. 358, iliyorekebishwa)*

22. Ikiwa mgonjwa anahisi usumbufu unapoweka mkono wako kwenye paji la uso wake, usiweke mkono wako. Ikiwa mgonjwa ni mvulana mwenye mvuto asiye na ndevu (hata kama si hivyo) na wewe مَعَاذَاللّٰه unahisi matamanio unapoweka mkono wako, kitendo chako cha kuweka mkono ni dhambi. Ukihisi matamanio kwa kumwangalia, kitendo chako cha kumtazama pia ni haramu.

23. Mazungumzo ya heshima na ya kupendeza yanapaswa kufanywa mbele ya mgonjwa ili aweze kufurahishwa. Taja

fadhila za maradhi na uzungumzie rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ili aweze kuzingatia malipo ya Akhera na kuepuka kulalamika.

24. Unapomtembelea mgonjwa, mpe wito wa wema (da'wah njema) kulingana na hali. Hasa, mshawishi kutekeleza swalah mara kwa mara, kwa sababu katika kipindi cha ugonjwa, hata watu wengi wanaoswali nao hughafilika na swalah.
25. Mhamasishe mgonjwa kutazama Idhaa ya Madani na umwambie kuhusu baraka zake.
26. Mhamasishe mgonjwa asafiri na qafilah ya Madani. Ikiwa hawezi kusafiri, basi mhimize amfanye yeyote katika familia yake asafiri kwa niaba yake na qafilah ya Madani. Mwambie kuhusu baraka za Madani qafilah ambamo wagonjwa waliponywa kimiujiza kwa sababu ya baraka za maombi yaliyofanywa wakati wa qafilah ya Madani.
27. Usikae muda mrefu na mgonjwa, na pia usipige kelele. Hata hivyo, ikiwa mgonjwa anataka utumie wakati mwingi zaidi pamoja naye, unaweza kufanya hivyo ikiwezekana, ukiheshimu matakwa yake.
28. Baadhi ya watu wana tabia ya kumwandikia baadhi ya dawa mgonjwa au mhudumu wake wanapokutana nao. Wengine wanasisitiza hata mgonjwa apate matibabu aliyoandikiwa, yaani, kunywa dawa fulani na utapona! Mgonjwa hatakiwi kupokea matibabu aliyoagizwa na mtu yeyote wa kawaida. Msemo unasema, 'Ujuzi mdogo ni hatari'. Mgonjwa anapaswa kushauriana na daktari wake kabla ya kutumia dawa iliyoandikwa na mtu. Kumbuka! Wale ambao sio madaktari lakini wanaagiza dawa ni watenda dhambi. A'la Hazrat

رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: "Ni Haramu kwa asiyekuwa daktari (نااہل) kuandikia watu dawa, na ni wajibu kwake kuacha kuandikia watu dawa. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 24, uk. 206)*

29. Kuchukua matunda au biskuti n.k kama zawadi kwa mgonjwa unapomtembelea ni tendo jema. Hata hivyo, kuepuka ziara hiyo kwa sababu ya kukosa la kumpelekea na kufikiria kwamba 'Ukimtembelea mgonjwa mikono mitupu, ataona vibaya' si vizuri. Mtu anapaswa kumtembelea mgonjwa hata kama hana chochote cha kumpelekea; kuepuka kumtembelea mgonjwa kwa sababu hii humnyima mtu malipo.

30. Wakati wa kutembelea mgonjwa, baadhi ya watu huchukua shada la maua, ambayo pia inaruhusiwa, lakini imeonekana kuwa kwa kawaida haina manufaa kwa yule ambaye amepewa. Kwa hivyo, jambo ambalo ni la manufaa linapaswa kutolewa kama zawadi. Inapendekezwa kwamba badala ya shada la maua au pamoja na shada la maua, popote inapofaa, pia mpe vijitabu (vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah) kwa mgonjwa, ili awape wageni wake, (na kama amelazwa hospitalini,) wagonjwa wake wa jirani na jamaa zao. Itakuwa vyema kiasi gani ikiwa mgonjwa mwenyewe atamtuma mtu fulani kununua vijitabu fulani na kupata thawabu kwa kuviweka kwa ajili ya makusudio hayo! Vijitabu vinapaswa kuchaguliwa kwa uangalifu mkubwa.

31. Kumzuru fasiki (فاسق) pia inajuzu kwa sababu ni haki ya Kiislamu ya kila Muislamu, na fasiki pia ni Muislamu. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 3, uk. 505)*

32. Haijuzu kumtembelea murtadi mgonjwa na mkafiri wa kiharbi. (Wakati huu, makafiri wote ni wa kiharbi duniani.)

33. Ni marufuku kumzuru mtu mzushi ambaye matendo yake ya uzushi bado hayajafikia ukafiri.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunnah na Adabu 16 zinazohusiana na sanda

Kauli sita ya Bwana Mtume Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

1. Mwenye kupanga sanda kwa ajili ya marehemu, kwa ajili yake kuna fadhila (jema) moja kwa kila unywele wa marehemu. *(Tareekh-e-Baghdad, juz. 4, uk. 263)* Kuhusiana na sehemu hii, 'Mwenye kupanga sanda kwa ajili ya marehemu', Allamah Abdul Rauf Munaawi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: yaani Mwenye kumuandalia maiti sanda kutoka mfukoni mwake (kwa kutumia pesa zake binafsi). *(Al-Tayseer, juzuu ya 2, uk. 442)*

2. Mwenye kupanga sanda kwa ajili ya marehemu, Mwenyezi Mungu Mtukufu atamfanya avae nguo nyepesi na ya hariri kwa wingi peponi. *(Al-Mustadrak, juzuu ya 1, uk. 690, Hadithi ya 1380)*

3. Mwenye kuogesha, kuvisha sanda, kumpaka maiti manukato, akabeba jeneza lake, akaswali Swalah yake na akaficha chochote kibaya kinachohusiana naye, atafutiwa madhambi yake kama alivyokuwa siku alipozaliwa na mama yake. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 2, uk. 201, Hadithi ya 1462)* Sehemu ya Hadithi 'chochote kibaya' maana yake ni kitu ambacho hakipaswi kufichuliwa, kama vile rangi ya uso wake kugeuka kuwa nyeusi.

4. Watayirishie maiti zenu sanda nzuri, kwa sababu wanakutana wao kwa wao kwenye makaburi yao na wanahisi furaha kutokana na sanda [zao] nzuri. *(Al-Firdaus, juzuu ya 1, uk. 98, Hadithi ya 317)*

5. Mtu miongoni mwenu akimpangia ndugu yake sanda, basi amtayarishie sanda nzuri. *(Muslim, uk. 470, Hadithi ya 943)*

6. Tayarisha sanda nyeupe kwa ajili ya marehemu wako. *(Tirmizi, juzuu ya 2, uk. 301, Hadithi ya 996)*

## Nia ya kumvisha Sanda [marehemu]

7. Nia ya kumvisha sanda marehemu:

   Kwa ajili ya kumridhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa ajili ya kufanya kitendo hiki cha lazima, nitamvisha sanda marehemu kwa mujibu wa Sunnah na kwa kufikiria sanda ambayo nitavishwa baada ya kufa kwangu.

8. Ni 'fard kifayah' kutayarisha sanda kwa ajili ya marehemu *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 817)*, yaani kama mtu yeyote atapanga sanda kwa ajili ya marehemu, watu wote watasamehewa kwa kutofanya kitendo cha lazima. Vinginevyo, wale wote waliopokea habari hiyo, lakini hawakupanga sanda kwa ajili ya marehemu watakuwa wenye dhambi.

## Sanda yenye kufuata mtindo wa Sunnah

9. Sanda ya wanaume: lifafah, yaani shuka, izaar, yaani vazi la chini, qamees, yaani vazi la juu. Kwa wanawake, zaidi ya haya matatu, kuna mbili zaidi zifuatazo: aurhni [kifuniko cha uso] na seenah-band [kifuniko cha kifua]. *(Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 160)*

10. Kijana yule ambaye bado hajabaleghe lakini amefikia umri wa matamanio ya kimwili anaangukia katika kundi la watu wazima. Kwa sanda yake, nguo ambazo zinapangwa kwa ajili ya watu wazima zinapaswa kupangwa. Nguo moja (izaar) inaweza kupangwa kwa ajili ya mvulana mdogo kuliko umri

huu (wa kufika matamanio), lakini vitambaa viwili (lifafah na izaar) vinapaswa kupangwa kwa ajili ya msichana mdogo kuliko umri huu. Ni vizuri ikiwa vitambaa viwili (lifafah na izaar) pia vimepangwa kwa ajili ya mvulana, na ni bora kupanga sanda kamili kwa wote wawili, hata kama mtoto ameishi siku moja tu. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 819)*

11. Wanazuoni wa Kiislamu pekee na viongozi wa kiroho wanaweza kuzikwa pamoja na imamah (kilemba). Imepigwa marufuku kuzika miili ya watu wa kawaida pamoja na imamah. *(Madani Wasiyyat Naamah, uk. 4)*

12. Hairuhusiwi kuweka harufu ambamo zafarani imechanganyiwa kwenye mwili wa mwanamume , lakini inajuzu kuweka harufu hiyo kwenye mwili wa mwanamke. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 821)*

13. Iwapo mtu aliyevaa ihram [na akafa katika hali hiyo hiyo], pawekwe manukato kwenye mwili wake, na uso wake na kichwa chake pia kifunikwe kwa sanda. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 821)*

## Maelezo ya Sanda

14. Lifafah (yaani bahasha):

    i. Inapaswa kuwa kubwa kuliko urefu wa marehemu ili iweze kufungwa kutoka pande zote mbili.

    ii. Izaar (yaani vazi la chini) liwe kuanzia juu ya kichwa hadi miguuni. Ni ndogo kuliko lifafah, kwa kutokuwa na sehemu ambayo ni ziada katika lifafah kwa ajili ya kuifunga.

iii. Qamees (yaani kafani 'vazi la juu') liwe kuanzia shingoni hadi chini ya magoti. Inapaswa kuwa sawa mbele na nyuma, na haipaswi kuwa na mikono na iliyokatwa. Kuna tofauti kati ya kafani ya mwanaume na mwanamke. Kata kafani ya mwanaume kuanzia mabegani na ya mwanamke kuelekea kifuani.

iv. Aurhni: Inapaswa kuwa na urefu wa yadi 1.5.

v. Seenah-band (yaani kifuniko cha kifua): hii inapaswa kuwa kutoka kwa kifua hadi kwenye kitovu, na ni bora ikiwa seenah-band iko ndefu hadi kwenye mapaja. *(Bahar-e-Shari'at, juz. 1, uk. 818, muhtasari)* Kwa kawaida, sanda iliyotengenezwa tayari hununuliwa. Si lazima mtu aione sawa na ukubwa unaoendana na Sunnah kulingana na urefu wa marehemu. Pia inawezekana kwamba sanda ni ndefu kiasi kwamba inaingia katika kundi la israaf [upotevu]. Kwa hivyo, tahadhari inaweza kutumika katika kukata sanda kutoka kwa safu ya kitambaa, kulingana na mahitaji. Ikiwa unapaswa kununua kitambaa kilichopangwa tayari, weka kitambaa na wewe baada ya kuikata. Ikiwa sanda inunuliwa kutoka kwa mali ya marehemu, kitambaa cha ziada kitagawanywa katika urithi.

15. Sanda iwe nzuri, yaani iwe sawa na bei ya nguo ambayo mwanamume alikuwa akiivaa kwa ajili ya Idi na Swala ya Ijumaa na mwanamke alikuwa akivaa kwa ajili ya kuenda nyumbani kwa wazazi wake. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 818)*

## Mbinu ya Kumfunika Marehemu

16. Baada ya kuogesha [marehemu], pangusa mwili wake kwa

upole kwa kitambaa chochote safi ili sanda isilowane. Washa vijiti vya 'joss' na uzipitishe karibu na sanda mara moja au mara tatu au mara tano au mara saba. Usizipitishe zaidi ya idadi hii ya nyakati. Sasa, weka kwanza chini lifafah, yaani bahasha kubwa ya kufungia, kisha weka tahband juu yake, na kisha weka kafani juu ya hii. Sasa mlaze marehemu kwenye kanga na umvishe kafani. Kisha weka harufu nzuri kwa ndevu (ikiwa marehemu hana ndevu, weka kwenye kidevu) na kwa mwili wote. Paka kafuri kwenye sehemu za mwili ambazo mtu anafanyia sajdah, yaani paji la uso, pua, mikono, magoti na miguu. Kisha kunja izaar, yaani vazi la chini, kwanza kutoka upande wa kushoto na kisha kutoka upande wa kulia. Kisha funga lifafah kwa njia ile ile, kwanza kutoka upande wa kushoto na kisha kutoka upande wa kulia ili sehemu ya kulia ibaki juu. Funga sanda kwa juu na chini ili isisogee. Mfanye mwanamke avae kafani; baada ya kumfanya avae kafani zigawe nywele zake sehemu mbili kisha ziweke kwenye kifua juu ya kafani. Weka aurhni chini ya sehemu ya juu ya nusu ya nyuma, na kuikunja juu ya kichwa, iweke kwenye uso kama pazia ili ibaki kwenye kifua. Inapaswa kuwa kutoka nusu ya nyuma ya marehemu hadi kifua kwa urefu na upana kama pengo kati ya masikio mawili. Kisha kunja izaar na lifafah kama kawaida. Kisha weka seenah-band juu yao kuanzia kifuani hadi mapajani na uifunge [kwa kamba]. (Kwa maelezo zaidi, soma kutoka ukurasa wa 817 hadi 822 wa Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1)

## Sunnah na Adabu 15 zinazohusu mazishi

Kauli nne ya kipenzi chetu Bwana Mtume صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم:

1. Mwenye kupokea habari za mauti yoyote, [kisha] akakutana na watu wa familia ya marehemu na kuwapa pole, Mwenyezi

Mungu Mtukufu humwandikia malipo ya qiirat moja. Basi akienda kwenye mazishi, Mwenyezi Mungu Mtukufu huandika malipo ya qiirat mbili; basi ikiwa ataswali swalah yake ya maiti, qiirat tatu, basi akihudhuria maziko,qiirat nne ; na kila qiirat ni sawa na Mlima Uhud. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 401, imetolewa | 'Umda-tul-Qaari, juzuu ya 1, uk. 400, chini ya Hadithi ya 47)*

2. Kuna haki sita za Muislamu kwa Muislamu. (Mojawapo ni kwamba) [Muislamu] anapokufa, Mwislamu mwingine ahudhurie mazishi yake. *(Muslim, uk. 1192, Hadithi ya 5 (2162), muhtasari)*

3. Anapokufa mtu ambaye ameandikiwa Pepo, Mwenyezi Mungu Mtukufu hawaadhibu watu wanaobeba jeneza lake, wanaotembea nyuma yake na wanaoswali swala yake ya maiti. *(Al-Firdaus, juzuu ya 1, uk. 282, Hadithi ya 1108)*

4. Malipo ya kwanza kabisa atakayopewa Muumini baada ya kifo chake ni kwamba watu wote walioswali swala yake ya maiti watasamehewa. *(Musnad-ul-Bazzaar, juzuu ya 11, uk. 86, Hadithi ya 4796)*

5. Sayyiduna Dawood عَلَيْهِ السَّلَام kwa unyenyekevu aliuliza katika mahakama ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, 'Ya Allah Mwenyezi! Ni malipo gani ya mwenye kuandamana na msafara wa mazishi kwa ajili ya kukuridhisha Wewe tu?' Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema: "Siku atakayo kufa Malaika watakwenda pamoja na msafara wa maziko yake, nami nitamsamehe." *(Sharh-us) -Sudoor, ukurasa wa 97)*

6. Mtu alimuona Sayyiduna Malik Bin Anas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا katika ndoto baada ya kufariki na akauliza, 'مَافَعَلَ اللهُ بِكَ؟' yaani 'Mwenyezi Mungu Mtukufu alikutendea vipi?' Alijibu,' Yeye عَزَّوَجَلَّ

amenisamehe kwa sababu ya kilma moja ambayo Sayyiduna Usman Ghani رَضِیَ اللهُ عَنْهُ angeisema baada ya kuona msafara wa mazishi. (Kilma hiyo ni:) "سُبۡحٰنَ الۡحَیِّ الَّذِیۡ لَایَمُوۡتُ". Kwa hiyo,mimi pia nilikuwa nikisema kilma hiyo baada ya kuona maandamano ya mazishi. Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ amenisamehe kwa sababu ya (kusema) kilma hii.' *( Ihya`-ul-'Uloom, juz. 5, uk. 266, muhtasari)*

7. Mtu anapaswa kuswali swala ya maiti kwa nia njema, k.m. kumridhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu, kutekeleza wajibu wa kuswali swala ya maiti, kutoa pole kwa familia ya marehemu na kujifunza somo.

8. Unapoenda na msafara wa mazishi, endelea kufikiria juu ya kifo chako mwenyewe na mwisho mzuri na mbaya. Endelea kufikiria hivi: Mimi pia nitachukuliwa siku moja kwa njia sawa na mtu huyu anachukuliwa leo; Pia nitazikwa kwa njia sawa na mtu huyu anakaribia kuzikwa chini ya tani za ardhi. Ni ibada na chanzo cha kupata thawabu kutafakari namna hii.

9. Kubeba jeneza la mazishi ni chanzo cha kupata thawabu. Rasuli kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alibeba jeneza la mazishi la Sayyiduna Sa'd Bin Mu'aaz رَضِیَ اللهُ عَنْهُ. *(Al-Tabqat-ul-Kubra juzuu ya 3, uk. 329 | Al-Binayah, juzuu ya 3, uk. 242, muhtasari)*

10. Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa, 'Madhambi arobaini makubwa yataondolewa kwa mwenye kubeba jeneza kwa hatua arubaini.' Zaidi ya hayo, imeelezwa katika Hadithi nyingine iliyobarikiwa, 'Allah Mtukufu atamsamehe kabisa yule anayebeba kwa mabega yake pembe zote nne za jeneza la maiti.' *( Jauharah, uk. 39 | Rad-ul-Muhtar, juzuu ya 3, uk. 158, 159 | Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 823)*

11. Mbinu ya Sunnah ni kubeba jeneza la maiti kutoka pembe zote nne, moja baada ya nyingine, na kutembea hatua kumi kila mara. Sunnah kamili ni kubeba kwanza upande wa kulia wa upande wa kichwa [wa marehemu], kisha upande wa kulia wa upande wa mguu, kisha upande wa kushoto wa upande wa kichwa na kisha upande wa kushoto wa upande wa mguu. Mtu anapotembea hatua kumi [akishikana kila upande], atachukua hatua arobaini kwa jumla. *(Aalamgeeri, juz. 1, uk. 162 | Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 822)* Baadhi ya watu wanaendelea kutangaza katika msafara wa mazishi, ' kila mmoja atembee hatua mbili.' Wanapaswa kutangaza, ' kila mmoja atembee hatua kumi.'

12. Wakati wa kubeba jeneza la maiti, hairuhusiwi, ni haramu na kitendo kinachopelekea Motoni kuwasukuma watu kimakusudi kwa namna ambayo inawaumiza, kama wanavyofanya baadhi ya watu katika msafara wa mazishi ya mtu fulani au katika msafara wa mazishi ambapo video n.k. yanafanywa.

13. Hakuna ubaya ikiwa mtu mmoja atabeba mwili wa mtoto aliyekufa mikononi mwake. Watu wanaweza kuichukua mikononi mwao mmoja baada ya mwingine. *('Aalamgeeri, juz. 1, uk. 162)* Hairuhusiwi na ni haramu kwa wanawake kwenda na msafara wa mazishi (iwe ni wa mtoto au mtu mzima). *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 823 | Radd-ul-Mukhtar, juzuu ya 3, uk. 162)*

14. Mume anaweza kubeba jeneza la mazishi la mke wake, kumshusha kaburini na hata kumuona usoni. Ni [vitendo] tu vya kuogesha na kugusa mwili moja kwa moja bila nguo yoyote kati yao ni haramu. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 812, 813)*

15. Inaruhusiwa kusoma Kalimah Twayyibah au Kalimah cha Shahadah au hamdi za Mwenyezi Mungu na qaswida za Bwana Mtume, n.k. katika utaratibu wa mazishi kwa sauti kubwa. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 139 - 158)*

*Janazah aagay aagay keh raha hay ay jahan walo!*
*Maray peechay chalay aa'o tumhara rehnuma mayn hun*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sunnah na adabu 22 zinazohusu makaburi na Mazishi

1. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

اَلَمْ نَجْعَلِ الْاَرْضَ كِفَاتًا ﴿۲۵﴾ اَحْيَآءً وَّ اَمْوَاتًا ﴿۲۶﴾

*Je! Hatukuifanya ardhi kuwa pahala pa kukusanyika? Kwa walio hai na waliokufa?*

*[Kanz-ul-Iman (tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 10, Surah Al-Mursalaat, Aya 25,26)*

Kuhusu aya hii iliyobarikiwa, imeelezwa kwenye ukurasa wa 927 wa 'Noor-ul-Irfan': "Kwa namna ambayo watu walio hai wanakusanywa juu ya ardhi na wafu ndani ya ardhi."

2. Ni fard kifayah kumzika marehemu [i.e. hata mtu mmoja akimzika, wote watasamehewa, la sivyo, waliopokea habari lakini hawakumzika watakuwa wenye dhambi]. Haijuzu kumlaza marehemu chini na kisha kumzingira (kwa kumjengea kuta) pande zote nne. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 842)*

3. Makaburi pia ni baraka ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambamo maiti huzikwa ili wanyama na vitu vingine visiwadhulumu.

4. Mzike marehemu karibu na watu wema kwani naye atapata baraka za ukaribu wao. مَعَاذَاللّٰه Hata akistahiki adhabu, wao [watu wema] watamwombea. Rehema inayowashukia [watu wema] pia itamzunguka [mtu mwenye dhambi]. Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mzikeni marehemu pamoja na watu wema.' *(Hiliya-tul-Awliya, juz. 6, uk. 390, Raqm 9042)*

5. Hakuna ubaya kumzika marehemu usiku. *(Jauharah, uk. 141)*

6. Haijuzu kuzika zaidi ya maiti mmoja bila ya dharura katika kaburi moja, lakini inaruhusiwa ikibidi. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 846 | Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 166)*

7. Ni mustahab kuweka jeneza kando ya kaburi kuelekea Qiblah ili marehemu ashushwe kaburini kutoka kwa upande wa Qiblah. Usiiweke jeneza katika sehemu ya mguu wa kaburi ili iletwe kutoka kwa upande wa kichwa. *(Bahar-e-Shari'at, juzuu ya 1, uk. 844)*

8. Watu wawili au watatu kama inavyotakiwa waingie kaburini; ni bora wakiwa na nguvu na ni wachamungu. Mwanamke aliyekufa anapaswa kuteremshwa kaburini na maharim [i.e. watu ambao nikah yake ilikuwa haramu [iliyoharamishwa] milele, kama kaka, mwana, baba, n.k.]. Ikiwa hawapo, jamaa wengine wamshushe kaburini, na ikiwa hawapo pia, watu wachamungu wanapaswa kuombwa kutekeleza kazi hii. *(Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 166)*

9. Weka mwili wa mwanamke ukiwa umefunikwa na kitambaa tangu wakati wa kumshusha kaburini hadi lahadi

zitakapowekwa.

10. Soma dua ifuatayo unapomteremsha marehemu kaburini: ‘بِسْمِ اللّٰهِ وَبِاللّٰهِ وَعَلٰى مِلَّةِ رَسُوْلِ اللّٰهِ’. *(Tanveer Al-Absaar, juzuu ya 3, uk. 166)*

11. Mlaze marehemu upande wake wa kulia kwa namna ambayo uso wake uwe unaelekea Qiblah. Fungua mafundo ya sanda kwani hayatakiwi sasa, na hakuna ubaya hata yasipofunguliwa. *(Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 166 | Jauharah, uk. 140)*

12. Mwenye kufungua mafundo ya sanda asome dua ifuatayo: ‘اَللّٰهُمَّ لَا تَحْرِمْنَا اَجْرَهٗ وَلَا تَفْتِنَّا بَعْدَهٗ’. *(Haashiya-tu-Tahtaawi, uk. 609)*

13. Funga kaburi kwa matofali ambayo hayajachomwa. Ikiwa ardhi ni laini, inaruhusiwa kuweka mbao. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 1, uk. 844)*

14. Sasa ardhi inapaswa kuongezwa juu. Ni mustahabu kurusha mchanga mara tatu kwa mikono miwili kutoka upande wa kichwa [wa marehemu]. Kwanza sema, ‘مِنْهَا خَلَقْنٰكُمْ’; mara ya pili, sema, ‘وَفِيْهَا نُعِيْدُكُمْ’; na mara ya tatu sema, ‘وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً اُخْرٰى’. Kisha tupa mchanga iliyobaki kwenye kaburi kwa kutumia jembe au kitu chochote kama hicho. *(Jauharah, uk. 141)*

15. Ni makruh kutupa mchanga zaidi kuliko ule uliotolewa kaburini. *(Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 166)*

16. Mchanga uliobaki kwenye mikono inaweza aidha kuondolewa au kuoshwa. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 1, uk. 845)*

17. Usifanye kaburi lenye pembe nne, bali lifanye kaburi kuwa kama nundu ya ngamia. Ni Sunnah kunyunyizia maji juu ya kaburi [baada ya kuzika]. Kaburi linapaswa kuwa la urefu wa mkono au zaidi kidogo. *(Bahar-e-Shari'at, juz. 1, uk. 846, kwa muhtasari Aalamgeeri, juzuu ya 1, uk. 166 | Rad-ul-Muhtar, juzuu ya 3, uk. 168)* Baada

ya mazishi, Adhini ilhali umesimama ukiwa umeelekeza uso wako Qiblah kwenye upande wa kichwa cha kaburi, kwani ina manufaa makubwa kwa maiti. *(Imetolewa kutoka, Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 5, uk. 370, imetolewa)*

18. Baada ya mazishi ni mustahabu kusoma rukuu ya kwanza ya Surah Al-Baqarah kuanzia ‘الٓمٓ’ hadi ‘مُفۡلِحُوۡن’ upande wa kichwa cha marehemu na rukuu ya mwisho kwa upande wa miguu, kutoka ‘اٰمَنَ الرَّسُوۡلُ’ mpaka mwisho wa Surah. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 1, uk. 846)*

19. Ni mustahabu kukaa karibu na kaburi baada ya maiti kuzikwa kwa muda unaotosha kuchinja ngamia na kugawanya nyama yake kwani marehemu atasikia raha na hatakuwa na woga kujibu maswali ya Nakirayn. Katika kipindi hiki, soma Qur'ani Tukufu, omba na umuombee msamaha marehemu, na umuombee marehemu awe thabiti katika kujibu maswali za Nakirayn. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 1, uk. 846, imerekebishwa)*

20. Inajuzu kuweka Shajarah au Ahd Naamah kaburini. Ni bora kutengeneza kijishimo kwenye ukuta kuelekea Qiblah mbele ya uso wa marehemu na kuweka Shajarah au Ahd Naamah humo. Kwa hakika, katika Durr-e-Mukhtar, imeelezwa kwamba kuandika Ahd Naamah juu ya sanda inaruhusiwa, na imeelezwa kwamba mtu anaweza kutumainia msamaha kwa kufanya hivyo. Inajuzu kuandika ‘بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ’ kwenye kifua na paji la uso la marehemu. Mtu mmoja aliweka wosia juu yake, hivyo ‘بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ’ ukaandikwa kwenye kifua na paji la uso wake baada ya kifo chake. Kisha mtu akamwona katika ndoto na akamuuliza kuhusu hali yake. Alisema: ‘Nilipowekwa kaburini, malaika wenye kuadhibu walinijia. Malaika walipoona “بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ” imeandikwa kwenye paji la uso

wangu, walisema, “Umesalimika kutoka kwa adhabu.”’ *( Bahar-e-Shari'at, juz. 1, uk. 848 | Durr-e- Mukhtar, juzuu ya 3, uk. 185, Tatar Khaniyyah, juzuu ya 2, uk. 170)*

21. Vile vile Inaweza kufanywa hivyo: andika ‘بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ’ kwenye paji la uso na Kalimah Twayyibah, ‘لَآ اِلٰہَ اِلَّا اللّٰہُ (صَلَّی اللّٰہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم) مُحَمَّدٌ رَّسُوۡلُ اللّٰہِ’ juu ya kifua, lakini baada ya kumuogesha marehemu na kabla ya kumfanya marehemu kuvaa sanda; andika kwa kidole cha shahada, bila kutumia wino. *(Bahar-e-Shari’at, juzuu ya 1, uk. 848, iliyorekebishwa | Rad-ul-Muhtar, juzuu ya 3, uk. 186)*

22. Ni wajibu kuzika mifupa ya marehemu inayotoka kaburini. *(Imetolewa kutoka, Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 406)*

## Sunna na Adabu 21 za

# Kutembelea Makaburi

Kauli tatu za Mustafa صَلَّی اللّٰہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم:

1. Niliwakataza kuzuru makaburi, lakini sasa mzuru makaburi kwani ndio sababu ya kutopendezwa na dunia na kumfanya [mtu] kukumbuka Akhera. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 2, uk. 252, Hadithi ya 1571)*

2. Mtu anapopita kwenye kaburi la namna hiyo ambalo mkaazi wake alikuwa anajulikana kwake duniani na akasema salamu, marehemu humtambua na kujibu salamu yake. *(Tareekh-e-Baghdad, juzuu ya 6, uk. 135, Hadithi ya 3175)*

3. Mwenye kuzuru makaburi ya wazazi wake wawili au mojawapo ya makaburi ya wazazi wake kila Ijumaa atasamehewa na ataandikwa kuwa ni mchamungu. *(Shu’ab-ul-Iman, juzuu ya 6, uk. 201, Hadithi ya 7901)*

4. Ni Sunnah kuzuru makaburi ya Waislamu. Ni fahari kubwa kuzuru madhabahu ya Awliya na mashahidi watukufu رَحِمَهُمُ اللّٰهُ, na kuwafikishia malipo ni kitendo kinachopendwa na husababisha mtu kupata thawabu. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 532, imetolewa)*

5. Ukitaka kuzuru [madhabahu ya mtu mtukufu au] kaburi la Mwislamu, kitendo cha mustahab ni kuswali rakaa 2 za nafl kwanza [katika wakati usio wa makruh] nyumbani kwako. Soma 'Ayat-ul-Kursi' mara moja na 'Surah Al-Ikhlaas' mara tatu baada ya 'Surah Fatihah' katika kila rakaa na kisha ufikishe malipo yake kwa mkaaji wa kaburi. Mwenyezi Mungu Mtukufu ataumba nuru katika kaburi la maiti huyo na atamlipa malipo makubwa yule [aliyefikisha malipo]. *('Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 350)*

6. Unapotembelea dhabahu lililobarikiwa au kaburi la muislamu, usijishughulishe na mazungumzo yasiyo na maana njiani. *('Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 350)*

7. Usibusu kaburi na wala usiliguse, bali simama kwa umbali kidogo nalo. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 522-526, imetolewa)*

8. Ni haramu kufanya sajdah ta'zeemi (kusujudu kwa heshima) kaburini, na ikifanywa kwa nia ya kufanya ibada, basi ni kufuru. *(Imetolewa kutoka: Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 22, uk. 423)*

9. Katika makaburi, tembea kwenye njia ya kawaida ambapo hapakuwa na makaburi ya Waislamu hapo awali. Ikiwa barabara ya kutembea imejengwa mpya, usitembee juu yake. Imeelezwa katika Fatawa-e-Shaami: 'Ni haramu kutembea kwenye njia iliyojengwa hivi karibuni ambayo imetengenezwa makaburini kwa kubomoa makaburi. Kwa hakika, kama mtu anadhania tu [ana shaka] kwamba njia hiyo ni mpya, hata

hivyo hairuhusiwi na ni dhambi kutembea juu yake.” *(Durr-e-Mukhtar, juz. 3, uk. 183).*

10. Imeonekana katika madhabahu mengi ya Awliya waliobarikiwa kwamba makaburi ya Waislamu yanabomolewa na sakafu inafanywa ili wageni waweze kutembelea. Kulala, kutembea, kusimama, kukaa katika dhikri na kisomo, n.k. vyote ni haramu Juu ya sakafu kama hiyo. Soma Fatihah kwa mbali.

11. Unapozuru kaburi, simama mahali uso wa marehemu ulipo. Kwa kuzingatia jambo hili, kuja kutoka upande wa miguu ya marehemu ili wewe uwe ndani ya maoni yake. Usitoke upande wa kichwa kwani marehemu atalazimika kukuangalia kwa kuinua kichwa chake. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 532, imetolewa)*

12. Simama makaburini kwa namna ambayo mgongo wako uelekee Qiblah na uso uko upande wa nyuso za wakaaji wa makaburi. Baada ya hayo soma ifuatayo: ‘اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَااَهْلَ الْقُبُوْرِ، يَغْفِرُاللّٰهُ لَنَاوَلَكُمْ لَنَا سَلَفٌ وَّنَحْنُ بِالْاَثَرِ’ Tafsiri : Amani iwe juu yenu! Mwenyezi Mungu Mtukufu atusamehe sisi na nyinyi! mmetutangulia, nasi tutakuja nyuma yenu. *(Imetolewa kutoka, Mirqat-ul-Mafatih, juzuu ya 4, uk. 253, chini ya Hadithi ya 1765)*

13. Kwa anaye soma dua ifuatayo baada ya kuingia makaburini, ‘اَللّٰهُمَّ رَبَّ الْاَجْسَادِ الْبَالِيَةِ وَالْعِظَامِ النَّخِرَةِ الَّتِيْ خَرَجَتْ مِنَ الدُّنْيَا وَهِيَ بِكَ مُؤْمِنَةٌ، اَدْخِلْ عَلَيْهَا رَوْحًا مِّنْ عِنْدِكَ، وَسَلَامًا مِّنِّيْ’ Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Ewe Mola Mlezi wa miili iliyooza na mifupa iliyooza! Warehemu walioiacha dunia katika hali ya imani na wafikishie salaam yangu’, Waumini wote waliofariki dunia kutoka kwa Sayyiduna Adam عَلَيْهِ السَّلَام mpaka siku hiyo watamuombea msamaha. *(Musannaf Ibn Abi Shaybah, juz. 8, uk. 257)*

14. Mtume Mpendwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَالِهٖ وَسَلَّم amesema: 'Mwenye kuingia makaburini kisha akasoma 'Surah Al-Fatihah', 'Surah Al-Ikhlaas' na 'Surah Al-Takasur' kisha akaomba ifuatavyo: Ewe Mwenyezi Mungu! Kila ambacho nimesoma kutoka kwa Qur'an, wafikishie ujira wake Waumini wanaume na Waumini wanawake wa makaburi haya", Waumini wote hao watakuwa waombezi wake [i.e. mwenye kufikisha ujira] Siku ya Kiyama.' *(Sharh-us-Sudoor, uk. 311)*

15. Imeelezwa katika Hadiyth iliyobarikiwa: "Mwenye kusoma 'Surah Al-Ikhlaas' [i.e. 'قُلْ هُوَاللهُ اَحَدٌ'] mara kumi na moja (Surah kamili) kisha akafikisha ujira wake kwa wafu atapata malipo sawa na idadi ya wafu." *(Durr-e-Mukhtar, juzuu ya 3, uk. 183)*

16. kijiti cha *joss* iliyowashwa haipaswi kuwekwa kwenye kaburi kwani ni dharau na ishara mbaya. Walakini, ikiwa unataka kufanya mazingira yenye harufu nzuri kwa wageni, weka kijiti cha *joss* karibu na kaburi kwenye nafasi tupu kwani kufanya mazingira kuwa na harufu nzuri kwa wengine ni tendo zuri. *(Imefupishwa kutoka: Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 482, 525, imetolewa)*

17. Katika sehemu nyingine, A'la Hazrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Imepokewa katika Sahih Muslim kutoka kwa Sayyiduna Amr Ibn 'Aas رَضِىَ اللهُ عَنْهُ. kuwa yeye alimwambia kijana wake katika wakati wake wa mwisho,'MImi nikifa, mwanamke yeyote atakayemlilia maiti asiende pamoja nami, wala moto usiende [pamoja nami]." *(Muslim, uk. 75, Hadithi ya 192)*

18. Usiweke taa ya mafuta, mshumaa uliowaka, nk kwenye kaburi. Hata hivyo, ikiwa nuru itahitajika kwa watu kutembea njiani au kusoma Qur'ani Tukufu katika [giza la] usiku, mshumaa au taa ya mafuta inaweza kuwekwa kando ya kaburi kwenye nafasi

tupu. Nafasi tupu isiwe mahali palipokuwa na kaburi ambalo sasa limebomolewa.

19. Siku nne zifuatazo ni bora kwa kutembelea makaburi: Jumatatu, Alhamisi, Ijumaa na Jumamosi. *(Aalamgeeri, juz. 5, uk. 350)* Kuzuru makaburi ni vyema baada ya swalah ya alFajiri siku ya Ijumaa. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 9, uk. 523, imetolewa)*

20. Inapendeza kuzuru makaburi katika mikesha yenye baraka, hasa Layla-tul-Bara'at (usiku wa tarehe 15 ya Shaabaan). *(Aalamgeeri, juz. 5, uk. 350)* Vile vile, ni vyema kuzuru makaburi wakati wa siku zenye baraka pia, kwa mfano, katika Eid zote mbili, tarehe 10 Muharram-ul-Haraam na katika siku kumi za mwanzo za Dhul-Hijjah. *(Aalamgeeri, juzuu ya 5, uk. 350)*

21. Wakati wa kutembelea makaburi, badala ya kuzungumza bila ya lazima na kufikiria juu ya mambo yasiyofaa, kumbuka kifo chako na mwaga machozi ikiwezekana. Kumbuka dhambi zako na uogope adhabu ya kaburi na utubu dhambi zako. Hebu fikiria kwamba leo watu hawa waliokufa wamelala katika makaburi yao peke yao; kwa njia hiyo hiyo, nami pia nitakuwa nimelala peke yangu katika kaburi la giza hivi karibuni.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Ombi kwa Wahubiri wa Kiume na Kike

Taja baadhi ya Sunnah na adabu kadiri inavyowezekana mwishoni mwa kila hotuba yenye msukumo wa Sunnah. Soma kifungu Na. 1 kabla ya kutaja Sunnah na adabu na kifungu Na. 2 baada ya kutaja Sunnah na adabu. (Wahubiri wa kike hawapaswi kutaja sehemu iliyo na habari juu ya Madani qafilah kutoka aya ya mwisho.)

1. Ndugu wapenzi wa Kiislamu, mwishoni mwa hotuba, ningependa kutaja ubora wa Sunnah na kutaja Sunnah na adabu chache. Mtume kipenzi صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenye kupenda Sunnah yangu ananipenda mimi, na mwenye kunipenda mimi atakuwa pamoja nami Peponi.' *(Ibn-e-Asakir, juz. 3, uk. 343)*

*Seenah tayri Sunnat ka Madinah banay Aaqa*

*Jannat mayn parosi Mujhay tum apna banana*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

2. Nunua na usome sehemu ya 16 ya Bahar-e-Shari'at, juz. 3 na kitabu chenye kurasa 120 'Sunnah na Adabu' kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah ili kujifunza Sunnah. Njia nyingine ya kujifunza Sunnah ni kusafiri na qafilah za Dawat-e-Islami pamoja na waja wa Mtume.

*Lootnay rahmatayn Qafilay mayn chalo*

*Seekhnay Sunnatayn Qafilay mayn chalo*

*Hon gi hal mushkilayn Qafilay mayn chalo*

*Khatam hoon shamatayn Qafilay mayn chalo*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

Baada ya kusoma kijitabu hiki, mpe mtu kwa nia ya kupata thawabu.

## Baada ya kusoma kijitabu hiki, wape wengine

Sambaza vitabu na vijitabu vyenye lulu za Madani vilivyochapishwa na Maktaba tul Madinah wakati wa harusi na mauti, katika maandamano ya ijtima'at, a'araas na Milad, n.k. na upate thawabu. Weka vijitabu mara kwa mara kwenye maduka yako ili kuwapa wateja wako kama zawadi kwa nia ya kupata thawabu. Tuma vitabu au vijitabu vyenye lulu za Madani kadiri unavyoweza kwenye nyumba za mtaa wako kupitia wachuuzi wa magazeti au watoto kila mwezi na ueneze wito wa kuelekea kwenye wema na upate thawabu nyingi.

# Bibliography


| Book | Publisher | Book | Publisher |
|---|---|---|---|
| Quran Pak | ………….. | Nuzha-tul-Qaari | Fareed Book Stall Lahore |
| Translation Kanz-ul-Iman | Maktaba-tul-Madinah Karachi | Fayz-ul-Qadeer | Dar-ul-Kutub Al-'Ilmiyyah Beirut |
| Tafseer Qurtubi | Dar-ul-Fikr Beirut | Al-Tayseer | Maktaba Imam Shafi'I Riyaz |
| Tafseer Mazhari | Ziya Al-Quran Publications | Haashiya Al-Hafni ala Al-Jami'-us-Sagheer | Matbu'ah Dar-ul-Nawadir |
| Bukhari | Dar-ul-Kutub Al-Ilmiyyah Beirut | Mirqat Al-Mafatih | Dar-ul-Fikr Beirut |
| Muslim | Dar-ul-Kitab Al-'Arbi Beirut | Ashi'a-tul-Lam'aat | Quita |
| Tirmizi | Dar-ul-Fikr Beirut | Mirqat-ul-Manajih | Ziya Al-Quran Publications Lahore |
| Abu Dawood | Dar-ul-Ihya Al-Tiras Al-'Arbi Beirut | Al-Hidaya | Dar-ul-Ihya Al-Tiras Al-Arabi Beirut |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ibn-e-Majah | Dar-ul-Ma'rifa Beirut | Johirah | Karachi |
| Mauta | Dar-ul-Ma'rifa Beirut | Fatawa 'Aalamgeeri | Dar-ul-Fikr Beirut |
| Musnad Ahmad Bin Hanbal | Dar-ul-Fikr Beirut | Durr Mukhtar | Dar-ul-Ma'rifa Beirut |
| Shu'ab-ul-Iman | Dar-ul-Kutub Al-'Ilmiyyah Beirut | Radd-ul-Muhtar | Dar-ul-Ma'rifah Beirut |
| Al-Mustadrak | Dar-ul-Ma'rifa Beirut | Tanveer Al-Absar | Dar-ul-Ma'rifah Beirut |
| Musnad Abu Ya'la | Dar-ul-Kutub Al-'Ilmiyyah Beirut | Haashiya Tahtawi ala Al-Maraqi | Karachi |
| Musnad Al-Bazar | Maktaba-ul-'Uloom wal Hikm Madinah Munawwarah | Al-Banaya | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut |
| Al-Firdaus bima Soor-ul-Khattab | Dar-ul-Kutub Al-'Ilmiyyah Beirut | Durar | Karachi |
| Mu'jam Kabeer | Dar-ul-Ihya Al-Tiras Al-'Arbi Beirut | Fatawa Qaazi Khan | Peshawar Pakistan |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mu'jam Awsat | Dar-ul-Fikr Beirut | Al-Tatar Khaniyyah | Karachi |
| Musannaf Abdul-Razzaq | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut | Al-Fatawa Al-Faqiyya-tul-Kubra | Dar-ul-Kutub Al-'Imiyyah Beirut |
| Musannaf Ibn Abi Shaybah | Dar-ul-Fikr Beirut | Jadd Al-Mumtar | Maktaba-tul-Madinah Karachi |
| Al-Jami-us-Sagheer | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut | Fatawa Razawiyyah | Raza Faundation Lahore |
| Jama'-ul-Jawami | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut | Bahar-e-Shari'at | Maktaba-tul-Madinah Karachi |
| Majma'-uz-Zawaaid | Dar-ul-Fikr Beirut | Jannati Zaywar | Maktaba-tul-Madinah Karachi |
| Kanz-ul-Ummal | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut | Tareekh Baghdad | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut |
| Attargheeb Watterheeb | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut | Ibn 'Asakir | Dar-ul-Fikr Beirut |
| Hilya-tul-Awliya | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut | Al-Tabqat Al-Kubra | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kitab-ul-Wara’ | Al-Maktaba Al-‘Asriyyah Beirut | Al-Durar Al-Kaaminah | Dar-ul-Ihya Al-Tiras ‘Arbi Beirut |
| Kitab-ul-Samat | Al-Maktaba Al-‘Asriyyah Beirut | Al-Shamail al-Muhammadiyyah | Dar-ul-Ihya Al-Tiras ‘Arbi Beirut |
| Al-Adab Al-Mufrad | Afseet Bi Madinah Tashqand | Sharh Al-Shifa | Dar-ul-Kutub Al-‘Ilmiyya Beirut |
| Maraseel Abi Dawood | Afghanistan | Subul Al-Huda | Dar-ul-Kutub Al-‘Ilmiyya Beirut |
| Umda-tul-Qaari | Dar-ul-Fikr Beirut | Seerat-e-Mustafa | Maktaba-tul-Madinah Karachi |
| Anwar Jamal-e-Mustafa | Shabbir Brothers Lahore | Al-Zawajir | Dar-ul-Ma’rifa Beirut |
| Manaqib Al-Imam Al-A’zam | Quetta | Kashf al-iltibas | Dar-ul-Ma’rifa Beirut |
| Hayat-e-A’la Hazrat | Maktaba-ul-Madinah Karachi | Al-Hasn Al-Haseen | Al-Maktaba Al-‘Asriyya Beirut |
| Qoot-ul-Quloob | Dar-ul-Kutub ‘Ilmiyyah Beirut | ‘Amal Al-Yaum wal layla | Dar Ibn Hazm |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ihya-ul-Uloom | Dar Sadir Beirut | Al-Maqasid-ul-Husna | Dar-ul-Kutub Al-'Ilmiyya Beirut |
| Ihya-ul-'Uloom (Urdu) | Maktaba-tul-Madinah Karachi | Ta'leem Al-Muta'allim | Karachi |
| Kimiya-e-Sa'adat | Intisharaat Ganjeenah Tehran | Ikram Al-Zayf | Maktaba Al-Sahabah Tanta Misr |
| Ithad-us-Sadat | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut | Hayat-ul-Haywan | Dar-ul-Kutub 'Ilmiyyah Beirut |
| Lawaqih-ul-Anwar | Dar-ul-Ihya Al-Tiras Al-Arabi Beirut | Islami Zindagi | Maktaba-tul-Madinah Karachi |
| Tanbih-ul-Ghafileen | Dar-ul-Kitab Al-'Arbi Beirut | Madani Wasiyyat Namah | Maktaba-tul-Madinah Karachi |
| Al-Budoor Al-Safirah | Mausista Al-Kutub Al-Shaqafiyyah Beirut | Hadaiq-e-Bakhshish | Maktaba-tul-Madinah Karachi |
| Sharh-us-Sudoor | Markaz-e-Ahl-e-Sunnat Barkat Raza Hind | Urdu Lughat | Urdu Lughat Board Karachi |

# Orodha Ya Yaliyomo

Ubora wa kumswalia Mtume Mtukufu ﷺ ........ 1
Sunna na Adabu 15 za Kutembea ........ 3
Adabu 7 za ........ 7
Kuvaa Viatu ........ 7
Sunna na Adabu 18 za ........ 9
kuketi ........ 9
Sunnah na Adabu 12 za Kuingia ........ 13
Sunnah na Adabu 15 kuhusu Majirani ........ 15
Sunnah na Adabu 13 za Kunywa Maji ........ 18
Maneno mawili yenye baraka ya Mustafa ﷺ ........ 18
Sunna na ........ 21
Adabu 32 za Kula Chakula ........ 21
Sunna na Adabu 30 za Ukarimu ........ 26
Sunnah na Adabu 13 za Kutendea ........ 32
Sunna na Adabu 11 za ........ 35
Sunna na Adabu 14 za kupeana mkono ........ 37
Sunna na Adabu 12 za Mazungumzo ........ 39
Sunna na Adabu 17 za ........ 41
Sunna na Adabu 4 za ........ 44
Sunna na Adabu 15 za ........ 45
Sunnah na adabu 22 kuhusu nywele na Mtindo wa nywele unaolingana na Sunnah n.k. ........ 47
Sunna na adabu 19 za kupaka mafuta na kuchana nywele. ........ 51
Sunna na Adabu 10 za ........ 59
Sunnah na Adabu 17 ........ 61
Sunnah na Adabu 25 zinazohusu ‘Imamah (Kilemba) ........ 65
Sunnah naAdabu 19 kuhusu uvaaji wa pete. ........ 68
Sunnah na Adabu 25 zinazohusu´Aqiyqah ........ 71

Sunnah na Adabu 18 za Kuweka Jina ........ 77
Sunna na Adabu 35 za Kusafiri ........ 82
Sunnah na adabu 33 za kumtembelea [mtu mgonjwa]........ 87
Sunnah na Adabu 16 zinazohusiana na sanda ........ 93
Nia ya kumvisha Sanda [marehemu] ........ 94
Sanda yenye kufuata mtindo wa Sunnah ........ 94
Maelezo ya Sanda ........ 95
Mbinu ya Kumfunika Marehemu ........ 96
Sunnah na Adabu 15 zinazohusu mazishi ........ 97
Sunna na Adabu 21 za ........ 105
Ombi kwa Wahubiri wa Kiume na Kike ........ 109
Baada ya kusoma kijitabu hiki, wape wengine ........ 111

# Method of taking the lead towards Paradise

Once, in an attempt to make two brothers who were annoyed with each other reconcile, Ala Hazrat رحمة الله عليه said: Whichever one of you takes the lead to reconcile will take the lead to Paradise.

*(Hayat-e-A'la Hazrat, vol. 1, p. 358)*

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran Purani Sabzi Mandi, Karachi, Pakistan
UAN +92 21 111 25 26 92 | Ext: 7213 +92 313-1139278
maktabatulmadinah.com Feedback@maktabatulmadinah.com